JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO




# MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/25

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS, TUME YA MIPANGO

# MPANGO WA MAENDELEO WA TAIFA WA MWAKA 2024/25

Juni, 2024

# Yaliyomo


Yaliyomo i
Orodha ya Vifupisho v
Muhtasari 1

**SURA YA KWANZA**
**Hali ya Uchumi** 6
1.1. Utangulizi 7
1.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi Kitaifa, Kikanda na Kimataifa 7
1.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia 7
1.2.2. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea 8
1.2.3. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi 8
1.2.4. Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara 8
1.2.5. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika 9
1.2.6. Mfumuko wa Bei wa Dunia 11
1.2.7. Mfumuko wa Bei wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika 12
1.2.8. Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki 12
1.3. Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa 13
1.3.1. Ukuaji wa Uchumi wa Taifa 13
1.3.2. Mfumuko wa Bei Nchini 16
1.3.3. Sekta ya Nje 17
1.3.4. Sekta ya Fedha 23
1.3.5. Deni la Serikali 28
1.3.6. Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu 31
*1.3.6.1 Ongezeko la Idadi ya Watu* 32
*1.3.6.2 Maendeleo ya Watu* 32
1.4. Tathmini ya Muda Mrefu ya Hali ya Uchumi wa Tanzania 34
1.5. Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024/25 38
1.5.1. Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla 39
1.5.2. Misingi (Assumptions) ya Mpango kwa Mwaka 2024/25 39

**SURA YA PILI**
**Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango** 40
2.1. Utangulizi 41
2.2. Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Kisekta Mwaka 2023/24 41
2.2.1. Sekta ya Usafirishaji na Uchukuzi 42
2.2.2. Sekta ya Nishati 48

2.2.3. Sekta ya Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano 52
2.2.4. Sekta ya Uzalishaji Viwandani 54
2.2.5. Sekta ya Kilimo 56
2.2.6. Sekta ya Mifugo 57
2.2.7. Sekta Ndogo ya Uvuvi 57
2.2.8. Sekta ya Madini 59
2.2.9. Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo 59
2.2.10. Sekta ya Utalii 60
2.2.11. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi 61
2.2.12. Biashara, Uwekezaji na Diplomasia ya Uchumi 62
2.2.13. Sekta ya Afya 63
2.2.14. Ustawi na Maendeleo ya Jamii 64
2.2.15. Sekta ya Elimu 65
2.2.16. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 67
2.2.17. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira 68
2.2.18. Utawala Bora na Utawala wa Sheria 69
2.2.19. Ujuzi na Uwezeshaji 71
2.2.20. Sekta ya Fedha 72
2.2.21. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi 73
2.3. Changamoto na Hatua za kukabiliana nazo katika utekelezaji wa Mpango wa 2023/24 77
2.3.1. Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24 77
2.3.2. Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto 77

**SURA YA TATU**
**Vipaumbele na Malengo Kwa Mwaka 2024/25** 78
3.1. Utangulizi 79
3.2. Mwelekeo wa Utekelezaji wa Miradi na Programu za Maendeleo kwa Mwaka 2024/25 80
3.2.1. Sekta ya Uchukuzi 81
3.2.2. Sekta ya Ujenzi 84
3.2.3. Sekta ya Nishati 86
3.2.4. Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari 88
3.2.5. Sekta ya Uzalishaji Viwandani 90
3.2.6. Sekta ya Kilimo 92
3.2.7 Sekta ya Mifugo 94
3.2.8. Sekta Ndogo ya Uvuvi 95
3.2.9. Sekta ya Madini 97
3.2.10. Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo 98

3.2.11. Sekta ya Utalii 100
3.2.12. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi 102
3.2.13 Biashara, Uwekezaji na Diplomasia ya Uchumi 103
3.2.14. Sekta ya Afya 106
3.2.15. Ustawi na Maendeleo ya Jamii 107
3.2.16. Sekta ya Elimu 108
3.2.17. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi 110
3.2.18. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira 111
3.2.19. Utawala Bora na Utawala wa Sheria 113
3.2.20. Ujuzi na Uwezeshaji 116
3.2.21. Sekta ya Fedha 119
3.2.22. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi 120
3.2.23. Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Uhamasishaji Uwekezaji nchini 120

**SURA YA NNE**

**Ufuatiliaji, Tathmini na Vihatarishi** 122
4.1 Utangulizi 123
4.2 Ufuatiliaji na Tathmini 123
4.3 Ufuatiliaji na Tathmini ya Programu na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2023/24 123
4.4. Ufuatitliaji na Tathmini kwa Mwaka 2024/25 125
4.4.1. Misingi na Mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini katika Mwaka 2024/2025 126
4.4.2. Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini 126
4.4.3. Mgawanyo wa Majukumu 126
4.5. Vihatarishi na Mikakati ya Kukabiliana Navyo kwa Mwaka 2024/2025 127
4.5.1 Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana Navyo 128
4.5.2. Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo 129

# Orodha ya Vifupisho

| | |
|---|---|
| **ADC** | Aquaculture Development Centres |
| **AFDP** | Agricultural and Fisheries Development Program |
| **ASDP II** | Agricultural Sector Development Programme II |
| **ATCL** | Air Tanzania Company Limited |
| **BAKITA** | Baraza la Kiswahili Tanzania |
| **BBT** | Building Better Tommorow |
| **BEVAC** | Beekeeping Value Chain Support |
| **CAMARTEC** | Centre For Agriculture Mechanization and Rural Technology |
| **CBE** | College of Bussiness Education |
| **CNG** | Compressed Natural Gas |
| **COSTECH** | Tanzania Commission for Science and Technology |
| **CRDB** | Cooperative and Rural Development Bank |
| **DART** | Dar es Salaam Rapid Transit |
| **DAWASA** | Dar es Salaam Water Supply and Sanitation Authority |
| **DC** | District Council |
| **DMDP** | Dar es Salaam Metropolitan Development Project |
| **DRC** | Democratic Republic of Congo |
| **DSE** | Dar es salaam Stock Exchange |
| **DUCE** | Dar es Salaam University College of Education |
| **EAC** | East Africa Community |
| **EACOP** | East Africa Crude Oil Project |
| **EIA** | Environment Impact Assessment |
| **EMU** | Electric Multiple Unit |
| **EP4R** | Education Program 4 Result |
| **FDC** | Folk Development Colleges |
| **FDI** | Foreign Direct Investment |
| **FYDP III** | Five Year Development Plan |
| **GEF** | Generation Equality Forum |
| **GDP** | Gross Domestic Product |
| **GePG** | Government Electronic Payment Gateway |
| **Ha** | Hacter |
| **HEET** | Higher Education for Economic Transformation |
| **HBS** | Household Budget Survey |

| | |
|---|---|
| **HDI** | Human Development Index |
| **HGA** | Host Government Agreement |
| **IAA** | Institute of Accountancy Arusha |
| **IFM** | Institute of Finance Management |
| **IMF** | International Monetary Fund |
| **IRDP** | Institute of Rural Development Planning |
| **JNHPP** | Julius Nyerere Hydropower Plant |
| **JNIA** | Julius Nyerere International Airport |
| **JV** | Joint Venture |
| **KIA** | Kilimanjaro International Airport |
| **KMTC** | Kilimanjaro Machine Tools |
| **KM** | Kilometer |
| **kV** | Kilovolt |
| **LNG** | Liquefied Natural Gas |
| **LTD** | Limited |
| **MCC** | Mbeya Cancer Centre |
| **MDAs** | Ministries, Departments and Agencies |
| **MGR** | Metre – Geuge Railways |
| **MOI** | Muhimbili Orthpaedic Institute |
| **NACP** | National AIDS Control Program |
| **NARCO** | National Ranching Company |
| **NEEC** | National Economic Empowerment Council |
| **NMB** | National Microfinance Bank |
| **NPMIS** | National Project Management Information System |
| **NRW** | Non-revenue Water |
| **OSC** | One Stop Facilitation Centre |
| **PFMRP** | Public Financial Management Reform Programme |
| **PPP** | Public-Private Partnership |
| **REA** | Rural Energy Agency |
| **REGROW** | Resilient Natural Resource Management for Tourism and Growth |
| **RISE** | Research on Improving Systems of Education |
| **RPC** | Regional Police Commissioner |
| **SACCOS** | Saving and Credit Cooperative Societies |
| **SADC** | Southern African Development Community |
| **SEQUIP** | Secondary Education Quality Improvement Project |
| **SEZ/EPZ** | Special Economic Zone/Export Processing Zone |

| | |
|---|---|
| **SGR** | Standard Gauge Railway |
| **SIDO** | Small Industries Development Organization |
| **SWASH** | School Water, Sanitation and Hygiene |
| **TACTIC** | Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness |
| **TADB** | Tanzania Agricultural Development Bank |
| **TAEC** | Tanzania Atomic Energy Commission |
| **TAFICO** | Tanzania Fisheries Corporation |
| **TaSUBa** | Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamoyo |
| **TATC** | Tanzania Automotive Technology Centre |
| **TAZARA** | Tanzania - Zambia Railway Authority |
| **TEA** | Tanzania Education Authority |
| **TEHAMA** | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| **TEMDO** | Tanzania Engineering and Manufacturing Design Organization |
| **TFSRP** | Tanzania Food System Resilience Program |
| **TIA** | Tanzania Institute of Accountancy |
| **TIRDO** | Tanzania Industrial Research and Development Organization |
| **TMX** | Tanzania Mercantile Exchange |
| **TPC** | Tanganyika Planting Company |
| **TVET** | Technical and Vocational Education and Training |
| **UCSAF** | Universal Communications Services Access Fund |
| **UMOCUltra** | Modern Oncology Centre |
| **U&T** | Ufuatiliaji na Tathmini |
| **UTT - AMIS** | Unit Trust of Tanzania- Asset Management and Investor Services |
| **UVIKO-19** | Ugonjwa wa Virusi vya Korona – 19 |
| **VAT** | Value Added Tax |
| **WEO** | World Economic Outlook |
| **WMA** | Weight and Measurement Agency |
| **WRRB** | Warehouse Receipt Regulatory Board |

# MUHTASARI

# USULI

Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 ni wa nne (4) katika utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26. Uandaaji wa Mpango huu umezingatia Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025 na Mpango Elekezi wa Maendeleo wa Miaka 15 wa mwaka 2011/12 – 2025/26. Serikali inaendelea na utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26 ambao ni wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Mpango huo wenye dhima ya ***"Kujenga Uchumi Shindani na Viwanda kwa Maendeleo ya Watu"*** umelenga kuchangia katika kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kwa kuongeza ufanisi na tija katika viwanda kwa kutumia rasilimali zinazopatikana kwa wingi nchini. Sambamba na hilo, maandalizi ya Mpango yamezingatia Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020, mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24, Mapendekezo ya Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2024/25 pamoja na nyaraka za kisera za kikanda na kimataifa ikiwemo: Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) 2050; Makubaliano ya Paris kuhusu Mabadiliko ya Tabianchi; Agenda 2063 ya Maendeleo ya Afrika; na Malengo ya Maendeleo Endelevu 2030.

Mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24 yamebainisha mafanikio katika sekta za kiuchumi na kijamii. Katika sekta ya afya, mafanikio hayo ni pamoja na kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano, kwa kila vizazi hai 1000 imepungua kutoka vifo 50 mwaka 2019/20 hadi kufikia vifo 43 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 88.9 ya lengo la kufikia vifo 40 ifikapo 2025/26; na kupungua kwa idadi ya vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kwa kila vizazi hai 100,000 kutoka vifo 220 mwaka 2019/20 hadi kufikia vifo 104 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 290 ya lengo la vifo 180 kufikia 2025/26. Katika sekta ya elimu, Serikali imeendelea kutoa elimu msingi na sekondari bila ada, kutoa ruzuku ya uendeshaji wa shule, kutoa posho ya madaraka kwa walimu wakuu 17,618 na maafisa elimu kata 3932, kutoa fidia ya ada kwa wanafunzi wa shule za bweni 218,473 na kutwa 2,831,006; Idadi ya wastani ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya ufundi imeongezeka kutoka wanafunzi 160,000 mwaka 2019/20 hadi

*Maandalizi ya Mpango yamezingatia Ilani ya uchaguzi ya Chama Cha Mapinduzi kwa ajili ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020*

**EAC** *Dira ya 2050*

SADC *Dira ya 2050*

*kupungua kwa idadi ya vifo vya watoto kutoka 50 kwa mwaka hadi 43*

*kupungua kwa idadi ya vifo vya wajawazito kutoka vifo 220 kwa mwaka hadi 104*

kufikia wanafunzi 235,804 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 14.0 ya lengo la kudahili wanafunzi 700,000 ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya wakufunzi kutoka wakufunzi 10,072 mwaka 2019/20 hadi kufikia 10,948 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la kufikia wakufunzi 15,000 ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya wahitimu wa vyuo vya ufundi na mafunzo kutoka 118,270 mwaka 2019/20 hadi kufikia 154,765 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la wahitimu 207,518 ifikapo mwaka 2025/26. Katika sekta ya maji, mafanikio yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa uwiano wa kaya za vijijini nchini zinazopata maji safi na salama kutoka katika vyanzo vilivyoboreshwa kutoka asilimia 36 mwaka 2019/20 hadi asilimia 56.1 mwaka 2022 sawa asilimia 52 ya kufikia lengo la asilimia 75 ifikapo 2025/26; na kuongezeka kwa asilimia ya watu katika mijini wanaopata maji safi na salama kutoka katika vyanzo vilivyoboreshwa kutoka asilimia 84 mwaka 2019/20 hadi kufikia asilimia 91.5 mwaka 2022 sawa na asilimia ya 68 kufikia lengo la asilimia 95 mwaka 2025/26.

Aidha, haya ni baadhi ya mafanikio mengi na makubwa yaliyopatikana, hata hivyo, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ili kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025.

*kutoa elimu msingi na sekondari bila ada*

*kutoa posho ya madaraka kwa walimu wakuu na maafisa elimu*

*kutoa fidia ya ada za shule za bweni na kutwa kwa wanafunzi*

*kuongezeka kwa idadi ya wahitimu wa vyuo vya ufundi na mafunzo*

*kuongezeka kwa uwiano wa kaya za vijijini na mijini zinazopata maji safi na salama*

*kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya ufundi*

*kuongezeka kwa idadi ya wakufunzi katika vyuo*

## Malengo na Shabaha ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa Mwaka 2024/25

Lengo kuu la Serikali katika Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/25 ni kukamilisha programu na miradi ya maendeleo ya kielelezo na kimkakati iliyopo katika hatua za mwisho za utekelezaji hususan miradi ambayo itawezesha sekta nyingine za kiuchumi na kijamii kustawi baada ya kukamilika. Utekelezaji wa Mpango wa mwaka 2024/25 katika usimamizi wa uchumi jumla unalenga: Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka asilimia ukuaji halisi wa asilimia 5.1 ya mwaka 2023; kuendelea kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati; Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.4 mwaka 2023/24; kuongeza mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka asilimia 12.6 mwaka ya 2023/24; kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

5.4%

*kuongeza kasi ya ukuaji wa pato halisi la taifa kufikia mwaka 2024.*

*kudhibiti kasi ya mfumuko wa bei*

*kuongeza pato la taifa kupitia mapato ya ndani*

*kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji*

## Maeneo ya Kipaumbele

Ili kuweza kufikia malengo na shabaha zilizobainishwa hapo juu Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 utajielekeza katika maeneo matano (5) ya kipaumbele ambayo kimsingi yameainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa 2021/22-2025/26 ambayo ni (i) Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi (ii) Kuimarisha Uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma (iii) Kukuza Biashara na Uwekezaji (iv) Kuchochea Maendeleo ya Watu na (v) Kuendeleza Rasilimali Watu.

***1. Kuchochea Uchumi Shindani***

***2. Kuimarisha uwezo wa Uzalishaji Viwandani na Utoaji Huduma***

***3. Kukuza Biashara na Uwekezaji***

***4. Kuchochea Maendeleo ya Watu***

***5. Kuendeleza Rasilimali Watu***

Aidha, msukumo zaidi umewekwa katika kukamilisha na kutekeleza miradi ya kielelezo na kimkakati ya miundombinu wezeshi katika sekta ya uchukuzi, usafiri na huduma za usafirishaji, sekta ya nishati, sekta ya mawasiliano na sekta ya maji, baadhi ya miradi hiyo kukamilisha ujenzi wa Reli kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR), miundombinu ya bandari, viwanja vya ndege, mtandao wa barabara za lami na madaraja, ufufuaji wa Shirika la Ndege Tanzania; kukamilisha mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere - MW 2,115, kukamilisha njia za kusafirisha umeme na vituo vya kupozea umeme, ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi la Afrika Mashariki kutoka Hoima (Uganda) hadi bandari ya Tanga eneo la Chongoleani na kuongeza kasi ya ujenzi na upanuzi wa Mtandao wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa ili kuharakisha mabadiliko ya kidigitali na mapinduzi ya nne ya viwanda nchini.

*Reli ya SGR*

*Miundombinu ya Bandari*

*Viwanja vya ndege*

*Mtandao wa Barabara za lami*

*Mradi wa kufua Umeme wa Maji Julius Nyerere*

*kukamilisha umeme na vituo vya kupozea umeme*

*ujenzi wa bomba la kusafirisha mafuta ghafi*

## Ugharamiaji wa Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa 2024/25

Katika Bajeti ya mwaka 2024/25 Serikali imetenga jumla ya shilingi shilingi bilioni 15,944.36 ya Bajeti ya Serikali kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali za maendeleo. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 12,303.52 ikijumuisha shilingi bilioni 1,189.08 za ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya elimu ya elimumsingi bure na Higher Education Students' Loans Board ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,640.84 ni fedha za nje. Aidha, Serikali itaongeza ushirikiano na ushiriki wa sekta binafsi katika kutekeleza na kugharamia miradi ya maendeleo kupitia njia bunifu na mbadala za ugharamiaji ikiwemo kupitia utaratibu wa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) ili kuongeza kasi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambayo tunakubaliana kuwa ndiyo injini ya ukuaji wa uchumi wa taifa letu.

**15,9 bil.**

*kugharamia shughuli za maendeleo*

**1,18 bil.**

*ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya elimu ya elimumsingi bure na HESLB. (fedha za ndani)*

## Maandalizi ya Mpango

Maandalizi ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 yameshirikisha wadau mbalimbali kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa, Taasisi na Mashirika ya Umma na Taasisi za Sekta Binafsi. Aidha, Washirika wa Maendeleo wameshirikishwa kupitia majadiliano katika maeneo mahsusi ya ushirikiano, ufadhili wa miradi ya maendeleo na programu za kisekta.

## Mpangilio wa Kitabu

Kitabu cha Mapendekezo ya Mpango kimegawanyika katika sura nne (4): Sura ya kwanza inaelezea hali ya uchumi; Sura ya pili inaelezea mapitio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/24; Sura ya tatu inaelezea Vipaumbele na Malengo kwa mwaka 2024/25; na Sura ya nne inaelezea maeneo ya ufuatiliaji, tathmini na vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango na hatua za kukabiliana navyo.

# HALI YA UCHUMI

# 01

# 1.1 UTANGULIZI

Mipango ya maendeleo ya Tanzania inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2000-2025. Pamoja na hatua zingine, Dira hii inalenga kuona kuwa Tanzania inafuzu kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 na kuwa na kiwango cha juu maendeleo ya watu. Katika kufikia Dira hii, Serikali imekuwa ikitekeleza Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano. Kwa sasa Serikali inatekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 -2025/26 wenye vipaumbele vitano, ambavyo ni kuchochea uchumi shirikishi na shindani, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza raslimali watu. Nguzo muhimu ya utekelezaji wa Mpango huu ni ukuaji wa uchumi. Taarifa hii inaeleza hatua zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana katika ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2023.

Sura hii inaelezea mwenendo wa viashiria vya uchumi kitaifa, kikanda, na dunia kwa mwaka 2023 pamoja na mwelekeo kwa mwaka 2024. Mwenendo wa viashiria hivyo unajenga mazingira muhimu yanayohitajika katika utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25. Viashiria vilivyofanyiwa mapitio ni pamoja na: pato la taifa; mfumuko wa bei; mwenendo wa sekta ya nje; sekta ya fedha; deni la Serikali; na viashiria vya maendeleo ya watu ikiwemo idadi ya watu na hali ya umaskini nchini.

## 1.2. Mapitio ya Hali ya Uchumi Kitaifa, Kikanda na Kimataifa

### 1.2.1. Ukuaji wa Uchumi wa Dunia

**3.2%**
**(2024 - 2025)**
*ukuaji wa uchumi wa dunia ni wa kiwango cha chini*

**3.8%**
**(2000 - 2019)**

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya mwezi Aprili 2024, matarajio ya msingi (baseline forecast) ni kuwa uchumi wa dunia utaendelea kukua kwa asilimia 3.2 mwaka wa 2024 na 2025, kwa kasi sawa na mwaka wa 2023. Matarajio haya ya ukuaji wa uchumi wa dunia kwa asilimia 3.2 ni wa kiwango cha chini ukilinganisha na wastani wa kihistoria wa miongo miwili iliyopita (2000-2019) wa asilimia 3.8. Kasi hii ndogo ya ukuaji wa uchumi hasa kwa mataifa yenye uchumi ulioendelea inaashiria

kuendelea kwa matumizi ya sera za fedha zenye mlengo wa kupunguza ujazo na ukwasi wa fedha katika uchumi na kupungua kwa misaada ya kibajeti (budget support) kwa nchi zinazoendelea kama Tanzania.

### 1.2.2. Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea kilipungua na kufikia asilimia 1.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 2.6 mwaka 2022. Ongezeko dogo la kasi ya ukuaji wa uchumi wa mataifa yaliyoendelea la asilimia 1.6 mwaka 2023 hadi matarajio ya asilimia 1.7 mwaka 2024 na asilimia 1.8 mwaka 2025, linasababishwa na madhara ya vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine ambayo kwa kiasi kikubwa imeyumbisha siyo tu uchumi wa nchi za Ulaya bali hata uchumi wa dunia nzima kutokana na kuongezeka kwa gharama za maisha kulikosababishwa na mfumuko wa bei za nishati barani Ulaya na bei za vyakula katika soko la dunia.

**1.6%**
**(2023)**
*kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi kimepungua*

**2.6%**
**(2022)**

### 1.2.3. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na zinazoibukia Kiuchumi

Kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi uliimarika na kufikia wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2023 ukilinganisha na asilimia 4.1 mwaka 2022. Hii inaashiria kuendelea kustahimili madhara yaliyotokana na vita kati ya Urusi na Ukraine ambayo yaliathiri uchumi wa nchi hizi. Ukuaji wa uchumi wa nchi hizi unatarajiwa kupungua na kufikia asilimia 4.2 mwaka 2024 na mwaka 2025. Aidha, kiwango cha ukuaji wa uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi za Bara la Asia, ikijumuisha China na India, kiliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 5.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.4 mwaka 2022.

**4.2%**
**(2024-2025)**
*kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi kinatarajiwa kupungua*

**4.3%**
**(2023)**
*kiwango cha ukuaji wa uchumi wa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi*


### 1.2.4. Uchumi wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kwa upande wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, ukuaji wa uchumi ulipungua kufikia wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 4.0 mwaka 2022. Upungufu huo ulitokana na utekelezaji wa sera ya kupunguza ujazi wa fedha kwenye uchumi wa Marekani ili kukabiliana na mfumuko wa bei katika nchi zilizoendelea na hivyo, kusababisha uhaba wa fedha za kigeni katika nchi zinazoendelea, hususan dola ya Marekani, kushuka kwa thamani ya fedha dhidi ya dola ya Marekani, kuongezeka kwa gharama za mikopo katika masoko ya fedha ya kikanda na kimataifa na kupungua kwa mauzo ya bidhaa kutoka nchi za Afrika kufuatia kupungua kwa uhitaji kutoka nchi washirika wakuu wa kibiashara. Aidha, uchumi kwa nchi za Afrika ulipungua kutokana na athari za muda mrefu za janga la UVIKO - 19 pamoja na uwiano hasi wa bei za bidhaa zinazouzwa na kununuliwa nje ya bara la Afrika. Aidha, uchumi wa nchi hizi unatarajiwa kuongezeka na kufikia ukuaji wa asilimia 3.8 mwaka 2024 na kuendelea kukua na kufikia asilimia 4.0 mwaka 2025. Kielelezo Na. 1.1 linaonesha mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa dunia na matarajio.

**3.4%**
**(2023)**
*ukuaji wa uchumi wa Nchi za kusini mwa jangwa la Sahara umeshuka*

**4.0%**
**(2022)**

Kielelezo Na. 1.1: Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi wa Dunia na Matarajio





***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF - WEO), Aprili 2024.*

### 1.2.5. Mwenendo wa Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika


Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili, 2024 kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kwa nchi za ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC) kilikuwa cha wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2022. Kupungua kwa ukuaji kulitokana na kuongezeka kwa mfumuko wa bei, kuongezeka kwa gharama za ukopaji katika masoko ya fedha ya kimataifa, kupungua kwa misaada na mikopo nafuu ya kibajeti, athari za mabadiliko ya tabianchi pamoja na athari za vita inayoendelea kati ya Urusi na Ukraine. Aidha, ukuaji wa uchumi kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashiriki (EAC) ulikuwa wa wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2022 kama inavyoonekana katika kielelezo Na.1.2 na 1.3.

Kielelezo Na. 1.2: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika




***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) toleo la Aprili, 2024*

**Kielelezo Na. 1.3: Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi Wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki**




***Chanzo:*** *Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) toleo la Aprili, 2024*

### 1.2.6. Mfumuko wa Bei wa Dunia

Mwaka 2023, mfumuko wa bei wa dunia ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 6.8 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 8.7 mwaka 2022. Kupungua kwa kasi ya ongezeko la bei za bidhaa na huduma duniani kulitokana na kuimarika kwa bei ya bidhaa, hususan nishati. Matarajio ya mfumuko wa bei wa Dunia utaendelea kupungua na kufikia asilimia 5.9 mwaka 2024 na asilimia 4.5 mwaka 2025. Aidha, mfumuko wa bei kwa nchi zilizoendelea ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2022. Vile vile, mfumuko wa bei kwa nchi zinazoendelea na zinazoibukia kiuchumi ulipungua na kufikia wastani wa asilimia 8.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 9.8 mwaka 2022.

**6.8%**
**(2023)**
*mfumuko wa bei wa dunia ulipungua*
**8.7%**
**(2022)**

### 1.2.7. Mfumuko wa Bei wa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika

Kwa mujibu wa taarifa ya Shirika la Fedha la Kimataifa (IMF) ya Aprili, 2024 mfumuko wa bei kwa nchi za Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika uliongezeka na kufikia wastani wa asilimia 16.2 mwaka 2023 ikilinganishwa na asilimia 14.5 mwaka 2022. Ongezeko la mfumuko wa bei lilitokana na sababu mbalimbali zikiwemo kupungua kwa ugavi wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya kikanda, kuongezeka kwa wastani wa bei za mafuta na mbolea kwa baadhi ya nchi hizo, pamoja na kasi ya kushuka kwa thamani ya sarafu kuliko ilivyotarajiwa. Nchi zilizokuwa na mfumuko wa bei wa juu ni pamoja na Zimbabwe (asilimia 667.4), Sudani ya Kusini (asilimia 40.2), Ghana (asilimia 37.5), Malawi (asilimia 30.3) na Ethiopia (asilimia 30.2). Aidha, kwa mwaka 2024 mfumuko wa bei kwa nchi hizo unatarajiwa kuwa wa wastani wa asilimia 15.3. Kwa upande wa mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika ulikuwa wastani wa asilimia 50.3 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 21.4 mwaka 2022.

**16.2%**
**(2023)**
*mfumuko wa bei wa kwa nchi za jumuiya ya maendeleo kusini mwa afrika umeongezeka*

**14.5%**
**(2022)**


### 1.2.8. Mfumuko wa Bei kwa Nchi za Ukanda wa Afrika Mashariki

Mwaka 2023, mfumuko wa bei kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 16.9 kutoka asilimia 8.3 mwaka 2022. Ongezeko hilo lilitokana na kupungua kwa ugavi wa mazao ya chakula katika baadhi ya masoko ya kikanda, kuongezeka kwa wastani wa bei za mafuta na mbolea kwa baadhi ya nchi. Aidha, kwa wastani, viwango vya mfumuko wa bei kwa nchi ya Tanzania, Kenya na Uganda ndivyo pekee viliendelea kuwa ndani ya lengo la Jumuiya la mfumuko usiozidi asilimia 8 kwa mwaka. Kielelezo Na.1.4 linaonesha mfumuko wa bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2023.

**16.9%**
**(2023)** *mfumuko wa bei wa kwa nchi za jumuiya ya afrika mashariki umeongezeka*

**8.3%**
**(2022)** *mfumuko wa bei wa kwa nchi za jumuiya ya afrika mashariki ulipungua*

Kielelezo Na. 1.4: Mfumuko wa Bei katika Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki kwa Mwaka 2023




***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa za Takwimu za nchi husika*

## 1.3. Mapitio ya Hali ya Uchumi wa Taifa

### 1.3.1. Ukuaji wa Uchumi wa Taifa


Mwaka 2023, Pato halisi la Taifa lilifikia shilingi bilioni 148,399.76 kutoka shilingi bilioni 141,247.19 mwaka 2022, sawa na ukuaji wa asilimia 5.1 ikilinganishwa na asimilia 4.7 mwaka 2022. Ukuaji huo ulichangiwa na: jitihada mbalimbali zilizochukuliwa na Serikali ikiwemo mikakati ya kukabiliana na athari za vita kati ya Ukraine na Urusi pamoja na uwekezaji wa kimkakati katika miundombinu ya nishati, maji, afya, elimu na usafirishaji; kuongezeka kwa uzalishaji wa madini, hususan dhahabu na makaa ya mawe; na kuongezeka kwa mikopo kwa sekta binafsi iliyochachua shughuli za kiuchumi. Hata hivyo, kiwango cha ukuaji wa Pato la Taifa kwa mwaka 2023 cha asilimia 5.1 kipo chini ya lengo la mwaka la asilimia 5.2. Hii ilitokana na: athari hasi ya vita kati ya Urusi na Ukraine, hususan kupanda kwa gharama za uzalishaji katika baadhi ya sekta; mabadiliko ya tabianchi yaliyoathiri uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa baadhi ya maeneo nchini



*mwaka 2023, pato halisi la taifa lilifikia **bilioni 148,399.76***

na kuharibu miundombinu ikiwemo madaraja na barabara; pamoja na hatua zilizochukuliwa na nchi zilizoendelea katika kukabiliana na mfumuko wa bei zilizosababisha kuongezeka kwa gharama za mikopo kutoka masoko ya kimataifa ya fedha na hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji.


**Kielelezo Na. 1.5: Mwenendo wa Ukuaji wa Pato la Taifa Mwaka 2018 - 2023**





| | 2018 | 2019 | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Q4(Kushoto) | 7.3 | 6.1 | 4.3 | 5.5 | 3.6 | 4.6 |
| Q3(Kushoto) | 7.3 | 8.0 | 5.4 | 5.4 | 5.2 | 5.3 |
| Q2(Kushoto) | 6.0 | 7.6 | 4.4 | 3.8 | 4.7 | 5.2 |
| Q1(Kushoto) | 7.5 | 6.3 | 5.3 | 4.9 | 5.5 | 5.4 |
| Mwaka (Kulia) | 7.0 | 6.9 | 4.5 | 4.8 | 4.7 | 5.1 |


***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

Mwaka 2023, sekta ya sanaa na burudani iliongoza kwa kuwa na ukuaji wa asilimia 17.7 ikifuatiwa na sekta ya fedha na bima asilimia 12.2, madini asilimia 11.3, malazi na huduma za chakula asilimia 8.3 pamoja na habari na mawasiliano asilimia 7.6 (Kielelezo Na. 1.2). Aidha, shughuli ya kilimo iliongoza kwa kuwa na mchango mkubwa kwenye Pato la Taifa wa asilimia 26.5 ikifuatiwa na ujenzi asilimia 13.2, madini asilimia 9.0 na biashara na matengenezo asilimia 8.3 (Kielelezo Na. 1.3).




**Kielelezo Na. 1.6: Ukuaji wa Pato la Taifa kwa Baadhi ya Shughuli za Kiuchumi (Asilimia)**




**Kielelezo Na. 1.7: Mchango wa Shughuli za Kiuchumi katika Pato la Taifa Mwaka 2023**




***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu, Mwaka 2023*

### 1.3.2. Mfumuko wa Bei Nchini

Mfumuko wa bei nchini ulifikia asilimia 3.1 katika kipindi kilichoishia mwezi Aprili 2024 ikilinganishwa na asilimia 4.3 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei ulifikia wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2023 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2022. Kiwango hiki ni cha chini ikilinganishwa na nchi wanachama wa EAC na kipo ndani ya malengo ya kati ya asilimia 3.0 hadi 7.0 na vigezo vya mtangamano wa kiuchumi kikanda (EAC na SADC). Kupungua kwa Mfumuko wa bei pamoja na mambo mengine kumetokana na utekelezaji madhubuti wa sera za fedha na bajeti na kuanza kuimarika kwa upatikanaji wa mazao ya chakula katika masoko ya ndani na ya nchi jirani.

**3.1%**
**(2024)**
*mfumuko wa bei nchini umeshuka*

**3.8%**
**(2023)**
*wastani wa mfumuko wa bei nchini*


**4.3%**
**(2022)**
*wastani wa mfumuko wa bei nchini*

Mfumuko wa bei kwenye vyakula na vinywaji baridi ulipungua kutoka asilimia 7.3 mwaka 2022 na kufikia asilimia 6.8 mwaka 2023. Aidha, mfumuko wa bei usiojumuisha vyakula na nishati (Core Inflation) ulifikia wastani wa asilimia 2.3 ikilinganishwa na asilimia 3.0 mwaka 2023 (Kielelezo Na. 3). Kwa upande mwingine mfumuko wa bei wa nishati, mafuta na bili za maji ulipungua kutoka asilimia 9.1 mwaka 2022 na kufikia asilimia 3.3 kwa mwaka 2023. Hii ilichangiwa kwa kiasi kikubwa na kupungua kwa bei ya nishati ya mafuta katika soko la dunia.

**6.8%**
**(2023)**

**7.3%**
**(2022)**
*mfumuko wa bei wa vyakula na vinywaji baridi ulipungua*

**Kielelezo Na. 1.8: Mwenendo wa Mfumuko wa Bei Nchini**




***Chanzo:*** *Ofisi ya Taifa ya Takwimu*

### 1.3.3. Sekta ya Nje

Sekta ya nje imeendelea kuimarika licha ya changamoto mbalimbali zilizoikumba dunia yaani magonjwa, vita, na kubadilika kwa sera za nchi zilizoendelea kulikopelekea kuongezeka kwa bei za bidhaa mbalimbali katika soko la dunia.

a. Urari wa Malipo ya Kawaida


Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, urari wa malipo yote ya nje uliimarika na kuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 1,616.4 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 3,977.8 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023. Mwenendo huu ulitokana na kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi sambamba na kupungua kwa gharama za uagizaji bidhaa na huduma nje ya nchi. Kupungua kwa nakisi ya malipo ya nje ni ishara nzuri kwa uchumi wa nchi, kwani inaweza kuonyesha kwamba nchi inakuwa na uwezo wa kudhibiti mahitaji yake ya fedha za kigeni na hata kujenga akiba ya fedha za kigeni. Hii ni muhimu katika kuhakikisha uthabiti wa kiuchumi na kifedha wa nchi.

b. Mwenendo wa Biashara ya Bidhaa na Huduma

i. Urari wa Biashara ya Bidhaa

Urari wa biashara ya bidhaa kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 4,533 ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 5,597.9 kwa kipindi kama hicho cha mwaka 2023. Hali hii ilichangiwa na kupungua kwa bei ya mafuta ya petroli na kupungua kwa bei na kiasi cha bidhaa za mbolea. Bidhaa nyingi ziliagizwa kutoka China, India, Falme za Kiarabu, Saudia Arabia, Japani na Afrika Kusini.

**Kielelezo Na. 1.9: Mchanganuo wa Uagizaji wa Bidhaa Nchini katika kipindi cha Julai hadi Machi mwaka 2024 (Asilimia)**





Aidha, hadi Machi 2024, thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi Ilikuwa dola za Marekani milioni 6,016.2, ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,629.2 kwa kipindi kama hicho mwaka 2023. Ongezeko hili lilichangiwa zaidi na mauzo ya dhahabu na bidhaa asilia, hususan tumbaku, korosho na kahawa, pamoja na mauzo ya mazao ya mboga na maua (Jedwali Na. 1.1). Aidha, bidhaa nyingi ziliuzwa katika nchi za India, Afrika Kusini, Falme za Kiarabu, Uswisi na China kama ilivyoainishwa katika kielelezo Na.1.10.

**$6,016m**
**(2024)**

*thamani ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi*

**$5,629m**
**(2023)**

**Kielelezo Na.1.10: Mchanganuo wa Masoko ya Bidhaa za Tanzania kwenda Nje ya Nchi katika kipindi cha Julai hadi Machi mwaka 2024 (Asilimia)**




**Jedwali Na. 1.1 Bidhaa Zilizouzwa Nje kwa kipindi cha Julai hadi Machi katika Mwaka 2020 hadi Mwaka 2024**

| Bidhaa | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Bidhaa Asilia (US$ milioni)** | | | | | | |
| **Kahawa** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 101.9 | 119.9 | 143.7 | 161.3 | 187.3 | 16.1 |
| Kiasi (‘000 tani) | 48.6 | 53.1 | 51.7 | 57.6 | 68.8 | 19.5 |
| Bei (US$ kwa tani) | 2,098.34 | 2,256.44 | 2,778.46 | 2,800.41 | 2,730.84 | -2.5 |
| **Pamba** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 114.6 | 50.0 | 79.2 | 104.3 | 106.2 | 1.8 |
| Kiasi (‘000 tani) | 100.7 | 41.6 | 45.4 | 50.3 | 76.6 | 52.4 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,138.40 | 1,203.72 | 1,745.00 | 2,075.50 | 1,380.67 | -33.5 |
| **Katani** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 13.5 | 14.5 | 14.5 | 21.1 | 14.0 | -33.6 |
| Kiasi (‘000 tani) | 8.5 | 9.2 | 9.1 | 12.8 | 9.0 | -29.2 |

| Bidhaa | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bei (US$ kwa tani) | 1,579.38 | 1,571.87 | 1,601.18 | 1,647.70 | 1,547.33 | -6.1 |
| **Chai** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 22.4 | 22.9 | 22.3 | 20.6 | 18.2 | -11.8 |
| Kiasi ('000 tani) | 16.2 | 17.4 | 16.1 | 13.7 | 14.3 | 4.3 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,378.63 | 1,319.26 | 1,382.80 | 1,503.64 | 1,283.54 | -14.6 |
| **Tumbaku** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 164.7 | 90.7 | 136.5 | 163.2 | 369.7 | 126.5 |
| Kiasi ('000 tani) | 47.9 | 24.7 | 41.5 | 43.2 | 85.7 | 98.2 |
| Bei (US$ kwa tani) | 3,435.73 | 3,679.22 | 3,292.63 | 3,776.63 | 4,255.01 | 12.7 |
| **Korosho** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 497.1 | 232.8 | 194.4 | 164.3 | 224.6 | 36.8 |
| Kiasi ('000 tani) | 418.8 | 214.2 | 191.9 | 171.7 | 242.8 | 41.4 |
| Bei (US$ kwa tani) | 1,186.79 | 1,086.66 | 1013.5155 | 956.94167 | 616.38691 | -35.6 |
| **Karafuu** | | | | | | |
| Thamani (US$ milioni) | 22.5 | 1.5 | 60.6 | 37.2 | 30.7 | -17.4 |
| Kiasi ('000 tani) | 4.7 | 0.3 | 8.7 | 5.6 | 4.6 | -17.7 |
| Bei (US$ kwa tani) | 4,762.07 | 4,686.05 | 6,978.03 | 6,612.56 | 6,017.56 | -9.0 |
| Jumla (Bidhaa Asilia) | 936.6 | 532.3 | 651.4 | 672.0 | 950.8 | 41.5 |
| **Bidhaa Zisizo Asilia (US$ millioni)** | | | | | | |
| Madini | 1,944.0 | 2,478.8 | 2,357.0 | 2,698.4 | 2,652.8 | -1.7 |
| Dhahabu | 1,872.3 | 2,306.3 | 1,952.1 | 2,150.1 | 2,347.5 | 9.2 |
| Almasi | 43.7 | 5.5 | 18.4 | 46.4 | 29.9 | -35.5 |
| Madini mengine | 28.0 | 167.0 | 386.5 | 502.0 | 275.4 | -45.1 |
| Bidhaa za Viwandani | 610.0 | 826.8 | 933.4 | 1064.9 | 1035.7 | -2.7 |
| Nyuzi za Pamba | 5.9 | 5.0 | 1.7 | 1.3 | 0.4 | -66.5 |
| Kahawa iliyozalishwa | 1.0 | 8.3 | 20.8 | 9.3 | 5.1 | -45.5 |
| Tumbaku iliyozalishwa | 16.3 | 13.8 | 29.6 | 28.4 | 30.1 | 5.9 |
| Mazao ya Katani | 14.9 | 23.1 | 26.5 | 21.7 | 21.3 | -1.9 |
| Mazao mengine ya Viwandani | 571.9 | 776.5 | 854.8 | 1004.1 | 978.8 | -2.5 |

| Bidhaa | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Samaki na Mazao ya Samaki | 112.2 | 103.3 | 129.1 | 120.5 | 122.5 | 1.6 |
| Mazao ya Mboga na Maua | 162.3 | 268.3 | 315.9 | 244.0 | 367.8 | 50.7 |
| Bidhaa zilizouzwa tena (re-exports) | 135.4 | 66.8 | 83.6 | 103.7 | 85.9 | -17.1 |
| Bidhaa nyinginezo | 279.9 | 413.9 | 576.8 | 409.4 | 467.2 | 14.1 |
| Jumla (Bidhaa zisizo Asilia) | 3,243.78 | 4,157.80 | 4,395.80 | 4,640.91 | 4,731.89 | 2.0 |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 382.2 | 407.3 | 421.1 | 316.3 | 333.5 | 5.4 |
| **Jumla Kuu (Bidhaa Zote)** | **4,562.63** | **5,097.37** | **5,468.30** | **5,629.20** | **6,016.16** | **6.9** |

***Chanzo:*** *Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki kuu ya Tanzania*

**Jedwali Na. 1.2 Thamani ya Bidhaa Zilizoagizwa kutoka Nje kwa kipindi cha Julai hadi Machi katika Mwaka 2020 hadi Mwaka 2024**

| Bidhaa | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa za Kukuza Mitaji | 2,668.9 | 2,446.4 | 3,163.9 | 4,104.3 | 4,279.2 | 4.3 |
| Vifaa vya Usafirishaji | 669.1 | 601.2 | 761.4 | 1,222.8 | 1,203.2 | -1.6 |
| Majengo na Ujenzi | 838.5 | 689.6 | 1,020.2 | 1,025.9 | 1,274.0 | 24.2 |
| Mitambo | 1,161.2 | 1,155.6 | 1,382.3 | 1,855.6 | 1,802.0 | -2.9 |
| | | | | | | |
| Bidhaa za Kati | 2,091.8 | 1,783.7 | 2,766.2 | 4,192.4 | 3,464.3 | -17.4 |
| Uagizaji Mafuta | 1,366.3 | 1,053.7 | 1,793.2 | 2,832.6 | 2,357.6 | -16.8 |
| Mbolea | 136.1 | 125.2 | 176.5 | 562.0 | 270.4 | -51.9 |
| | | | | | | |
| Malighafi za Viwanda | 589.4 | 604.9 | 796.5 | 797.8 | 836.3 | 4.8 |
| Bidhaa za Matumizi ya Kawaida | 1,933.5 | 1,924.8 | 2,463.2 | 2,928.8 | 2,804.0 | -4.3 |

| Bidhaa | 2020 | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | Badiliko (Asilimia) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Bidhaa za Vyakula | 355.3 | 279.3 | 444.5 | 655.2 | 670.6 | 2.4 |
| Bidhaa Nyingine | 1,578.2 | 1,645.5 | 2,018.7 | 2,273.6 | 2,133.4 | -6.2 |
| Bidhaa zisizo rekodiwa | 1.6 | 1.6 | 1.6 | 1.6 | 1.6 | 0.0 |
| **Jumla (FoB)** | **6,695.8** | **6,156.5** | **8,394.9** | **11,227.1** | **10,549.2** | **-6.0** |

***Chanzo:*** *Mamlaka ya Mapato Tanzania na Benki kuu ya Tanzania*

ii. Urari wa Biashara ya Huduma

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ziada ya urari wa biashara ya huduma iliongezeka kwa asilimia 65.2 na kufikia dola za Marekani milioni 3,557.2 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,153.7 mwaka 2023. Hii ilichangiwa na kuongezeka kwa mapato yatokanayo na shughuli za utalii kutokana na kuimarika kwa sekta hiyo, pamoja na kuongezeka kwa mapato ya huduma za usafirishaji. Katika kipindi hicho, mapato yanayotokana na utalii yaliongezeka kwa asilimia 27.8 na kufikia dola za Marekani milioni 2,927.7 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 2,291.4, wakati idadi ya watalii ilikuwa 1,569,206 ikilinganishwa na watalii 1,288,605. Aidha, shughuli za utalii na usafirishaji zilichangia asilimia 92.4 ya biashara yote ya huduma.

iii. Urari wa Biashara ya Bidhaa na Huduma

Urari wa biashara ya bidhaa na huduma ulikuwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 975.8 kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Machi 2024, ikilinganishwa na nakisi ya dola za Marekani milioni 3,444.2 kwa kipindi kama hicho mwaka uliotangulia. Kupungua huko kulichangiwa na kuongezeka zaidi kwa mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi pamoja na kushuka kwa gharama za uagizaji bidhaa nje ya nchi. Aidha, kupungua kwa nakisi ya biashara kunaweza kuwa ishara nzuri kwa uchumi, kwani inaweza kupunguza utegemezi wa nchi kwa fedha za kigeni na kusaidia kustawisha shughuli za kiuchumi ndani ya nchi.

d. Akiba ya Fedha za Kigeni

Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kuridhisha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Hadi kufikia Machi 2024, Kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani milioni 5,327.1 ikilinganishwa na dola za Marekani milioni 5,012.5 kipindi kama hicho mwaka 2023. Kiasi hicho kinatosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi 4.4, zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua minne.

### 1.3.4. Sekta ya Fedha

a. Mwenendo wa Viwango vya Riba

Katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024, wastani wa riba ya jumla katika soko la fedha baina ya mabenki ulifikia asilimia 6.34 ikilinganishwa na asilimia 4.79 kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Aidha, riba ya jumla ya dhamana za Serikali za muda mfupi ilifikia asilimia 9.51, ikilinganishwa na asilimia 5.57 kwa kipindi kama hicho kwa mwaka 2023. Benki Kuu kwa kushirikiana na wadau mbalimbali imeendelea na jitihada za kupunguza viwango vya riba za mikopo, ikiwemo kuhakikisha wananchi wengi wanapata na kuzifikia huduma rasmi za kifedha. Viwango vya riba za mikopo vilipungua ambapo wastani wa riba za jumla za mikopo ulikuwa asilimia 15.49 ikilinganishwa na asilimia 16.18 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Viwango vya riba za mikopo ya mwaka mmoja vilipungua na kufikia wastani wa asilimia 16.53 ikilinganishwa na asilimia 16.05 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Viwango vya riba za mikopo kwa kipindi cha mwaka mmoja vimeendelea kupungua na kufikia wastani wa asilimia 16.09 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 16.90 katika kipindi kama hicho mwaka 2022/23. Kupungua kwa viwango vya riba za mikopo ya mwaka mmoja kunaweza kuashiria sera za kifedha zinazolenga kupunguza gharama za kukopa na kukuza ukuaji wa uchumi. Hii inaweza kufanya mikopo iwe nafuu zaidi kwa wakopaji na kuchochea matumizi na uwekezaji. Aidha, wastani wa riba za amana za muda maalum uliongezeka hadi asilimia 7.25 kutoka asilimia 7.23 katika kipindi kama hicho 2022/23. Kwa upande mwingine, wastani wa riba za amana za mwaka mmoja uliongezeka na kufikia asilimia 8.91 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na asilimia 8.61 mwaka 2022/23. Ongezeko la viwango vya riba za amana za mwaka mmoja linaweza kuwa juhudi za kuvutia wawekezaji kwa kutoa faida zaidi kwa amana zilizowekwa kwa muda mrefu.

| 6.34% | 4.79% |
| --- | --- |
| **(2023/24)** | **(2022/23)** |
| *wastani wa riba ya jumla katika soko la fedha baina ya mabenki* | *wastani wa riba ya jumla katika soko la fedha baina ya mabenki* |

b. Ujazi wa Fedha na Karadha

Utekelezaji wa sera ya fedha katika kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 uliweza kufikia malengo yaliyokusudiwa, licha ya kukabiliwa na changamoto zilizotokana na mwenendo usioridhisha wa uchumi wa dunia. Ukwasi katika uchumi ulitosheleza mahitaji ya shughuli za uzalishaji na kuwezesha benki za biashara kutoa mikopo kwa sekta binafsi. Ujazi wa fedha kwa tafsiri pana zaidi (M3) ulikua kwa wastani wa asilimia 10.9 kufikia shillingi billion 44,318.4 ukilinganisha na shillingi billioni 39,961.5, kipindi kama hicho mwaka 2023. Aidha, ujazi wa fedha kwa tafsiri pana (M2) ulikuwa kwa wastani wa asilimia 8.9 kufikia shillingi billioni 33,824.8, ikilinganishwa na shillingi billioni 31,048.8 katika kipindi

kama hicho mwaka 2023. Vilevile, ujazi wa fedha kwa tasfiri finyu (M1) uliongezeka kwa asilimia 5.3 kufikia shilingi bilioni 20,263.6 katika kipindi kinachoishia Aprili 2024, ikilinganishwa na shillingi billioni 19,248.3, katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Hali hiyo ya kuongezeka kwa ujazi wa fedha kwa tafsiri zote tatu inaashiria kuimarika kwa shughuli za uchumi unaochangiwa na ukuaji wa mikopo ya sekta binafsi uliojielekeza kukuza uzalishaji na ajira, uwekezaji na kuongeza matumizi katika bidhaa na huduma. Hivyo, inatoa fursa kwa Serikali kuendelea kuimarisha sera za fedha katika kukuza uchumi na kusaidia ukuaji wa sekta binafsi

c. Mikopo kwa Sekta Binafsi

Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili, 2024, mikopo katika sekta binafsi imeendelea kuwa imara hadi kufikia ukuaji wa shillingi billioni 33,746.5, sawa na asilimia 17.6, kutoka ukuaji wa shillingi billioni 28,702.9, katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Ukuaji huo ulitokana na maboresho katika mazingira ya biashara na kuimarika kwa shughuli za kiuchumi nchini. Aidha, mikopo kwa sekta ya kilimo ilikua kwa asilimia 60.6, kutokana na matokeo ya hatua za kisera zilizolenga kushusha viwango vya riba pamoja na juhudi za Serikali kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo. Vilevile, mikopo katika sekta ya viwanda na uzalishaji ulikua kwa asilimia 29.1, uchimbaji madini (asilimia 18.1), na mikopo kwa shughuli binafsi asilimia 16.7. Katika kipindi hicho, sehemu kubwa ya mikopo iliendelea kuelekezwa katika shughuli binafsi (biashara ndogo na za kati), sawa na asilimia 37.0 ya mikopo yote, ikifuatiwa na shughuli za biashara asilimia 12.8, kilimo asilimia 11.6 na viwanda asilimia 10.2. Matokeo hayo yanaonesha mwelekeo chanya katika ukuaji wa uchumi na maendeleo ya sekta mbalimbali nchini. Ongezeko la mikopo kwa sekta binafsi, hususan katika sekta za kilimo, viwanda na uzalishaji, na uchimbaji madini, linaashiria uimarishaji wa mazingira ya biashara na ukuaji wa shughuli za kiuchumi. Hatua za kisera zilizolenga kupunguza viwango vya riba na kuongeza bajeti katika sekta muhimu kama kilimo zimeonekana kuwa na matokeo chanya katika kuchochea ukuaji huu.

d. Mwenendo wa Thamani ya Shilingi

Mwenendo wa thamani ya shilingi iliendelea kuwa tulivu licha ya changamoto mbalimbali zinazoikumba dunia ikiwemo utekelezaji wa sera ya fedha katika nchi zilizoendelea uliolenga kupunguza ukwasi katika kukabiliana na mfumuko wa bei. Katika kipindi cha mwezi Julai hadi Aprili 2024, dola moja ya Marekani ilibadilishwa kwa wastani wa shilingi 2,501.38 ikilinganishwa na shilingi 2,319.80 katika kipindi sawia mwaka 2023. Katika kuendelea kuimarisha utulivu wa shilingi, Benki Kuu ilichukua hatua mbalimbali zilizowezesha kuongeza fedha za kigeni katika soko, ikiwemo kuuza dola pamoja na kutekeleza sera ya fedha yenye lengo la kupunguza ukwasi wa shilingi. Hali hii imesaidia nchi kuwezesha wafanyabishara kuwa na uhakika wa kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje pamoja na kuvutia uwekezaji na utalii.

**(2024)** **$ 1 – ⇄ – 2,501**


*dola moja ya kimarekani kwa shilingi ya kitanzania*

**(2023)** **$ 1 – ⇄ – 2,319**

*dola moja ya kimarekani kwa shilingi ya kitanzania*

e. Mikopo Chechefu

Katika kipindi kinachoishia mwezi Aprili, 2024, kiwango cha mikopo chechefu kilipungua na kufikia asilimia 4.3 ikilinganishwa na asilimia 5.5 mwaka 2023. Kupungua kwa mikopo chechefu kulitokana na hatua mbalimbali zilizoendelea kuchukuliwa na Benki Kuu ya Tanzania zikiwemo: kuongeza ufuatiliaji wa utoaji mikopo na kuwaondoa wafanyakazi wa benki wasio waaminifu; kuzielekeza benki kutumia ripoti za mikopo kutoka kwa kampuni za kuchakata na kutunza kumbukumbu za mikopo; utekelezaji wa kanuni za kuwalinda walaji/watumiaji wa huduma za benki kwa kuhakikisha utunzaji wa haki na usawa kwa wakopaji; na kuzitaka benki na taasisi za fedha kuimarisha taratibu za utoaji na ufuatiliaji wa mikopo. Aidha, idadi ya taasisi zilizotumia kanzidata ya wakopaji iliongezeka na kufikia 185 Aprili 2024 ikilinganishwa na taasisi 182 Aprili 2023. Vilevile, idadi ya wakopaji waliosajiliwa kwenye kanzidata ya wakopaji iliongezeka na kufikia 8,958,203 ikilinganishwa na wakopaji 5,650,384 Aprili 2023.




f. Ukwasi na Faida za Biashara katika Benki

Sekta ya fedha imeendelea kuwa imara huku viashiria hatarishi vikipungua kutokana na matarajio ya kuendelea kuimarika kwa uchumi. Sekta ya kibenki ambayo ni sehemu kubwa ya sekta ya fedha imeendelea kuwa imara, yenye kutengeneza faida, ukwasi na mtaji wa kutosha. Amana, mikopo na rasilimali pia ziliendelea kuongezeka. Uwiano wa mtaji wa msingi kwa rasilimali zote ulifikia asilimia 19.4 mwezi Aprili 2024, ikilinganishwa na kiwango kinachokubalika kisheria cha asilimia 10. Aidha, uwiano wa ukwasi wa sekta ya benki kiujumla (Liquid Assets to Demand Liabilities) ulikuwa asilimia 25.5 mwezi Aprili 2024 ikilinganishwa na asilimia 25.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023. Uwiano huu ulikuwa juu ya kiwango cha chini kinachokubalika kisheria cha angalau asilimia 20 na hivyo kuendelea kuwa toshelevu kwa mahitaji ya shughuli mbalimbali za kiuchumi. Sekta ya benki imeendelea kutengeneza faida, ambapo faida baada ya kodi (kabla ya ukaguzi wa mahesabu) kwa miezi minne 2024 ilifikia shilingi bilioni 729.6 kutoka shilingi bilioni 447.8 miezi minne ya mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 62.9.

g. Soko la Upili la Hatifungani

### Mauzo ya Hatifungani za Serikali

Mauzo ya hatifungani za Serikali zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Aprili 2024 yaliongezeka kwa asilimia 60.75 na kufikia shilingi trilioni 3.90, ikilinganishwa na shilingi trilioni 2.43 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Aprili 2023. Kuongezeka kwa mauzo ya

hatifungani za Serikali kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa kushirikiana na wadau wengine.

### Mauzo ya Hatifungani za Kampuni

Mauzo ya hatifungani za kampuni zilizoorodheshwa kwenye Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Aprili 2024 yaliongezeka kwa asilimia 186.01 na kufikia shilingi bilioni 2.89, ikilinganishwa na shilingi bilioni 1.01 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Aprili 2023. Kuongezeka kwa mauzo ya hatifungani za Kampuni kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa kushirikiana na wadau wengine.

### Mauzo ya Hisa (Equity Turnover)

Mauzo ya hisa katika Soko la Hisa Soko la Hisa la Dar es Salaam katika kipindi kilichoishia Aprili 2024 yaliongezeka kwa asilimia 146.86 na kufikia shilingi bilioni 267.53, ikilinganishwa na shilingi bilioni 108.38 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Aprili 2023. Kuongezeka kwa mauzo ya hisa kumetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana kwa kushirikiana na wadau wengine.

### Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja

Mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja katika kipindi kilichoishia Aprili 2024 ulikuwa mzuri. Thamani ya uwekezaji katika mifuko ya uwekezaji wa pamoja iliongezeka kwa asilimia 44.73 na kufikia shilingi trilioni 2.10 katika kipindi kilichoishia Aprili 2024, ikilinganishwa na shilingi trilioni 1.45 katika kipindi kilichoishia Aprili 2023. Ongezeko hili limetokana na kuongezeka kwa ushiriki wa wawekezaji kutokana na elimu inayotolewa na Serikali kupitia Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA) kwa kushirikiana na wadau wengine, pamoja na matumizi ya teknolojia katika utoaji wa huduma kwa wawekezaji. Jedwali lifuatalo linaonesha mwenendo wa uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja.

**Jedwali 1.3: Mwenendo wa Uwekezaji katika Mifuko ya Uwekezaji wa Pamoja**

| Meneja wa Mifuko | Jina la Mfuko | 31 Desemba 2022 | | 31 Desemba 2023 | | Ongezeko la Thamani | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Thamani ya Mfuko | Bei ya Kipande (Shilingi) | Thamani ya Mfuko (Shilingi) | Bei ya Kipande (Tsh) | Ongezeko la Thamani ya Mfuko | Ongezeko la bei ya Kipande |
| UTT Amis Plc | Mfuko wa Umoja | 351,843,423,644.70 | 1017.7875 | 314,225,287,302.81 | 911.8869 | 11.97% | 11.61% |
| | Mfuko wa Wekeza Maisha | 14,006,304,687.19 | 892.2839 | 8,405,578,297.45 | 777.366 | 66.63% | 14.78% |
| | Mfuko wa Watoto | 17,592,710,639.78 | 654.5292 | 9,967,538,940.30 | 574.64 | 76.50% | 13.90% |
| | Mfuko wa Jikimu | 25,062,884,535.00 | 170.6146 | 19,741,990,950.31 | 161.2614 | 26.95% | 5.80% |
| | Mfuko wa Ukwasi | 1,039,036,641,413.48 | 398.4238 | 682,986,408,123.98 | 355.2832 | 52.13% | 12.14% |
| | Mfuko wa Hatifungani | 627,363,482,005.86 | 116.9688 | 398,615,781,444.29 | 115.4104 | 57.39% | 1.35% |
| Watumishi Housing Investments | Mfuko wa Faida | 21,885,434,145.49 | 114.00000 | 14,800,921,479.37 | 103.2586 | 47.87% | 10.40% |
| **Thamani ya Jumla** | | **2,096,790,881,071.49** | | **1,448,743,506,538.52** | | **44.73** | |

***Chanzo:*** *UTT AMIS Plc*

h. Mwenendo wa Soko la Hisa

Mwenendo wa biashara katika soko la hisa hupimwa kwa kuangalia viashiria ambavyo huonyesha mwelekeo wa ufanisi wa soko. Viashiria hivyo ni pamoja na: Mtaji wa Soko (Market Capitalisation); Fahirisi za Soko (Share Index); Mauzo katika Soko la Hisa; na Ushiriki kwenye Soko la Hisa. Katika kipindi kilichoishia Aprili, 2024 mwenendo wa Soko la Hisa la Dar es Salaam ulikuwa mzuri. Ufanisi huu umetokana na juhudi za Serikali katika kutoa elimu kuhusu fursa na faida za kuwekeza katika masoko ya mitaji.

### Mtaji wa Soko la Hisa

Mtaji wa Jumla wa Soko la Hisa yaani Total Market Capitalisation katika kipindi kilichoishia Aprili 2024 uliongezeka kwa asilimia 6.68 na kufikia shilingi trilioni 16.61 ikilinganishwa na shilingi trilioni

15.57 katika kipindi kilichoishia Aprili 2023. Aidha, Mtaji wa Soko la Hisa kwa kampuni za ndani yaani Domestic Market Capitalisation katika kipindi kilichoishia Aprili 2024 uliongezeka kwa asilimia 7.14 na kufikia shilingi trilioni 11.78 ikilinganishwa na shilingi trilioni 10.99 katika kipindi kilichoishia Aprili 2023. Kuongezeka kwa mtaji wa Soko la Hisa kumetokana na kuongezeka kwa bei ya hisa za kampuni zilizoorodheshwa DSE ambazo zinatoa huduma katika sekta za viwanda na fedha. Kampuni hizo ni pamoja na CRDB Bank Plc, NMB Bank Plc, DSE Plc, National Investment Company Limited (NICO), Swissport Tanzania Plc, Twiga Cement Plc, Tanga Cement Plc, Tanzania Breweries Plc na Tanzania Cigarette Plc.

### Fahirisi ya Soko (Market Index)

Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni zote yaani All Share Index katika kipindi kilichoishia Aprili 2024, iliongezeka kwa asilimia 6.59 na kufikia alama 1,990.21 ikilinganishwa na alama 1,867.18 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Aprili 2023. Aidha, Fahirisi ya soko kwa hisa za kampuni za ndani yaani Tanzania Share Index (TSI) katika kipindi kilichoishia Aprili 2024, iliongezeka kwa asilimia 7.0 na kufikia alama 4,445.50 ikilinganishwa na alama 4,154.18 zilizorekodiwa katika kipindi kilichoishia Aprili 2023. Kuongezeka kwa Fahirisi ya soko kunaashiria ufanisi wa soko la hisa kwa kampuni zilizoorodheshwa katika soko la hisa hususan kuongezeka kwa bei ya hisa za baadhi ya kampuni zilizoorodheshwa DSE ambazo zinatoa huduma katika sekta za viwanda na fedha.


### 1.3.5. Deni la Serikali

Hadi Machi 2024, deni la Serikali lilikuwa shilingi bilioni 91,708.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 77,010.4 katika kipindi kama hicho mwaka 2023, sawa na ongezeko la asilimia 19.1. Kati ya kiasi hicho, deni la ndani lilikuwa shilingi bilioni 30,753.8 na deni la nje lilikuwa shilingi bilioni 60,954.5. Aidha, ongezeko la deni lilitokana na Serikali kuendelea kupokea fedha za mikopo ya zamani na mipya kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya kugharamia miradi ya maendeleo, ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya barabara, reli, viwanja vya ndege, umeme na maji. Vile vile, ongezeko la deni lilichangiwa na kupanda kwa viwango vya kubadilisha fedha pamoja na kuongezeka kwa riba kwenye mikopo ya nje ambayo riba zake hutegemea mabadiliko ya hali ya soko (floating rates).

**Machi 2024**
**91,708 bil.**
*deni la Serikali*

**Machi 2023**
**77,010 bil.**
*deni la Serikali*

**Kielelezo Na. 1.11: Mwenendo wa Deni la Serikali Machi 2017 - 2024 (Shilingi Bilioni)**




| | Machi **2017** | Machi **2018** | Machi **2019** | Machi **2020** | Machi **2021** | Machi **2022** | Machi **2023** | Machi **2024** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni la Ndani | 12,074 | 14,159 | 13,133 | 14,731 | 16,117 | 21,778 | 26,852 | 30,754 |
| Deni la Nje | 12,074 | 35,730 | 37,639 | 40,245 | 12,074 | 47,483 | 50,159 | 60,954 |
| Deni la Serikali | 12,074 | 49,728 | 50,772 | 54,967 | 12,074 | 69,261 | 77,010 | 91,708 |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha*

Matokeo ya tathmini ya Uhimilivu wa Deni iliyofanyika Desemba 2023 yalionesha kuwa deni ni himilivu kwa kipindi cha muda mfupi, wa kati na mrefu. Tathmini hiyo hufanyika kwa kuzingatia vigezo vya uhimilivu ambavyo ni uwiano wa deni halisi kwa Pato la Taifa, uwiano wa deni halisi kwa malipo ya nje na uwiano wa malipo ya deni kwa mapato ya ndani na mapato yatokanayo na mauzo ya nje.

Viashiria vya deni vilionesha kuwa kwa mwaka 2023/24: thamani ya sasa ya deni la nje kwa Pato la Taifa ni asilimia 20.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 40; thamani ya sasa ya deni la nje kwa mauzo ya nje ni asilimia 114.2 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 180; ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato yatokanayo na mauzo ya nje ni asilimia 11.1 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 15; na ulipaji wa deni la nje kwa kutumia mapato ya ndani ni asilimia 11.6 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 18. Aidha kwa upande wa viashiria vya deni lote (deni la nje na la ndani), thamani ya deni kwa Pato la Taifa ni asilimia 36.4 ikilinganishwa na ukomo wa asilimia 55.

**Kielelezo Na. 1.11: Mwenendo wa Deni la Serikali Machi 2017 - 2024 (Shilingi Bilioni)**

| Viashiria vya Deni la Nje | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2033/34 | Ukomo |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Deni (PV)/pato la taifa | 20.1 | 20.1 | 20.1 | 20.1 | 18.1 | 17.6 | 15.8 | 40 |
| Deni (PV)/uuzaji wa bidhaa nje | 114.2 | 114.2 | 114.2 | 114.2 | 101.4 | 105.1 | 93.8 | 180 |
| Ulipaji wa deni la nje/Uuzaji wa bidhaa nje | 11.1 | 11.1 | 11.1 | 11.1 | 11.3 | 12.2 | 10.0 | 15 |
| Ulipaji wa deni / Mapato ya ndani | 11.6 | 11.6 | 11.6 | 11.6 | 12.0 | 12.2 | 10.0 | 18 |
| Viashiria vya Deni la Nje na Ndani | 2023/24 | 2024/25 | 2025/26 | 2026/27 | 2027/28 | 2028/29 | 2033/34 | Ukomo |
| Deni (PV)/ Pato la Taifa | 36.4 | 36.4 | 36.4 | 36.4 | 36.4 | 33.0 | 30.3 | 55 |
| Deni (PV)/ Mapato ya ndani | 209.2 | 209.2 | 209.2 | 209.2 | 209.2 | 189.6 | 172.8 | - |
| Ulipaji wa deni/ Mapato ya ndani | 44.3 | 44.3 | 44.3 | 44.3 | 44.3 | 30.9 | 25.2 | - |

***Chanzo:*** *Wizara ya Fedha*

Katika kuhakikisha kuwa Deni la Serikali linaendelea kuwa himilivu, Serikali inatekeleza mikakati ifuatayo:

i. Kuandaa Mkakati wa Muda wa Kati wa kuongeza mapato (Medium-Term Revenue Strategy) kupitia Wizara ya Fedha kwa lengo la kuongeza ufanisi wa ukusanyaji wa kodi na mapato mengine yasiyo kodi ili kuhakikisha kuwa sehemu kubwa ya bajeti inagharamiwa kupitia mapato ya ndani;

ii. Kuendelea kudhibiti matumizi yasiyo ya lazima ndani ya Serikali ili kupunguza shinikizo la rasilimali fedha za uendeshaji wa shughuli muhimu za Serikali katika mfuko mkuu;

iii. Kuendelea kukopa zaidi kwenye mikopo yenye masharti nafuu kutoka vyanzo vya nje kwa lengo la kupunguza gharama za ulipaji wa deni la Serikali na kuendelea kutekeleza miradi ya maendeleo.

Aidha, mikopo yenye masharti ya kibiashara itaelekezwa kwa miradi ya miundombinu ambayo yenye uwezo wa kuongeza mapato, inayochochea ukuaji wa haraka wa uchumi na kuongeza mauzo ya bidhaa na huduma nje ya nchi;

iv. Kuendelea kukuza na kuboresha sekta ya fedha nchini ili kuwa mhimili mkubwa wenye uwezo kugharamia miradi mbalimbali ya Serikali kupitia soko la ndani la mikopo na mitaji kwa gharama nafuu zaidi bila kukwamisha sekta binafsi nchini kulifikia soko hilo kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali za kiuchumi. Hatua hii itasaidia kupunguza utegemezi kwenye mikopo inayotoka kwenye vyanzo vya nje na kupunguza vihatarishi katika deni la Serikali vinavyotokana na athari za mabadiliko ya viwango vya ubadilishaji fedha (exchange rate risk); na

v. Kuendelea kutoa miongozo sahihi kwa taasisi za umma zinazochukua mikopo kupiti mizania (balance sheet) yao kwa lengo la kutekeleza miradi ya maendeleo ili kuepuka madeni sanjari (contingent liabilities) yasiyolipika.

Machi 2024, Kampuni ya Moody's Investors Services ilifanya mapitio ya kwanza ya uchumi wa Tanzania ili kubaini uwezo wa nchi kukopesheka. Katika mapitio hayo, Tanzania ilipandishwa hadi daraja la B1 ikiwa ni mtazamo thabiti (STABLE Outlook) kutoka daraja la B2 ikiwa ni mtazamo chanya (POSITIVE Outlook) Machi 2023. Daraja la B1 linaashiria kuendelea kuimarika kwa uchumi wa nchi, hususan katika kipindi cha misukosuko ya kiuchumi iliyotokana na majanga mbalimbali kutoka nje ya nchi katika miaka ya hivi karibuni. Hii inaashiria uwezo wa nchi kuendelea kuhimili misukosuko ya kiuchumi kutoka nje (external shocks). Aidha, mtazamo thabiti (STABLE Outlook) unaashiria uwezekano mdogo wa nchi kubadilishwa daraja katika kipindi cha muda wa kati.

Kupandishwa kwa daraja kulichangiwa na ukuaji wa uchumi kuendelea kuwa imara na wenye uwezo wa kuhimili misukosuko mbalimbali ya kiuchumi ndani na nje ya nchi, maboresho ya sekta ya umma yaliyochangia kuimarika kwa ufanisi katika utendaji kazi pamoja na kuongezeka kwa ukusanyaji wa mapato na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma. Kukamilika kwa mapitio kunaiwezesha nchi kuendelea kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje unaochangia katika kuongeza ajira, fedha za kigeni, teknolojia pamoja na kuwezesha upatikanaji wa fedha kwa gharama nafuu kutoka masoko ya fedha ya kimataifa.

### 1.3.6. Hali ya Umaskini na Maendeleo ya Watu


Hali ya umaskini kwa miaka mingi imekuwa ikitafsiriwa kwa kigezo kimoja cha viwango vya mapato au matumizi. Hata hivyo, hali ya umaskini hupimwa kwa kigezo zaidi ya kimoja ambayo hujumuisha nyanja mbalimbali zikiwemo uchumi, huduma za jamii, nishati na ujenzi wa miundombinu ambayo ndizo viashiria vya msingi katika kupima maendeleo ya watu. Mathalan, lengo la Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025 ni kuiondoa nchi kwenye kundi la nchi masikini na kuingia kwenye kundi la nchi ya kipato cha kati ambapo kipimo chake ni

wastani wa pato kwa mtu (GDP per capita) la kiasi cha dola za Marekani 3,000 ifikapo mwaka 2025. Katika kufikia lengo la Dira ya Taifa 2025, Serikali imeendelea na jitihada mbalimbali za kuboresha pato kwa mtu ambazo zimepelekea wastani wa pato kwa mtu kuongezeka kutoka shilingi 2,844,641 sawa na dola za marekani 1,229.1 mwaka 2022 hadi shilingi 3,055,606 sawa na dola za marekani 1,275.5 mwaka 2023. Ongezeko hii limeifanya Tanzania kuendelea kuwa katika kundi la nchi zenye hadhi ya kipato cha kati cha chini.

Sambamba na hilo, Serikali imeendelea na juhudi mbalimbali za kuboresha maendeleo ya watu ambazo zimechangia kuimarika kwa maisha ya watu kama inavyojidhihirisha katika viashiria vilivyoainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano. Juhudi hizo ni pamoja na: kuendelea kutoa elimu msingi na sekondari bila ada; kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za maji mjini na vijijini; kuendelea kuboresha ushiriki wa sekta binafsi katika utoaji wa huduma za afya hususan maeneo ya vijijini; kuendelea na ujenzi katika wa zahanati, vituo vya afya na hospitali; kuendelea na ujenzi wa barabara za kufungua fursa za kiuchumi maeneo ya mijini na vijijini.


*1.3.6.1 Ongezeko la Idadi ya Watu*

Kwa mujibu wa matokeo ya Sensa ya Watu na Makazi ya Mwaka 2022, idadi ya watu Tanzania imeongezeka na kufikia watu 61,741,120 mwaka 2022 kutoka watu 44,928,923 mwaka 2012 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 3.2. Matokeo hayo yanadhihirisha kuwa ukuaji wa idadi ya watu inaongezeka kwa kiwango cha asilimia 3.2 kila mwaka huku ukuaji wa uchumi ukiendelea kuwa asilimia 5 kila mwaka. Hii inaashiria kuwa ukuaji wa uchumi hauendani na jitihada za kupunguza umaskini hususan katika kuimarisha matumizi ya bidhaa na huduma kwa umma ikiwemo miundombinu na huduma za kijamii. Hivyo, msumuko umewekwa katika kuongeza ukuaji wa uchumi kufikia kiwango cha ukuaji wa asilimia 8 hadi 10 ili kupunguza kiwango cha umaskini. Katika kufikia malengo hayo, Serikali itajielekeza katika kuongeza uwekezaji katika shughuli za uzalishaji, kutoa fursa za wanawake katika kupata elimu ya afya ya uzazi, na kuendelea kuzalisha ajira hususan kwa vijana.



*1.3.6.2 Maendeleo ya Watu*

Kwa mujibu wa Taarifa ya Dunia ya Maendeleo ya Watu ya Mwaka 2023, Tanzania ilishika nafasi ya 167 kati ya nchi 193 katika maendeleo ya watu mwaka 2022 ikilinganishwa na nafasi ya 160 mwaka 2021. Aidha, Fahirisi ya Maendeleo ya Watu - HDI ilifikia 0.532 mwaka 2022 ikilinganishwa na 0.529 mwaka 2021. Fahirisi ya Maendeleo ya Watu - HDI hupima maendeleo ya watu kwa kuzingatia vigezo vya elimu, afya na hali ya Maisha. Kipimo hiki kinatafsiriwa kuwa kadiri tarakimu inavyokaribia moja (1), inaashiria kuimarika kwa maendeleo ya watu. Katika kuhakikisha, Tanzania inapiga hatua katika kushika nafasi bora zaidi kidunia, Kwa upande wa Elimu, Serikali imeendelea na ujenzi wa shule za msingi na sekondari, ukarabati wa vyumba vya madarasa, ujenzi na ukamilishaji wa mabweni. Kwa upande wa elimu ya juu, Serikali imeongeza ujenzi wa vyuo 29 vya ufundi stadi, ukarabati wa vyuo 13 na kazi inaendelea kujenga na kuimarisha miundombinu katika kampasi 14 za vyuo vikuu. Serikali imeongeza fedha za mikopo ya elimu ya juu kutoka shilingi bilioni 654 kwa mwaka 2022/2023 hadi shilingi bilioni 786.7 mwaka 2023/2024.





Katika sekta ya afya, Serikali imeendelea kuimarisha miundombinu ya kutolea huduma za afya; upatikanaji na usambazaji wa chanjo, dawa, vifaa, vifaa tiba na vitendanishi katika ngazi zote. Katika mwaka 2023/2024, Serikali iliendelea kuimarisha huduma za matibabu ya ubingwa na ubingwa bobezi, kuimarisha mfumo wa ugharamiaji wa huduma za afya nchini, kuimarisha utoaji wa mafunzo ya wataalam katika Sekta ya Afya na kuimarisha Mifumo ya TEHAMA. Kuhusu bima ya afya, Serikali imetunga Sheria ya Bima ya Afya kwa Wote ya Mwaka 2023. Lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa huduma bora za afya kwa watanzania wote pindi wanapozihitaji.

Kwa upande wa matumizi ya TEHAMA, hadi kufikia mwezi Februari 2024, jumla ya hospitali za rufaa za mikoa 17 na hospitali nne za kibingwa zimewekewa huduma ya tiba mtandao ambazo ni Iringa, Njombe, Mount Meru (Arusha), Manyara, Singida, Shinyanga, Simiyu, Mwalimu Nyerere Memorial (Musoma), Sekou Toure (Mwanza), Geita, Bukoba (Kagera), Maweni (Kigoma), Kitete (Tabora), Ligula (Mtwara), Sumbawanga, Bombo (Tanga) Bugando, Benjamini Mkapa na Hospitali ya Kanda – Mbeya. Hali ya upatikanaji wa dawa, vifaa tiba na vitendanishi, imefikia asilimia 81 katika ngazi ya vituo vya kutolea huduma za afya ambapo kwa zahanati imefikia asilimia 77, Vituo vya Afya asilimia 71, Hospitali za Halmashauri asilimia 73, Hospitali za Rufaa za Mikoa asilimia 99 na Hospitali za Rufaa za Kanda, Maalumu na Taifa asilimia 86. Aidha Serikali imeendelea kuboresha hali ya maisha hususani kwa upande wa sekta ya maji, ambapo baadhi ya mafanikio

yaliyopatikana ni pamoja na: kuongezeka kwa uwiano wa kaya za vijijini nchini zinazopata maji safi na salama kutoka katika vyanzo vilivyoboreshwa kutoka asilimia 36 mwaka 2019/20 hadi asilimia 56.1 mwaka 2022 sawa asilimia 52 ya kufikia lengo la asilimia 75 ifikapo 2025/26; na kuongezeka kwa asilimia ya watu katika mijini wanaopata maji safi na salama kutoka katika vyanzo vilivyoboreshwa kutoka asilimia 84 mwaka 2019/20 hadi kufikia asilimia 91.5 mwaka 2022 sawa na asilimia ya 68 kufikia lengo la asilimia 95 mwaka 2025/26.

**Kielelezo Na. 1.12: Mwenendo wa Fahirisi ya Maendeleo ya Watu, (1990 – 2022)**





## 1.4. Tathmini ya Muda Mrefu ya Hali ya Uchumi wa Tanzania

Tathmini ya muda mrefu inaonesha mambo makubwa matatu. Mosi, pamoja na changamoto zilizoyumbisha uchumi wa dunia katika vipindi mbalimbali, ikiwemo mabadiliko ya tabia nchi, ugonjwa wa UVIKO – 19, na vita mbalimbali, uchumi wa Tanzania umekuwa stahimilivu na umekuwa ukikua katika hali endelevu. Kwa mfano, katika kipindi cha miongo miwili iliyopita, kati ya mwaka 2000 na mwaka 2020, uchumi wa Tanzania ulikua kwa kiwango cha wastani wa asilimia sita kwa mwaka.

Pili, mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi yamekuwa yakiongezeka mwaka hadi mwaka. Kwa mfano, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi iliongezeka kutoka dola za Marekani bilioni 6.4 mwaka

2020, na yameendelea kuongezeka hadi kufikia dola za Marekani bilioni 8.2 mwaka 2023 (Tazama Kielelezo Na. 1.13). Hali hii ilisababisha kuongezeka kwa uwiano kati ya mauzo ya bidhaa nje ya nchi kutoka asilimia 9.6 mwaka 2000 hadi asilimia 20.9 mwaka 2023.

Tatu,aina ya bidhaa za Tanzania zinazouzwa nje ya nchi zimebadilika katika kipindi cha miongo miwili iliyopita. Kwa mfano, katika miaka ya 2000 asilimia ya 57 ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi ilihusisha mazao ya kilimo katika masoko ya Ulaya, Marekani, na Afrika. Hata hivyo, miaka 20 baadaye, mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi yametawaliwa zaidi na madini na bidhaa nyingi zinauzwa katika masoko ya Asia na nchi za Afrika. Kwa mfano, asilimia 49 ya bidhaa zilizouzwa nje ya nchi mwaka 2023 ilikuwa ni madini, ikifuatiwa na bidhaa za viwandani (17%) na mazao ya kilimo (12%).




Kwa mujibu wa taarifa ya Hali ya Uchumi wa Tanzania ya Benki ya Dunia ya Septemba 2023, uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika na kuhimili vyema athari za UVIKO - 19 na changamoto zingine za dunia zilizojitokeza katika miaka mitatu iliyopita kutokana na sababu kubwa tatu. Mosi, utekelezaji wa mageuzi makubwa yaliyolenga katika kuchochea na kuimarisha ushindani katika uchumi, sambamba na eneo la kwanza la kipaumbele katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26 -"Kuchochea Uchumi Shindani na Shirikishi". Pili, kuendelea kuboresha na kuimarisha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini. Tatu, kuendelea kuaminiwa na taasisi za fedha duniani, pamoja na wadau wetu wa maendeleo. Hii ilithibitishwa pia na taarifa ya tathmini iliyotolewa na Taasisi ya Moody's ya Machi 2024 ambayo ilibadili kipimo (rating) cha Tanzania kutoka imara (stable) kwenda chanya (positive). Katika taarifa yao, taasisi hii walieleza kuwa uchumi wa Tanzania umeendelea kuimarika katikati ya changamoto nyingi za dunia ukionesha ustahimilivu mkubwa. Sababu zilizotolewa na Taasisi ya Moody's ni pamoja na Tanzania kuwa na msingi mzuri wa uchumi mchanganyiko (diversified economy), kuongezeka kwa mauzo ya bidhaa nje ya nchi, ustahimilivu wa deni, sera imara za kifedha, pamoja na kuendelea kuimarika na kuboreka kwa mazingira ya biashara na uwekezaji.

Pamoja na mwelekeo mzuri wa ukuaji wa uchumi wa Tanzania katika kipindi cha miongo mitatu iliyopita mambo manne muhimu yanajitokeza kuhusu uchumi

wa Tanzania. Mosi, ukuaji wa uchumi umekuwa ukihusisha sekta chache na ambazo haziajiri watu wengi kutoka kaya maskini. Sekta zilizoongoza kwa ukuaji kwa mwaka 2023 ni pamoja na Sanaa (17.7%), fedha na bima (12.2%), madini (11.3%) na malazi na chakula (8.3%). Sekta ambazo zilitarajiwa kuajiri watu wengi zilikua kwa kasi ndogo. Sekta hizi ni pamoja na kilimo (4.2%), viwanda (4.3%) na biashara (4.2%). Matokeo ya hali hii ni kwamba ukuaji wa uchumi umekuwa hauendani na kasi ya kupunguza umaskini kwa kiwango cha kuridhisha. Kwa mfano, wakati ambapo kiwango cha umaskini kilishuka kutoka asilimia 27 mwaka 2022 hadi asilimia 26.5 mwaka 2023, kasi ya ongezeko la kipato kwa mwananchi mmoja moja haijawa ya kuridhisha. Hali ya kushuka kwa kasi ya kupunguza umaskini ilichochewa zaidi na mlipuko wa ugonjwa wa UVIKO-19 ulioathiri uzalishaji na hivyo kuwaondoa baadhi ya watu katika shughuli za kiuchumi na ajira.

Pili, ukuaji wa uchumi nchini umekuwa ukitegemea uwekezaji wa umma katika miundombinu na sekta binafsi haijaonekana kuchukua nafasi yake kikamilifu katika kuchochea ukuaji wa uchumi kama ilivyotarajiwa. Uwekezaji kupitia sekta binafsi ndio unaotarajiwa kuchochea ajira na uzalishaji.

Tatu, mauzo ya bidhaa nje ya nchi yameendelea kutegemea bidhaa ambazo hazijaongezwa thamani. Kwa mfano, kama inavyooneshwa katika kielelezo Na. 1.13,wakati uzalishaji viwandani ulitarajiwa kuchangia asilimia 24 ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi ifikapo mwaka 2025 mchango wa sekta kwa wastani wa miaka mitano (2019-2023) ulikuwa asilimia 17.1 pekee (ukilinganisha na asilimia 16.9 mwaka 2019/20). Hii inamaanisha kuwa mauzo haya hayajachangia vya kutosha katika kuzalisha ajira. Nne, nchi yetu bado inanunua zaidi kutoka nje kuliko kiwango tunachouza. Hivyo, bado tuna urari mkubwa katika biashara. Kwa mfano, kama inavyooneshwa katika Jedwali Na 1.5, thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi kwa mwaka 2023 ilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 13.7 ukilinganisha na thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi ya Dola za Kimarekani bilioni 8.2. Wastani wa thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi katika kipindi cha miaka mitano (2019-2023) ilikuwa Dola za Kimarekani bilioni 33.9 ukilinganisha na thamani ya manunuzi ya bidhaa kutoka nje ya nchi ya Dola za Kimarekani bilioni 54.4. Hii ndiyo kusema nchi yetu bado inatumia fedha nyingi za kigeni kuagiza bidhaa ambazo zingeweza kuzalishwa nchini.

**2019 - 2023**


**$13.7 bil.**

*thamani ya mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi*

**$54.4 bil.**

*thamani ya manunuzi ya bidhaa kutoka nje ya nchi*

**Kielelezo Na. 1.13: Kiwango cha mauzo ya bidhaa za Tanzania nje ya nchi kwa sekta.**




**Jedwali 1.5 : Uwiano wa thamani ya mauzo na manunuzi ya bidhaa**

| Na | Mwaka | 2023 | 2019-2023 |
|---|---|---|---|
| 1. | Manunuzi kutoka nje (imports, USD million) | 13,729 | 54,388 |
| 2. | Mauzo nje ya nchi (exports, US$milion) | 8,189 | 33,908 |
| 3. | Urari (balance) | (5,540) | (20,480) |

Hivyo basi, ili kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi unakuwa na athari chanya katika kuinua kiwango cha miasha ya watu na kupunguza umaskini, mipango ya muda mfupi na mrefu ijayo itajikita katika kuhakikisha kuwa ukuaji wa uchumi wetu ***unakuwa jumuishi, unapunguza umaskini, unazalisha ajira nyingi, unaoleta ustawi na unachochea mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi.*** Ili kufikia azma hii, Serikali itachukua hatua zifuatazo:

i. Kuendelea kuwekeza katika kukuza uzalishaji katika sekta ya kilimo kwa kuhamasisha na kuwezesha matumizi ya mbolea bora, kilimo cha umwagiliaji na kilimo biashara;

ii. Kuendelea kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji ili kuchochea ukuaji wa sekta binafsi;

iii. Kuweka na kutekeleza mkakati wa kuchochea uwekezaji katika viwanda vyenye kulenga kuzalisha bidhaa zitakazoifanya nchi ijitosheleze kwa mahitaji ya bidhaa muhimu na kukuza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi;

iv. Kwa kuzingatia nafasi ya madini katika kuendelea kukuza ujazo wa mauzo ya nje, na kwa kuzingatia umuhimu wa madini ya kimkakati (strategic mineral resources-SMR) katika kutimiza azima ya dunia ya kuzalisha nishati safi na salama kwa mazingira, tutaweka mazingira mahususi kwa lengo la kuvutia wawekezaji watakaokuwa tayari kujenga viwanda vya kuongeza thamani ya madini hapa nchini, hususan katika ujenzi wa viwanda vya kuzalisha betri za magari na mitambo;

v. Ili kuchochea ukuaji wa uchumi vijijini, Serikali itaweka mkazo maalum katika kuchochea maendeleo vijijini kwa kuchukua hatua zifuatazo:

a. Kuendelea kuwekeza katika ujenzi wa miundombinu ya barabara na mawasiliano vijijini. Katika kuongeza kasi na kiwango cha wananchi wa vijijini kutumia teknolojia ya habari katika shughuli za kiuchumi, kijamii na elimu, Serikali itaendelea kutekeleza mradi wa mawasiliano vijijini (mobile network rural coverage project) na kuanzisha na kutekeleza mpango maalum wa kuunganisha vijijini kidigitali (rural broadband programme). Aidha, Serikali itaongeza kasi ya kusogeza huduma za maji, afya na umeme vijijini. Katika kukuza stadi za maisha na ujuzi miongoni mwa vijana, Serikali itaweka mazingira na kuwezesha ujenzi wa vyuo vya mafunzo ya amali;

b. Serikali itapitia upya mfumo wa uuzaji wa mazao ya kilimo, mifugo, na misitu kwa lengo la kurahisisha na kuwezesha mazingira ya kufanya biashara vijijini;

c. Kuweka mazingira maalum katika kuvutia ujenzi wa viwanda vidogo vijijini kwa lengo la kufanya ongezeko la awali la thamani (primary processing) katika sekta za kimkakati, zikiwemo kilimo, mifugo, uvuvi, na misitu. Serikali itatumia sera za kifedha na kikodi ili kuvutia wawekezaji katika maeneo ya vijijini ili mazao ya kilimo, mifugo, uvuvi na misitu yatoke vijijini yakiwa yameanza kufanyiwa uchakataji wa awali (semi-processed). Viwanda vya vijijini vitabakisha thamani kubwa kijijini na kutoa nafasi ya ajira kwa vijana na wanawake ambao wengi wao sasa wana elimu ya sekondari. Katika hatua hii, tutahitaji kulipanga upya shirika la viwanda vidogo nchini (SIDO); na

d. Kupitia upya sera za fedha, sheria na kanuni zinazosimamia mikopo kwa lengo la kuzisukuma taasisi za kifedha kuelekeza mikopo katika sekta ya kilimo, ufugaji, uvuvi, na wachimbaji wadogo wa madini.

## 1.5. Mwelekeo wa Hali ya Uchumi wa Taifa kwa Mwaka 2024/25

Kwa kuzingatia mapitio ya hali ya uchumi kama ilivyoanishwa katika sehemu 1.3, lengo kuu la Serikali katika Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2024/25 itakuwa

kuchochea kasi ya ukuaji wa uchumi, kupanua wigo wa ujumuishi katika shughuli za uchumi, kuongeza kasi ya mageuzi ya uchumi na kuondoa umaskini, kutekeleza mikakati ya kuongeza mauzo ya bidhaa zilizoongezwa thamani nje ya nchi ili kuongeza mapato ya fedha za kigeni na kuweka mkazo kwenye shughuli za uchumi zinazozalisha ajira kwa wingi na kuchochea ustawi kwa Watanzania wote.

### 1.5.1. Malengo na Shabaha za Ukuaji wa Uchumi Jumla

Malengo na shabaha za uchumi jumla ni kama ifuatavyo:

i. Kuongeza kasi ya ukuaji wa Pato Halisi la Taifa kufikia asilimia 5.4 mwaka 2024 kutoka ukuaji halisi wa asilimia 5.1 mwaka 2023;
ii. Kuendelea kudhibiti mfumuko wa bei na kuhakikisha kuwa unabaki kwenye wigo wa tarakimu moja ya wastani wa asilimia kati ya 3.0 - 5.0 katika muda wa kati;
iii. Mapato ya ndani kufikia asilimia 15.8 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 ikilinganishwa na matarajio ya asilimia 15.4 mwaka 2023/24;
iv. Mapato ya kodi kufikia asilimia 12.9 ya Pato la Taifa mwaka 2024/25 kutoka matarajio ya asilimia 12.6 mwaka 2023/24;
v. Kuwa na nakisi ya bajeti (ikijumuisha misaada) isiyozidi asilimia 3.0 ya Pato la Taifa; na
vi. Kuwa na akiba ya fedha za kigeni kwa kiwango cha kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa kipindi kisichopungua miezi minne (4).

### 1.5.2. Misingi (Assumptions) ya Mpango kwa Mwaka 2024/25

Mafanikio ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 yamejegwa katika misingi ifuatayo:

i. Kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji na ugharamiaji wa miradi ya maendeleo na shughuli za uwekezaji na biashara;
ii. Kuendelea kuhimili na kudhibiti athari za mabadiliko ya tabia nchi na majanga ya asili na yasiyo ya asili ikiwemo ukame, vita, magonjwa ya mlipuko na mafuriko;
iii. Kuimarika kwa uchumi wa dunia na utulivu wa bei na upatikanaji wa mitaji na mikopo katika masoko ya mitaji na mikopo
iv. Kuendelea kwa upatikanaji na usalama wa chakula nchini;
v. Kuendelea kuwepo wa amani, usalama, umoja na utulivu wa ndani na nchi jirani;
vi. Kuendelea kudumisha utawala bora na utawala wa sheria nchini;
vii. Kuwa na raslimali watu ya kutosha na bora inayokidhi matakwa ya wakati ambayo yanatawaliwa na teknolojia na ubunifu; na
viii. Kuongezaka kwa nidhamu ya kuzingatia na kutekeleza mipango ya kisekta kwa wakati na kama ilivyopitishwa na vyombo mbalimbali vya maamuzi kama Baraza la Mawaziri na Bunge la Jamhuri ya Muungano.

# MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO

02


# 2.1 UTANGULIZI

Mipango ya maendeleo ya Tanzania inaongozwa na Dira ya Taifa ya Maendeleo 2000-2025. Pamoja na hatua zingine, Dira hii inalenga kuona kuwa Tanzania inafuzu kuingia katika kundi la nchi za uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 na kuwa na kiwango cha juu maendeleo ya watu. Katika kufikia Dira hii, Serikali imekuwa ikitekeleza Mipango ya Maendeleo ya Taifa ya Miaka Mitano. Kwa sasa Serikali inatekeleza Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 -2025/26 wenye vipaumbele vitano, ambavyo ni kuchochea uchumi shirikishi na shindani, kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na utoaji huduma, kukuza uwekezaji na biashara, kuchochea maendeleo ya watu na kuendeleza raslimali watu. Nguzo muhimu ya utekelezaji wa Mpango huu ni ukuaji wa uchumi. Taarifa hii inaeleza hatua zilizochukuliwa na mafanikio yaliyopatikana katika ukuaji wa uchumi kwa mwaka 2023.

Sura hii inaeleza utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24 kwa kipindi cha Julai 2023 hadi Aprili 2024 ambao unajumuisha miradi na programu mbalimbali zilizotekelezwa ili kufikia malengo ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano ambao ni mpango wa mwisho katika utekelezaji wa Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Vile vile, inabainisha changamoto zilizojitokeza katika kipindi cha utekelezaji na mikakati ya kukabiliana nazo.

## 2.2. Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo ya Kisekta Mwaka 2023/24

Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24 ulilenga kutekeleza programu na Miradi ya maendeleo kupitia sekta za kiuchumi na kijamii zenye thamani ya shilingi bilioni 15,215.59 sawa na asilimia 34.4 ya bajeti ya Serikali ya shilingi bilioni 44,388.1. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 11,933.51 sawa na asilimia 78.4 ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,282.08 sawa na asilimia 21.6 ni fedha za nje.




Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma zilipanga kutekeleza programu na miradi mbalimbali katika mwaka 2023/24. Utekelezaji ulihusisha miradi mipya na inayoendelea. Taarifa ya utekelezaji hadi kufikia Aprili, 2024 ni kama ifuatavyo:

### 2.2.1. Sekta ya Usafirishaji na Uchukuzi

Sekta ya usafirishaji na uchukuzi imekuwa ni miongoni mwa sekta muhimu zinazochochea ukuaji wa uchumi na nyenzo madhubuti ya maendeleo ya watu. Umuhimu wa sekta hii umejidhihirisha katika uchumi wa dunia ambapo fursa nyingi za kiuchumi zinahusishwa na urahisi wa usafirishaji wa bidhaa na watu kutoka sehemu moja kwenda nyingine. Uhusiano kati ya wingi na ubora wa miundombinu ya usafiri na kiwango cha maendeleo ya kiuchumi ni dhahiri kuwa nchi zenye uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu na mitandao iliyounganishwa vizuri uhusishwa na viwango vya juu vya maendeleo. Kwa kuzingatia umuhimu huo, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali ya miundombinu ya usafirishaji na uchukuzi itakayoleta fursa na manufaa ya kiuchumi na kijamii kama vile kufikiwa kirahisi kwa masoko, ajira na kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta nyingine za uchumi.

Miundombinu ya usafiri na usafirishaji ikijumuisha reli, bandari, barabara na madaraja, na usafiri wa anga ni muhimu katika kuchochea shughuli za kiuchumi. Aidha, eneo la kijiografia linaipa Tanzania fursa ya kipekee katika usafirishaji, biashara na uwekezaji ikilinganishwa na nchi jirani. Kutokana na faida linganifu, Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano umejielekeza katika kuboresha miundombinu ya reli, bandari, barabara na madaraja, na usafiri wa anga.

#### A. Reli

Uendelezaji wa reli za SGR na MGR utasaidia kupunguza muda wa kusafirisha mizigo kutoka Bandari ya Dar es Salaam kuelekea nchi jirani zinazotumia bandari. Na hivyo kuiwezesha nchi kutumia fursa ya kijiografia ili kukuza uchumi. Miradi iliyotekelezwa katika eneo hili ni pamoja na:

i. **Mradi Na. 4281: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR):**

Mradi huu ni mradi wa kielelezo ambao utekelezaji wake ulianza Februari 2017 na unatarajiwa kukamilika Machi 2027. katika kipindi cha utekelezaji mradi unatarajiwa kugharimu dola za Marekani bilioni 7.6.

Shughuli zilizopangwa ni: Kukamilisha ujenzi wa reli ya Standard Gauge kwa

kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) na Morogoro - Makutupora (km 422); kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341); Makutupora – Tabora (km 368); Tabora - Isaka (Km 165); Tabora- Kigoma(506); kuendelea na taratibu za manunuzi ya Mkandarasi na Mshauri Elekezi kwa kipande cha Uvinza- Musongati ( km 156.6); ununuzi wa injini, mabehewa na mitambo kwa ajili ya matengenezo ya njia; kugharamia uendeshaji wa reli ya SGR; kuendelea na ugharamiaji wa mafunzo ya wataalamu wa uendeshaji na usimamizi wa treni ya SGR; kuendelea na taratibu za upatikanaji wa fedha za ujenzi wa reli kwa vipande vya Kaliua – Mpanda - Karema (km 321); Uvinza – Malagarasi (km 156); Isaka - Rusumo – Kigali (km 495) ; Isaka – Rusumo (km 371); na Ulipaji wa fidia kwa wananchi wanaopisha ujenzi wa reli ya SGR.



Hatua zilizofikiwa ni pamoja na: Kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Dar es Salaam – Morogoro (km 300) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 98.93 pamoja na ujenzi wa njia ya kuelekea bandarini yani port link ambao utekelezaji umefikia asilimia 76.12; kipande cha Morogoro – Makutupora (km 422) umefikia asilimia 96.61; kipande cha Mwanza - Isaka (km 341) asilimia 56.21; kipande cha Makutupora - Tabora (km 371) asilimia 14.22; kipande cha Tabora - Isaka (km 165) asilimia 5.38; na kipande cha Tabora – Kigoma (km 506) asilimia 1.81.

Shughuli nyingine zilizotekelezwa ni pamoja na: Ununuzi wa vichwa viwili (2) vya treni na mabehewa 30 kwa ajili ya majaribio na uendeshaji wa awali ambapo mabehewa sita (6) yamewasili; ununuzi wa vichwa vya treni 17 vya umeme ambapo utengenezaji umefikia asilimia 83 na tayari vichwa vya treni vya umeme tisa (9) vimepokelewa na kuanza majaribio na vichwa nane (8) vilivyosalia vinatarajiwa kuwasili mwishoni mwa mwezi Mei, 2024; ununuzi wa seti za treni 10 za kisasa (Electric Multiple Unit - EMU) kwa ajili ya uendeshaji umefikia asilimia 70 ambapo seti ya kwanza imewasili nchini tarehe 26 Machi, 2024; kuwasili kwa mabehewa 65 katika 89 ya abiria yaliyosalia yanatarajiwa kuwasili kuanzia mwezi Juni 2024 na ununuzi wa mabehewa 1,430 ya mizigo.




Kukamilika kwa mradi huu kutaiwezesha Tanzania kuunganisha mtandao wa usafiri na usafirishaji na nchi jirani. Vile vile, itaongeza ufanisi wa usafirishaji wa abiria na mizigo kwa kupunguza muda wa safari na gharama za usafirishaji mizigo; kuiwezesha bandari ya Dar es salaam kuhimili ushindani; na kuchochea uanzishwaji wa viwanda maeneo mengine ya nchi kutokana na kuwepo kwa uhakika wa usafirishaji wa malighafi na bidhaa pamoja na uanzishwaji wa makazi na miji midogo katika maeneo yanayojengwa stesheni. Aidha, kukamilika kwa mradi huu kama ulivyoanishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano utaleta matokeo mahsusi na ya haraka kwenye maeneo ya kiuchumi kama vile kuongeza uzalishaji wa bidhaa, ushindani kikanda na kimataifa, mauzo nje, na ajira, hivyo kutekeleza mojawapo ya malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayoelezea nchi kuwa na uchumi shindani.

ii. **Mradi Na. 4213: Mfuko wa Reli.**

Utekelezaji wa mradi huu utaimarisha usafiri na usafirishaji wa bidhaa na abiria; kupunguza msongamano na uharibifu katika barabara; kuchochea shughuli za kiuchumi katika maeneo yanayounganishwa na reli; kuunganisha viwanda, na masoko pamoja na kuchachua matumizi ya bandari ya Dar es Salaam; uhifadhi wa mazingira kwa kupunguza matumizi ya magari barabarani ambayo ni chanzo cha gesi hatari kwa mazingira; kutoa fursa za ajira wakati wa ujenzi na ukarabati pamoja na kutoa huduma, hivyo kuchangia kuboresha maisha ya watu.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango ni pamoja na: Reli (Nafasi ya nchi kidunia) imekuwa 63 mwaka 2023/24 kutoka nafasi ya 83 mwaka 2019/20 sawa na asilimia 153.8 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa urefu wa reli ya Kisasa (SGR) kutoka km 395.2 mwaka 2019/20 hadi km 795.45 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 48.5 ya lengo la kujenga km 1,219 mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa idadi ya abiria wanaosafiri kwa njia ya reli kutoka 972,000 mwaka 2019/20 hadi 1,816,592 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 71.0 ya lengo ifikapo 2025/26.

### B. Bandari

Bandari ni moja ya kiunganishi muhimu cha usafiri na usafirishaji wa abiria na shehena za mizigo kati ya nchi yetu na mataifa mengine. Uwekezaji katika ukanda wa bahari Kuu, maziwa na bandari kavu utaongeza ajira na mapato ya Serikali na hivyo kuchangia kwenye ukuaji wa uchumi.

Katika kipindi cha utekelezaji wa mpango, Serikali imeendelea kutekeleza Miradi ifuatayo: Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam; Bandari ya Tanga, Bandari ya Mtwara, Bandari ya Bagamoyo, Bandari Kavu katika Eneo la Ruvu pamoja na bandari za maziwa makuu ni Victoria, Nyasa na Tanganyika.

Utekelezaji wa miradi ya uboreshaji wa bandari unachangia ukuaji wa uchumi kwa kuimarisha biashara na kuongeza mapato; kuongeza ufanisi na kupunguza muda wa kupakia na kupakua mizigo; kuchochea maendeleo ya viwanda na biashara ndani ya nchi; kutoa fursa za ajira zitakazoongeza kipato na kuboresha maisha ya wananchi; kuimarisha uhusiano wa kikanda kwa kuwa kitovu cha usafirishaji kwa nchi zisizo na bandari; kuongeza usalama katika usafiri na usafirishaji; na kuimarisha sekta ya utalii.

Mafanikio yaliyofikiwa katika utekelezaji wa miradi hiyo ni pamoja na: Kupungua kwa muda wa makasha kukaa bandarini kutoka siku saba (7) mwaka 2019/20 hadi siku tano (5) mwaka 2023/24 sawa na asilimia 100 ya lengo ifikapo 2025/26 na kuongezeka kwa kiasi cha mizigo iliyohudumiwa kutoka tani milioni 14.56 mwaka 2022/23 hadi kufikia tani 20.72 mwaka 2023/24.

### C. Barabara na Madaraja

Miundombinu ya barabara na madaraja ni muhimu katika kuchochea shughuli za kiuchumi, kuunganisha Tanzania na Nchi jirani, kupunguza msongamano wa magari katika barabara za mijini na kuwezesha usafiri na usafirishaji wa abiria, bidhaa na malighafi kutoka eneo moja hadi lingin. Katika utekelezaji wa Mpango, Serikali imeendelea kutekeleza Miradi ifuatayo:

i. **Mradi Na. 4015: Daraja la Kigongo – Busisi (Mwanza)**:

Mradi huu ni mradi wa kielelezo ambao umeanza kutekelezwa Februari 2020 na unatarajiwa kukamilika Desemba 2024. Utekelezaji wa mradi huu utagharamu kiasi cha shilingi bilioni 699.27. Shughuli zilizopangwa kutekelezwa kwa mwaka 2023/24: Kukamilisha ujenzi wa daraja na barabara unganishi zenye urefu wa km 1.66.

Katika kipindi cha Utekelezaji wa Mpango, hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ujenzi wa daraja pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa km 1.66 ambapo utekelezaji umefikia asilimia 88.

Mradi huu ni miongoni mwa miradi ya ujenzi wa madaraja makubwa na madaraja ya juu ya kimkakati ambao utachochea shughuli za kiuchumi na kurahisisha usafiri na usafirishaji kwenda nchi jirani. Vile vile, kukamilika kwa ujenzi wa Daraja la

Kigongo – Busisi litakuwa kivutio kikubwa cha watalii Nchini. Ujenzi wa daraja hili ni sehemu ya utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano ambao umeweka kipaumbele katika kuwezesha uwepo wa miundombinu imara ikiwemo madaraja na barabara ili kuinua sekta mbalimbali za kimkakati.

**ii. Miradi ya Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi:**

Mradi Na. 4147: Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499), Mradi Na. 4149: Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235), Mradi Na. 4190: Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda (km 211), Mradi Na. 4193: Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro - Singida (km 460), Mradi Na. 4188: Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni - Mkiwa (km 528), Mradi Na. 4112: Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7), Mradi Na. 4041: Barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) na Daraja la Mnywamaji, Mradi Na. 4174: Upanuzi wa Barabara ya Kimara – Kibaha (km 25.7) Ikijumuisha Upanuzi wa Madaraja ya Kibamba, Kiluvya na Mpiji, Mradi Na. 4024: Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145), Mradi Na. 4101: Barabara ya Tanga - Pangani – Makurunge (km 174.5), Mradi Na. 4014: Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu (km 240), Mradi Na. 4022: Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4), Mradi Na. 4123: Barabara ya Dumila – Kilosa (km 141).

Utekelezaji wa miradi hii unatarajiwa kuleta manufaa mbalimbali ikiwemo: kuboresha usafirishaji na kupunguza gharama za usafiri, hivyo kuchochea biashara katika maeneo mbalimbali; kuvutia wawekezaji katika sekta mbalimbali kama kilimo, utalii na viwanda, kwa kuwawezesha kupata masoko na malighafi kwa urahisi zaidi; kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko; kuboresha na kurahisisha upatikanaji wa huduma muhimu kama afya, elimu na maji safi na salama, hasa katika maeneo ya vijijini;  na kupunguza ajali za barabarani na kutoa njia za haraka za kufikisha msaada katika matukio ya dharura.

**iii. Miradi ya Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani:**

Mradi Na. 4124: Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 117), Mradi Na. 4115: Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai – Kamwanga/ Sanya Juu (km 271), Mradi Na. 4154: Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 432.56), Mradi Na. 4164: Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 341.25), Mradi Na. 4128: Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1). Utekelezaji wa miradi hii unatarajiwa kuwa na manufaa mbalimbali ikiwemo: kuimarisha biashara za kikanda kwa kuboresha ufikiaji wa bandari na masoko ya mipakani, kupunguza gharama za usafiri, na kurahisisha usafirishaji wa bidhaa na huduma kwa urahisi na haraka zaidi; kuvutia uwekezaji wa kigeni na kukuza ukuaji wa uchumi kwa kuongeza uzalishaji, kutanua masoko na kutoa fursa za ajira; na kuimarisha ushirikiano na mataifa jirani na kikanda.

iv. **Miradi ya Barabara za Mikoa na Kupunguza Msongamano: Mradi Na. 4145:**

Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68), Mradi Na. 4285 Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Dar es Salaam), Mradi Na. 4146: Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma. Kukamilika kwa miradi hii kunatarajiwa kuwa na manufaa mbalimbali ikiwemo: kuongeza ufanisi katika usafirishaji, kupunguza muda unaopotezwa kwenye foleni na hivyo kuboresha uzalishaji katika uchumi; kuongeza thamani ya ardhi, makazi na mali katika maeneo yaliyoboreshwa, hivyo kuvutia uwekezaji zaidi; kurahisisha ufikiaji wa maeneo mbalimbali ya miji, hivyo kurahisisha maisha ya kila siku ya wananchi; kupunguza msongamano na hatari za ajali, hivyo kuboresha usalama wa watumiaji wa barabara; na athari chanya za kimazingira kufuatia kupungua kwa msongamano kutakapopelekea kupungua kwa matumizi ya mafuta na hivyo kupunguza uchafuzi wa hewa.

v. **Miradi ya Barabara za Vijijini na Mijini: Mradi Na. 4170:**

Matengenezo na Ukarabati wa Barabara; na Mradi Na. 4169: Mradi wa Uboreshaji wa Barabara maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo. Utekelezaji wa miradi hii unatarajiwa kuwa na manufaa mbalimbali ikiwemo: kuongeza urahisi wa kusafirisha bidhaa kutoka katika maeneo ya uzalishaji hususan mazao ya kilimo, mifugo na uvuvi hadi kwenye masoko; kupunguza gharama za usafirishaji; kupunguza upotevu wa mazao unaotokana na mazao kuharibika kutokana na miundombinu hafifu; kuvutia wawekezaji katika sekta za kilimo na viwanda, na hivyo kuchochea maendeleo ya viwanda vinavyotegemea kilimo; kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii kama shule, vituo vya afya, na huduma za maji safi, hivyo kuinua kiwango cha maisha kwa wakazi wa vijijini; na kuimarisha mawasiliano kati ya vijiji na miji.

vi. **Miradi ya Ujenzi wa Nyumba za Serikali na Madaraja: Mradi Na. 4126:**

Ujenzi wa Madaraja Makubwa, Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali, Mradi Na. 6370: Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji Tanzania (Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness-TACTIC), Mradi na. 6507: Uboreshaji wa Bonde la Mto Msimbazi, Mradi Na. 4021: Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (RISE). Utekelezaji wa miradi hii unatarajiwa kuwa na manufaa mbalimbali yakiwa ni pamoja na: Kutoa fursa za ajira kwa wananchi, hususan katika sekta za ujenzi na huduma; kuboresha mazingira ya kibiashara na kukuza uchumi wa maeneo husika; na kuongeza ufanisi na tija katika utendaji na utoaji huduma za Serikali.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango ni pamoja na: Tanzania kufikia nafasi ya 55 ya miundombinu katika mpangilio kati ya nchi 189 Kimataifa, sawa na asilimia 83 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26; Tanzania kuwa nafasi ya 39 ya barabara katika mpangilio wa kimataifa ikilinganishwa na nafasi ya 86 mwaka 2019/20 sawa na asilimia 151 ya lengo ifikapo 2025/26; mtandao wa barabara umefika km 181,655.49 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na kilometa 89,204 mwaka 2019/20 sawa na ongezeko la asilimia la

104; kuongezeka kwa urefu wa mtandao wa barabara za lami kufikia kilometa 12,029 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na kilometa 10,479 mwaka 2019/20, sawa na asilimia 51 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26.



**2023/24**
**km 181,655**
*Mtandao wa barabara umefikia*

## D. Usafiri wa Anga na Viwanja vya Ndege

Usafiri wa Anga na Viwanja vya ndege ni muhimu katika ustawi wa uchumi kwakuwa inawezesha kukuza shughuli za utalii; kutoa ajira mbalimbali; kukuza biashara za ndani na nje ya nchi; kusafirisha abiria na mizigo; na kuongeza pato la taifa. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:


### i. Mradi Na. 4294: Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania:

Mradi wa kuboresha Shirika la Ndege Tanzania ni miongoni mwa miradi ya kielelezo unaotekelezwa katika sekta ya uchukuzi.Mradi huu umeanza kutekelezwa Oktoba 2016 na unatarajiwa kukamilika Oktoba 2034.Gharama za mradi ni kiasi cha shilingi trilioni 7.35.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa: Kufanya malipo kwa ajili ya ununuzi wa ndege tatu (3) moja (1) ya masafa ya kati, moja (1) ya masafa mafupi na moja (1) ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 23; ukarabati na ununuzi wa vifaa vya karakana za matengenezo ya ndege za JNIA na KIA (KIMAFA); kuanza ujenzi wa karakana mpya ya kisasa katika kiwanja cha JNIA; kugharamia mahitaji ya awali ya ndege ndogo moja (1) aina ya Dash 8 Q400; kuendelea na ukarabati wa jengo la ofisi za ATCL Makao Makuu na lililopo Kiwanja cha Ndege cha JNIA Terminal I; kuendelea na ukarabati wa nyumba 38 zilizopo KIA; ujenzi wa eneo la mafunzo ya awali kwa wanaanga; ujenzi na ukarabati wa majengo kwa ajili ya kuhifadhi mizigo katika viwanja vya ndege vya JNIA, KIA na Songwe pamoja na kujenga ofisi za ATCL katika Mji Mkuu Dodoma



**2016-34**
**2** *ununuzi wa ndege za kusafiria*



**2016-34**
**1** *ununuzi wa ndege ya mizigo yenye kubeba tani 23*

Hatua zilizofikiwa ni pamoja na: Kupokelewa kwa ndege 15 hivyo kufanya Shirika kuwa na jumla ya ndege 16. Katika mwaka 2023/24, ndege mbili (2) aina ya Boeing 737-9 Max zimepokelewa. Aidha, Serikali imeendelea na ukarabati wa miundombinu na ununuzi wa vifaa na vipuri kwa ajili ya kuwezesha kufanya matengenezo makubwa na madogo ya ndege aina zote katika karakana za JNIA na KIA.

Uboreshaji wa huduma za Shirika la Ndege nchini unatarajiwa kuchochea uwekezaji katika sekta za utalii na usafirishaji, kufungua biashara za ndani na nje ya nchi na kuongeza fedha za kigeni.

### ii. Miradi ya miundombinu ya Usafiri wa Anga: Mradi Na. 4290:

Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa, Mradi Na. 6377: Kuboresha Miundombinu na

Ununuzi wa Vifaa vya Kufundishia, Mradi Na. 4209: Kiwanja cha Ndege cha Mwanza, Mradi Na. 4206: Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Mradi Na. 4206: Kiwanja cha Ndege cha Songwe, Mradi Na. 4226: Viwanja vya Ndege vya Mikoa, Mradi Na. 4286: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato, Mradi Na. 4221: Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga, Mradi Na. 4222: Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga, Mradi Na. 4156: Kiwanja cha Ndege cha Kigoma, Mradi Na. 4159: na Kiwanja cha Ndege cha Tabora.

Utekelezaji wa miradi hii kunatarajiwa kuwa na athari chanya katika maeneo mbalimbali ya kiuchumi na kijamii ikiwemo: kuongeza kiwango cha usafiri na usafirishaji wa abiria na mizigo; kuongezeka kwa usalama katika usafiri wa anga; kuongeza ufanisi na kupunguza gharama na muda wa usafiri; kuchochea ukuaji wa uchumi kwa kuvutia biashara ya kimataifa, uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje, na kuimarisha biashara za ndani kwa kutoa masoko na fursa za usafirishaji; kuchochea uzalishaji wa ajira; na kuimarisha mawasiliano na ushirikiano wa Kikanda.

Mafaniko yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuimarisha usafiri wa anga na viwanja vya ndege ni kama ifuatavyo: kuongezeka kwa idadi ya ndege zilizonunuliwa kutoka 11 mwaka 2019/20 hadi 16 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 62.5 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya viwanja vya ndege vyenye taa za kuongozea Ndege kutoka viwanja vinne (4) mwaka 2019/20 hadi viwanja 10 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 100 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa Viwanja vya ndege vyenye mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege kufikia sita (6) mwaka 2023/24 ikilinganishwa na kiwanja kimoja (1) mwaka 2019/20 sawa na asilimia 38.5 ya lengo ifikapo 2025/26; kuongezeka kwa mitambo ya ulinzi kwenye viwanja vya ndege kufikia 82 mwaka 2023/24 kutoka mitambo 46 mwaka 2019/20 sawa na asilimia 144 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya rada za hali ya hewa zilizonunuliwa kutoka rada tano (5) mwaka 2019/20 hadi rada nane(8) mwaka 2023/24 sawa na asilimia 150 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26.




**2019/20 - 2023/24**

**10** *kuongezeka kwa idadi ya viwanja vya ndege*



**2019/20 - 2023/24**

**6** *kuongezeka kwa idadi ya viwanja vya ndege vyenye mfumo wa usimamizi*



**2019/20 - 2023/24**

**82** *kuongezeka kwa mitambo ya ulinzi kwenye viwanja vya ndege*

### 2.2.2. Sekta ya Nishati


Sekta ya nishati ni muhimu katika kuchagiza na kuchochea shughuli za biashara na uwekezaji nchini, ikiwemo uzalishaji viwandani. Aidha, sekta hii imegawanyika katika uzalishaji,usafirishaji na usambazaji wa umeme nchini, pamoja na utafutaji na uwekezaji wa mafuta na gesi. Serikali imeendelea kutekeleza mikakati mbalimbali inayochochea upatikanaji wa nishati toshelevu kwa ukuaji wa uchumi kama ilivyoainishwa

katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa (FYDP III) ambao unatekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025. Katika kipindi cha utekelezaji mwaka 2023/24, miradi ifuatayo imeendelea kutekelezwa:

i. **Mradi Na. 3172: Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115**

Mradi huu ni mradi wa kielelezo, ambapo utekelezaji wake ulianza Juni 2018 na unatarajiwa kukamilika Desemba 2024 Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi trilioni 6.5.


Hadi kufikia Aprili 2024, hatua iliyofikiwa ni pamoja na: Kuanza uzalishaji na kuunganishwa kwa mtambo namba tisa (9) wenye uwezo wa kuzalisha MW 235 kwenye Gridi ya Taifa,aidha mtambo namba nane (8) upo katika hatua za mwisho za ukamilishaji na kuendelea na ufungaji wa mitambo saba (7) iliyobaki ambayo ipo katika hatua mbalimbali; na kuendelea na ujenzi wa barabara za kudumu katika eneo la mradi ambapo utekelezaji umefikia asimilia 85.6, daraja la kudumu (asilimia 97.2), nyumba za makazi na ofisi (asilimia 98.5). Kwa ujumla utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 97.43.



**2018 - 2024**

**MW 235**

*kiasi cha umeme kinachozalishwa kupitia mtambo namba 9 kwenye gridi ya taifa.*





**Aprili 2024**

*kwa ujumla utekelezaji wa mradi ulipofikia*

Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza kiwango cha umeme katika gridi ya Taifa. Hivyo, kuchochea shughuli za uwekezaji katika sekta mbalimbali za uzalishaji na uwekezaji katika sekta za kilimo na viwanda. Aidha, upatikanaji wa umeme wa uhakika utaboresha maisha ya watu kutokana na kurahisisha upatikanaji wa huduma za kijamii.

ii. **Mradi Na. 3155: Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquefied Natural Gas - LNG) – Lindi**

Mradi huu ni wa kielelezo ambao upo katika hatua za awali za majadiliano na unatarajiwa kugharimu kiasi cha dola za Marekani bilioni 42. Mradi huu unatarajiwa kuzalisha tani milioni 5 za gesi kwa mwaka na hivyo kuchangia katika ukuaji wa uchumi, fursa za ajira, huduma za ugavi na biashara pamoja na kupunguza matumizi ya kuni na mkaa.



**$42 bilioni**

*mradi huu utazalisha tani milioni 5 za gesi na kuchangia ukuaji wa uchumi*

Shughuli zilizopangwa: Kuanza kazi za awali za maandalizi ya mradi; kuanza tafiti mbalimbali za kitaalamu zikiwemo Usanifu wa Awali wa Kihandisi (Pre-FEED); kuendelea kuwajengea uwezo Wataalamu wa Serikali katika uendeshaji na usimamizi wa Mradi; kuendelea na stadi za kisayansi na stadi za mitambo itakayosimikwa katika eneo la mradi; na kufanya tathmini kuhusu hali za wananchi waliolipwa fidia ili kupisha mradi (post – compensation livelihood study).

Hadi kufikia Aprili 2024, hatua iliyofikiwa ni pamoja na: Serikali kupitia TPDC imeendelea kushirikiana na Kampuni za Shell na Equinor kufanya maandalizi ya kutekeleza miradi ya uboreshaji wa hali ya maisha kwa wananchi waliopisha eneo la mradi (post compensation livelihood restoration program), ikiwemo kusaini Mkataba wa Makubaliano ya ujenzi wa shule ya msingi ya Likong'o iliyopo Manispaa ya Lindi. Aidha, kukamilika kwa mradi huu kutafanya nchi kupata mapinduzi makubwa ya kiuchumi na kuifanya Tanzania kuwa moja ya nchi zinazochangia katika usalama wa nishati duniani. Hii itawezesha nchi kufikia malengo ya Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 ya kuwa na maisha bora kwa kila watanzania.

**iii. Mradi Na. 3176: Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) lenye urefu wa km 1,443**

Mradi huu unalenga kusafirisha mafuta ghafi kutoka Hoima hadi Tanga ambapo utekelezaji wake ulianza Februari 2022 na unatarajiwa kukamilika Desemba 2025. Mradi huu ni miongoni mwa miradi ya kielelezo ambao unatarajiwa kugharimu kiasi cha dola za Marekani bilioni 5.088.

Shughuli zilizopangwa ni: Kukamilisha ulipaji wa fidia kwa wananchi ikiwemo kuhamisha makaburi zaidi ya 400; kukamilisha ujenzi wa nyumba za fidia kwa wananchi; kuanza ujenzi wa bomba; kuendelea na ujenzi wa kambi za wafanyakazi; kuendelea na ujenzi wa kiwanda cha kuunganisha mabomba; kuanza ujenzi wa bandari na matenki ya kupokea mafuta; kuanza ujenzi wa gati; na kuendelea kuchangia hisa za kampuni.

Hadi kufikia Aprili 2024, hatua iliyofikiwa ni pamoja na: kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi ya Shilingi bilioni 34.93 kwa wananchi 9,823 kati ya 9,904 waliopisha utekelezaji wa mradi, sawa na asilimia 99.2; kukamilika kwa ujenzi wa nyumba 340 sawa na asilimia 100 ya makazi mbadala kwa wananchi 294 waliopoteza makazi na kupisha mkuza; kukamilika kwa ujenzi wa karakana ya kuweka mfumo wa upashaji joto kwenye mabomba; na kuendelea na ujenzi wa maeneo 14 ya makambi. Aidha, mabomba yenye urefu wa kilomita 400 yameshawasili nchini na zoezi la kuwekewa mfumo wa kupasha joto, usalama na mawasiliano wa bomba (thermal insulation and fiber optic cables) linaendelea.

Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza ajira na mapato ya Serikali kupitia tozo na ada mbalimbali. Aidha, ujenzi wa

**400**

*makaburi yaliyohamishwa kukamilisha ujenzi wa nyumba za fidia kwa wanachi*

**Aprili 2024**

**34.93 bil.**

*malipo ya fidia kwa wananchi waliopisha utekelezaji wa mradi*

**Aprili 2024**

**340**

*ujenzi wa nyumba kwa wanachi waliopoteza makazi na kupisha mradi*

**Aprili 2024**

**km 400**

*mabomba ya kuwekewa mfumo wa kupasha joto, usalama na mawasiliano*

bomba utahamasisha shughuli za utafiti na uchimbaji wa mafuta kwenye maeneo yenye viashiria vya upatikanaji wa mafuta. Hivyo, Tanzania kunufaika kupitia miundombinu ya usafirishaji mafuta pindi uwepo wa mafuta katika maeneo hayo utakapobainika. Vile vile, mradi huu utawezesha kuongeza mapato ya bandari ya Tanga pamoja na kukuza shughuli za kiuchumi katika eneo la Chongoleani. Kwa msingi huo, utekelezaji wa mradi huu utawezesha nchi kuwa na uchumi shindani na wenye ukuaji endelevu kama ilivyoanishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 kupitia utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano.

**iv. Miradi ya kufua umeme:**

Miradi ya kuzalisha umeme kwa kutumia gesi asilia Kinyerezi I – Extension MW 185; Kufua Umeme wa Maji Rusumo (MW 80); Kufua Umeme wa Maji wa Malagarasi (MW 49.5); Kufua Umeme wa Maji wa Kakono (MW 87.8); na Kuzalisha Umeme Jua Shinyanga (Kishapu Solar – MW 150). Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza jumla ya MW 552.3 katika Gridi ya Taifa na hivyo kuchagiza shughuli za biashara na uwekezaji.

**v. Miradi ya Usafirishaji umeme: Mradi Na. 3111:**

Mradi wa uimarishaji wa Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization); Mradi Na. 3175: Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Singida – Arusha – Namanga, Mradi Na. 3179: Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Rufiji – Chalinze – Dodoma na Chalinze - Kinyerezi , Chalinze – Kinyerezi kV400, Kinyerezi – Somanga kV 400, Mradi Na. 3166: Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 – North West Grid Extension (Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi), Mradi Na. 3181: Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 Benaco – Kyaka. Kuongezeka kwa urefu wa njia za kusafirishia umeme, kufika katika maeneo ambayo hayakuwa na Gridi ya Taifa na kupunguza upotevu wa umeme kutokana na kuimarishwa kwa njia za kusafirisha umeme. Mtandao wa usafirishaji wa umeme uliosambaa utarahisisha shughuli za uunganishaji wa umeme kwa watumiaji mbalimbali, hivyo kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii.

Aidha, Serikali imeendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini, pamoja na mradi wa kusambaza Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Pwani na Lindi, na kuendeleza miradi ya nishati jadidifu (jotoardhi, upepo na umeme-jua). Kuongezeka kwa upatikanaji wa nishati maeneo ya vijijini kutachochea maendeleo na shughuli za uzalishaji na hivyo kupunguza uharibifu wa mazingira unaotokana na shughuli za kibinadamu.

Mafaniko yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha sekta ya nishati ni kama ifuatavyo: Kuongezeka kwa uwezo wa kuzalisha umeme kutoka MW 1,602.3 mwaka 2019/20 hadi MW 2,138 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 16.2 ya lengo la MW 4,915; kuongezeka kwa urefu wa gridi ya taifa kutoka Km 5,896.3 mwaka 2019/20 hadi Km 7,745.4 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 53.5 ya lengo la Km 9,351. Aidha, Vijiji 11,837 vimeunganishwa na umeme kupitia mradi wa turnkey wa REA III sawa na asilimia 96.37 ya lengo la vijiji 12,318 katika mikoa 26.

Katika kipindi cha utekelezaji wa Mpango, Serikali imeendelea kuhakikisha kwamba umeme wa uhakika umeleta utulivu katika sekta za uzalishaji hususan viwanda vya saruji, nguo na marumaru na hivyo kuvutia shughuli za biashara, uwekezaji na ajira. Jitihada zote hizi zitaiwezesha nchi kufikia uchumi wa kati kukiwa na nishati ya uhakika ifikapo mwaka 2025

### 2.2.3. Sekta ya Habari, Teknolojia ya Habari na Mawasiliano

Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA) ni nyenzo muhimu katika kuongeza ufanisi wa sekta za uzalishaji, huduma na utawala. Uimarishaji wa sekta hii uwezesha kurahisisha na kupunguza gharama za uendeshaji na ufanyaji biashara na utoaji wa huduma za kijamii. Serikali kwa kushirikiana na sekta binafsi imeendelea na utekelezaji wa mikakati mbalimbali inayolenga kuongeza upatikanaji wa huduma za TEHAMA nchini.

Katika utekelezaji wa Mpango, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali kama ifuatavyo:

i. **Miradi ya Miundombinu ya Mawasiliano: Mradi Na. 4283:**

Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa, Mradi Na. 4234: Mfumo wa Anwani za Makazi na Mradi Na. 4280: Tanzania ya Kidijitali. Utekelezaji wa miradi hii utawawezesha kuboresha utoaji wa huduma bora na zenye gharama nafuu za mawasiliano nchini na kurahisisha shughuli za biashara na uwekezaji.

ii. **Miradi ya Uhabarishaji na Ubunifu: Mradi Na. 4279:**

Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji, Mradi Na. 6567: Habari kwa Umma, Mradi Na. 4292: Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA (ICT Park), Mradi Na. 6505: Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji, Mradi Na. 4937: Ujenzi wa Kiwanda cha Kupiga Chapa (Government Press Development Programme), na Mradi Na. 6226: Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA. Utekelezaji wa miradi hii utawezesha kufikisha habari na matangazo kwa wananchi walio wengi kupitia maudhui yaliyotengenezwa kitaalamu. Hivyo, kujenga rasilimali watu inayopenda kujifunza na yenye uelewa na masuala mbalimbali yanayoendelea kitaifa na kimataifa.

Mafaniko yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha matumizi ya TEHAMA ni kama ifuatavyo: Kuongezeka kwa watumiaji wa mtandao wa internet kutoka asilimia 43 mwaka 2019/20 hadi asilimia 58.1 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 40.8 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya watu waliofikiwa na masafa ya mawasiliano kutoka asilimia 45 mwaka 2019/20 hadi asilimia 86 (3G) na 79 (4G) mwaka 2023/24 na kuongezeka kwa maeneo yaliyofikiwa na masafa ya mawasiliano kufikia asilimia 70 (3G) na 63 (4G) mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 80 ifikapo mwaka 2025/26 kuongezeka kwa taasisi za Serikali zilizoungwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano kutoka asilimia 20 mwaka 2019 hadi asilimia 50 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 60 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya watu wanaomiliki simu za mkononi kutoka watu milioni 25.1 mwaka 2019/20 hadi watu milioni 37 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la watu milioni 28.6 ifikapo 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya Kaya zinazotumia mfumo wa anwani za makazi na misimbo ya posta

kutoka kaya 450,980 mwaka 2019/20 hadi kaya 11,126,234 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na kaya 1,975,000 ifikapo 2025/26; kuongezeka kwa Taasisi za Umma zinazotumia mfumo anwani na misimbo ya posta kutoka 48,516 mwaka 2019/20 hadi 99,545 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 105 ya lengo; na kuongezeka kwa idadi ya watu wanaopata mtandao wa simu za mkononi kutoka asilimia 94 mwaka 2019/20 hadi asilimia 98 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 133 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26. Aidha, Serikali itaendeleza matumizi ya TEHAMA kwenye uzalishaji wa bidhaa na utoaji wa huduma kwa ujumla ili kuhudumia wateja wa hapa nchini pamoja na kutumia fursa za uwepo wa Soko hususan nchi jirani na kwenye Ukanda wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) pamoja na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Bara la Afrika (SADC).

2019/20 **43%** kutoka → 2023/24 **58.1%** kufikia

*kuongezeka kwa watumiaji wa mtandao wa internet nchini.*

2023/24 **86%** 3G ..... **79%** 4G

*kuongezeka kwa watu waliofikiwa na mawasiliano.*

2023/24 **37 mil.** wamiliki simu

*kuongezeka kwa idadi ya watu wanaomiliki simu za mkononi*

2019 **20%** kutoka → 2023/24 **50%** kufikia

*kuongezeka kwa taasisi za Serikali zilizoungwa na mkongo wa taifa wa mawasiliano.*

2023/24 **99,545** idadi ya kaya

*kuongezeka kwa taasisi za umma zinazotumia mfumo anwani na misimbo ya posta.*

2023/24 **11.1 mil.** idadi ya kaya

*kuongezeka kwa kaya zinazotumia mfumo wa anwani*

### 2.2.4. Sekta ya Uzalishaji Viwandani

Sekta ya viwanda imeendelea kuwa mhimili na kiungo muhimu katika ukuaji wa uchumi, kupitia uongezaji wa thamani katika uzalishaji wa bidhaa mbalimbali. Aidha, sekta binafsi imekuwa na mchango mkubwa katika uendelezaji wa sekta hii, ambayo imechangia katika upatikanaji wa ajira na fedha za kigeni kupitia mauzo nje. Uwekezaji katika sekta ya viwanda umejikita katika Maeneo Maalum ya Uwekezaji (EPZ na SEZ) na maeneo binafsi. Serikali imeendelea kuimarisha sekta hii kwa kuboresha mazingira ya uwekezaji kwa sekta binafsi na kuimarisha taasisi zinazochochea maendeleo ya viwanda ili ziweze zalisha teknolojia bora kwa matumizi ya viwanda. Katika kipindi cha utekelezaji mwaka 2023/24, miradi ifuatayo imeendelea kutekelezwa:

i. **Kanda Maalumu za Kiuchumi: Mradi Na. 4920: Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo**

Mradi huu wa kielelezo umejikita katika uwekezaji wa bandari ya Bagamoyo na uendelezaji wa maeneo maalumu ya uzalishaji bidhaa mbalimbali. Utekelezaji wa mradi huu unalenga kukuza uwekezaji kutoka nje ili kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni, uhamisho wa teknolojia, kuimarisha urari wa biashara, kuongeza ajira na mapato ya ndani.

Shughuli zilizopangwa: Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya barabara yenye urefu wa kilomita tatu (3) kwa kiwango cha lami katika eneo la mradi wa Bagamoyo SEZ; ukarabati wa miundombinu ya ndani katika eneo la uwekezaji la Benjamin William Mkapa SEZ; na urasimishaji wa makazi 107 yasiyopangwa ya Mlingotini, Zinga na Kiromo kwa kuyapanga ili kuweka miundombinu ya msingi na huduma za jamii.

Hadi kufikia Aprili 2024, hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uhuishaji wa upembuzi yakinifu na Mpango Kabambe wa mradi; kuendelea na ujenzi wa barabara yenye urefu wa kilomita tatu (3) ambapo utekelezaji umefikia asilimia 69; na ukarabati wa ukuta na mifereji ya maji ya mvua (drainage) katika eneo la Benjamin William Mkapa - SEZ ambapo utekelezaji umefikia asilimia 30.

Serikali itaendelea kuimarisha miundombinu katika kanda maalumu za uchumi na maeneo maalumu ya uwekezaji ili kujenga uchumi shindani kama ilivyoanishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano unaosisitiza ustawi wa viwanda kwa maendeleo ya uchumi na watu kwa lengo la kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025 inayolenga kuifanya Tanzania kuwa nchi yenye uchumi shindani na maendeleo endelevu.

i. **Mradi Na. 1122: Magadi Soda Engaruka**

Mradi huu ni wa kielelezo ambao ni muhimu kwa ustawi wa viwanda nchini vinavyotumia malighafi ya magadi soda. Utekelezaji wa mradi huu utaokoa kiasi cha fedha cha zaidi ya shilingi bilioni 30 kwa mwaka kinachotumika kuagiza Magadi soda kutoka nje ya nchi kwa ajili ya matumizi ya malighafi viwandani.

Shughuli zilizopangwa ni: Kulipa fidia wananchi wanaopisha mradi (PAP); kuendelea na hatua za kutafuta mwekezaji wa mradi; kufanya uhakiki wa taarifa zilipo katika tafiti zilizofanyika (Brine Resource appraisal and Techno-economic study review); na kulipa leseni za uchimbaji.

Hadi kufikia Aprili 2024, hatua iliyofikiwa ni: Kukamilika kwa uhakiki wa uthamini wa ulipaji fidia kwa wananchi watakaopisha mradi; kukamilika kwa zoezi la ugawaji wa maeneo katika maeneo matatu (3) ya mradi kwa ajili ya uwekezaji ambapo maeneo mawili (2) yanatarajiwa kutangazwa; kulipia leseni ya uchimbaji pamoja na kuanza maandalizi ya ujenzi wa miundombinu ya msingi. Utekelezaji wa mradi huu utawezesha ukuaji wa viwanda vinavyotumia magadi soda kama malighafi ya uzalishaji ikiwemo viwanda vya madawa, makaratasi na uchenjuaji wa madini, utaongeza fedha za kigeni kutokana na uuzaji wa bidhaa zitakazozalishwa na kuongeza fursa za ajira.

### ii. Mradi Na. 3171: Makaa ya Mawe Mchuchuma na Mradi Na. 3161: Chuma Liganga

Miradi hii ni miongoni mwa miradi ya kielelezo ambapo utekelezaji wake unatarajia kuzalisha tani milioni tatu (3) za makaa ya mawe kwa mwaka, chuma (tani milioni 2.9) kwa mwaka, Vanadium na Titanium pamoja na tani milioni 1.0 za chuma cha pua kwa mwaka Uwekezaji katika miradi hii unatarajiwa kutoka kwa Sekta Binafsi.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa katika miradi hii pacha ni pamoja na: Kulipia leseni za uchimbaji nje ya leseni za Kampuni ya ubia; kutafuta mwekezaji mpya, kufanya majadiliano na kuingia mkataba wa ubia; kufanya ukarabati wa ofisi Ludewa; na ununuzi wa gari ya mradi.

Hadi kufikia Aprili 2024, hatua iliyofikiwa ni: Kuendelea na ulipaji wa fidia kwa wananchi katika vitongoji vya Mnyusi, Ilongi, Myoruwa na Luhaha ambapo utekelezaji wake umefikia asilimia 97.99; kulipia leseni za uchimbaji nje ya leseni za Kampuni ya ubia; kufanyika kwa vikao viwili (2) vya majadiliano na mwekezaji; na kukamilisha taratibu za manunuzi ya gari la mradi.

Miradi hii pacha inatarajiwa kuchangia katika agenda ya mageuzi ya viwanda hususan katika maeneo ya saruji, chuma cha pua na mbolea. Vile vile, kuimarisha urari wa biashara na malipo kutokana na kupungua kwa kiasi cha fedha kinachotumika kuagiza chuma nje ya nchi, pamoja na kuongeza fursa za ajira na uwekezaji.

### iii. Miradi ya Uimarishaji wa Taasisi Wezeshi za Sekta ya Viwanda: Mradi Na. 6260: Kuwezesha Taasisi

Utekelezaji wa mradi huu umewezesha kuimarika kwa kiwanda cha mashine na vipuri KMTC ambacho kimeanza uzalishaji wa vipuri na mitambo baada ya kufungwa kwa mtambo wa kuyeyushia chuma. Aidha, mradi huu umewezesha kuanza kwa maaandalizi ya miradi ya Makaa ya Mawe ya Katewaka na Maganga Matitu Sponge Iron, ambayo itazalisha makaa ya amwe na chuma, ili kupunguza uagizaji wa chuma kutoka nje. Kutekelezwa kwa mradi huu kutachochea maendeleo ya viwanda na uwekezaji nchini, hivyo kupelekea kukua kwa mchango wa sekta ya viwanda na uzalishaji katika pato la taifa, matumizi bora na yenye tija ya rasilimali chuma na makaa ya mawe, pamoja na shughuli za biashara na ajira.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya uzalishaji wa bidhaa ni pamoja na: Kuongezeka kwa

mchango wa sekta ya uzalishaji bidhaa viwandani katika teknolojia ya chini kutoka asilimia 35 mwaka 2019/20 hadi asilimia 40 mwaka 2023/24, sawa na asilimia 71.4 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka mchango uwa sekta ya uzalishaji viwandani katika mapato ya mauzo nje kutoka asilimia 17.1 mwaka 2019/20 hadi asilimia 19.6 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 131.6 ya lengo ifikapo mwaka 2025/26.

### 2.2.5. Sekta ya Kilimo

Sekta ya Kilimo imeendelea kuwa uti wa mgongo wa maendeleo ya kiuchumi na kijamii nchini. Sekta hii imekuwa ikichangia katika kutoa malighafi kwa viwanda na masoko kwa bidhaa zilizochakatwa, kuongeza ajira, kuimarisha usalama wa chakula na lishe na kuongeza mauzo ya mazao nje ya nchi. Aidha, Serikali imeendelea kuleta mabadiliko katika sekta ya kilimo kwa kuongeza uzalishaji, biashara na kipato cha mkulima wa hali ya chini ili kuboresha hali ya maisha, usalama wa chakula na lishe na mchango katika Pato la Taifa.

Miradi ya kuimarisha shughuli za kilimo cha mazao: miradi hii inajumuisha miradi inayolenga kuimarisha upatikanaji wa pembejeo, huduma za ugani, tafiti na masoko ambapo katika kipindi cha mwaka 2023/24 miradi ifuatayo imetekelezwa: Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II; Mradi 4408: Programu ya Mifumo Himilivu ya Chakula (TFSRP); Mradi 4430: Programu ya kuwezesha upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo; Mradi Na. 4499: Kudhibiti Sumukuvu; na Mradi Na. 4427: Kuendeleza Kilimo na Uvuvi – AFDP.

Kukamilika kwa miradi hii kutaongeza thamani ya mazao na shughuli za uzalishaji kupitia kuimarishwa kwa miundombinu ya utafiti na kufanya tafiti zitakazozingatia ugunduzi wa aina bora za mbegu na mbinu bora za kilimo; kuongeza uzalishaji, upatikanaji na usambazaji wa pembejeo kwa wakulima nchini kupitia mpango wa ruzuku (mbegu,mbolea, viuatilifu) na zana za kilimo; kupungua kwa utegemezi wa kilimo cha mvua kwa wakulima na kuwawezesha kulima mwaka mzima kutokana na kuimairishwa kwa kilimo cha umwagiliaji; kuwawezesha wakulima kuwa taarifa za msingi kuhusu huduma za masoko na huduma nyingine za msaada muhimu kwa maendeleo ya kilimo kupitia kuimarika kwa huduma za ugani na mafunzo; kuimairika kwa hali ya usalama wa chakula na lishe kutokana na kuboreshwa kwa miundombinu ya uhifadhi wa mazao; na kuongezeka kwa idadi ya vijana waliojiajiri kwenye sekta ya kilimo kutokana na kuanzishwa kwa kilimo cha mashamba makubwa (block farming).

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi ya sekta ya kilimo ni pamoja na: Kuongezeka kwa utoshelevu wa chakula kutoka asilimia 118 mwaka 2019/20 hadi asilimia 124 mwaka 2023/24 sawa asilimia 50 ya lengo la asilimia 130 kwa mwaka 2025; kuongezeka kwa hekta za umwagiliaji kutoka hekta 694,715 mwaka 2019/20 hadi kufikia hekta 727,280.6 mwaka 2023/24 ikiwa matarajio ni kufikia lengo la hekta 1,200,000 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa upatikanaji wa Mbegu bora za mazao na kufikia tani 68,473.67 mwaka 2023/24 ikiwa matarajio ni kufikia ni lengo la tani 140,000 kwa mwaka 2025/26. Mafanikio mengine ni kuongezeka kwa asilimia ya ardhi ya kilimo inayotumia zana za kisasa (mechanization services) katika mnyororo

wa thamani kutoka asilimia 47 mwaka 2019/20 na kufikia asilimia 52 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 17.9 ya lengo la asilimia 75 ifikapo 2025/26, na kuongezeka kwa idadi ya mashamba makubwa (Block Farms) kutoka hekta 110 mwaka 2019/20 hadi hekta 138 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 31 ya lengo ifikapo 2025/26.

### 2.2.6. Sekta ya Mifugo

Sekta ndogo ya mifugo imeendelea kuwa sekta muhimu katika kuchangia ukuaji wa uchumi na uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya sekta za viwanda. Sekta hii kwa mwaka 2023 ilichangia asilimia 6.2 katika pato la taifa na kuongeza fedha za kigeni kutokana na mauzo ya nyama na ngozi nje ya nchi.

Miradi ya uendelezaji wa sekta ndogo ya mifugo; Katika kipindi cha mwaka 2023/24, Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II- mifugo) ambao unajumuisha uimarishaji wa afya ya mifugo;upatikanaji wa mbegu bora za mifugo, upatikanaji wa malisho, vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo; huduma za ugani; utafiti na mafunzo ya Taaluma za mifugo;uongezaji thamani na biashara ya mifugo na mazao yake; uendelezaji wa Vituo Atamizi vya uwekezaji vya vijana; na uimarishaji wa Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO).

Katika kipindi cha mwaka 2023/24, utekelezaji wa shughuli hizo umechangia katika: Ongezeko la idadi ya mifugo, uzalishaji wa maziwa, mayai na nyama. Aidha, kuongezeka kwa kiwango cha uzalishaji wa mazao ya mifugo kumechochea ukuaji wa biashara ndani na nje ya nchi, hivyo kupelekea kuongezeka kwa mapato.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi ya sekta ndogo ya mifugo ni pamoja na: kupungua kwa kiwango cha vifo vya mifugo kutoka asilimia 27 mwaka 2019/20 hadi asilimia 12 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 100 ya lengo la asilimia 12 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa uzalishaji wa nyama kutoka tani 702,000 mwaka 2019/20 hadi tani 803,264 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 40.5 ya lengo la tani 951,700 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa uzalishaji maziwa kutoka lita bilioni 3.01 mwaka 2019/20 hadi lita bilioni 3.97 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 69 ya lengo la lita bilioni 4.3 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa uchakataji wa nyama kutoka tani 286 mwaka 2019/20 hadi tani 300 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 6.54 ya lengo la tani 500 mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa Mauzo Nje ya Nyama kutoka tani 692.46 mwaka 2019/20 hadi tani 13,745.38 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 2.15 ya lengo la tani 7,200 mwaka 2025/26.

### 2.2.7. Sekta Ndogo ya Uvuvi

Sekta Ndogo ya Uvuvi ni miongoni mwa sekta muhimu za kiuchumi inayochangia katika uzalishaji wa malighafi kwa ajili ya sekta ya viwanda na chakula. Katika mwaka 2023 sekta ndogo ya uvuvi ilichangia asilimia 1.7 katika pato la taifa na kuongeza fedha za kigeni kutokana na mauzo ya samaki nje ya nchi pamoja na kutoa ajira, kuimarisha upatikanaji wa lishe bora.

i. **Mradi Na: 4702 Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Kilwa Masoko – Lindi.**

Mradi huu ni mradi wa kielelezo ambao utekelezaji wake ulianza mwezi Juni 2022 na unatarajiwa kukamilika Februari 2025.

Utekelezaji wa mradi huu unatarajiwa kugharimu kiasi cha shilingi bilioni 280.6.

Shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni: Kuendelea na ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko - Lindi; na ununuzi wa meli tatu (3) za uvuvi wa Bahari Kuu.

Hadi kufikia Aprili, 2024, utekelezaji wa mradi umefikia asilimia 53. Kukamilika kwa mradi huu kutaongeza upatikanaji wa samaki kwa ajili ya matumizi ya nyumbani na viwandani. Hivyo kuimarisha upatikanaji wa lishe bora kwa jamii, na kuongeza mauzo nje kutokana na uvuvi utakaofanyika katika bahari Kuu.

ii. **Miradi ya kuendeleza sekta ndogo ya uvuvi: Mradi Na. 4427:**

Kuendeleza Kilimo na Uvuvi – AFDP; Mradi Na. 4703: Ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO); Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II-uvuvi); na Programu 4429: Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi. Utekelezaji wa miradi hii utawezesha kuimarisha mchango wa sekta ndogo ya uvuvi katika Pato la Taifa, kuimarisha lishe za wananchi katika maeneo ambapo miradi inatekelezwa, kuimarisha ajira, kupunguza uharibifu wa mazingira na kukuza biashara na masoko hususan katika maeneo ya utekelezaji wa miradi.

Mafaniko yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa ajili ya kuimarisha sekta ya uvuvi ni kama ifuatavyo: Kuongezeka kwa uzalishaji wa samaki kutoka tani 497,567.28 mwaka 2019/20 hadi tani 513,218.90 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 18 ya lengo la tani 600,000 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya viwanda vya kusindika samaki kutoka viwanda 12 mwaka 2019/20 hadi viwanda 17 sawa na asilimia 100 ya lengo la mwaka 2025/26; kuongezeka kwa uzalishaji wa chakula cha samaki kutoka tani 464 mwaka 2019/20 hadi tani 3,309.9 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 139 hivyo kuvuka lengo la tani 2,500 mwaka 2025/26.

### 2.2.8. Sekta ya Madini

Sekta ya Madini ni sekta inayofungamanishwa na Sekta nyingine za kiuchumi kama vile viwanda na kilimo ili kuzalisha bidhaa mbalimbali zinazotumia malighafi mfano mbolea, betri za magari, simu, kompyuta na bidhaa nyingine. Ufanisi katika sekta hii umeiwezesha Tanzania kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja kutoka nje (FDI). Miongoni mwa madini na vito vya thamani vinavyovutia uwekezaji ni pamoja na: dhahabu; almasi; tanzanite; rubi; na nikeli. Katika mwaka 2023/24 miradi iliyotekelezwa ni pamoja na;

i. **Miradi ya kuendeleza rasilimali za madini: Mradi Na. 1119:**

Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini. Utekelezaji wa mradi huu utawezesha upatikanaji wa taarifa mbalimbali za jiosayansi kupitia tafiti zinazohusu uwepo wa madini nchini. Vile vile, mradi huu umewezesha udhibiti wa vitendo vya utoroshaji wa madini kwenda nje ya nchi na kukomesha biashara haramu ya madini, kuongeza mchango wa sekta ya madini katika Pato la Taifa na maeneo yanayozunguka migodi, pamoja na fedha za kigeni.

ii. **Miradi ya Mafunzo na utafiti za sekta ya madini: Mradi Na. 1120:**

Kituo cha Jemolojia Tanzania. Utekelezaji wa mradi huu utawezesha kuongezeka

kwa wataalamu kutoka kwenye fani za teknolojia ya madini ya vito na usonara ambao watachangia katika kuongeza thamani ya madini yanayozalishwa nchini.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo ni pamoja na: kiwango cha wastani wa ukuaji wa sekta ya madini kuongezeka kutoka asilimia 6.9 mwaka 2019/20 na kufikia hadi 11.3 mwaka 2023 ikiwa ni zaidi ya lengo la asilimia 7.7 ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa mchango katika Pato la Taifa kutoka asilimia 5.6 mwaka 2019/20 hadi kufikia asilimia 9.0 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la kufikia asilimia 10 kwa mwaka 2025/26; kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutoka dola za Marekani milioni 2,977 mwaka 2019/20 hadi dola za Marekani milioni 3,551.4 mwaka 2023 ikiwa lengo la kufikia dola za Marekani 5,505 mwaka 2025/26; kupungua kwa mauzo ghafi nje kutoka asilimia 15 mwaka 2019/20 hadi asilimia 9 mwaka 2023/2024 ikilinganishwa na lengo la asilimia tano (5) ifikapo mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa mchango katika mapato ya fedha za kigeni kutoka asilimia 50.3 mwaka 2019/20 hadi asilimia 56.2 mwaka 2023 ikiwa ni zaidi ya lengo la asilimia 50.5 ifikapo mwaka 2025/26.

### 2.2.9. Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo

Utekelezaji wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa katika tasnia ya utamaduni, Sanaa na Michazo umejikita katika hatua za kimkakati zinazochochea uchumi shindani na shirikishi hususani kuweka mazingira rafiki yatakayochochea ukuaji wa tasnia, ajira, kuongeza mchango kwa Pato la Taifa. Sekta hii inajumuisha shughuli za michezo, muziki, filamu, ngoma, tamthilia, vichekesho, sarakasi na kazi za mikono kama vile uchoraji, uchongaji, uhunzi, ufumaji, ushonaji na ususi pamoja na usanifu wa majengo na michezo ya kubahatisha. Katika mwaka 2023/24 miradi iliyotekelezwa ni pamoja na:

i. **Miradi ya Utamaduni: Mradi Na. 6521**

Kuimarisha Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Kukiuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa na Mradi Na. 6293: Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika. Utekelezaji wa miradi hii itawezesha kuenzi na kutambulisha tamaduni za watanzania na Afrika kwa ujumla duniani na hivyo kuongeza mapato ya Serikali kupitia utalii. Vile vile, kutawezesha kuitangaza lugha ya kiswahili, hivyo kuongeza watanzania watako pata ajira nje ya nchi.

ii. **Miradi ya Sanaa: Mradi Na. 4353:**

Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSUBa), na Mradi Na. 6502: Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania. Utekelezaji wa miradi hii umeongeza fursa za ajira hususan kwa vijana na kuimarisha ujuzi katika tasnia za sanaa na michezo, hivyo kupunguza umaskini nchini.

iii. **Miradi ya Michezo: Mradi Na. 6523**

Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam, Mradi Na. 6504 - Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi (Dar es Salaam na Dodoma); Mradi Na. 6503 - Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma; na Mradi Na. 6586 – Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Arusha. Kukamilika kwa miradi

hii kutaimarisha sekta ya michezo nchini na hivyo kuongeza fursa ya ushindani wa nchini katika masuala ya michezo kikanda, na kimataifa, ambapo kutapelekea Serikali kuongeza mapato kupitia uwekezaji wa makampuni ya michezo na kuzalisha fursa za ajira.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo ni pamoja na: kuongezeka kwa wataalam wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya Tanzania kutoka watanzania 56 mwaka 2019/20 hadi watanzania 113 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la watanzania 656 ifikapo mwaka 2025/26; Kuongezeka kwa idadi ya machapisho ya Kiswahili yaliyouzwa nje ya nchi kutoka machapisho 200 mwaka 2019/20 hadi kufikia machapisho 2,189 mwaka 2023/24 ikilinganisha na lengo la machapisho 700 mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa idadi ya wasanii /watalamu katika tasnia ya ubunifu/makundi yanayofanya maonesho yao nje ya nchi kutoka 1,620 mwaka 2019/20 hadi kufikia 1,968 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la 1,755 mwaka 2024/25.

### 2.2.10. Sekta ya Utalii

Sekta ya utalii ni mojawapo ya sekta za huduma, ambayo ina mchango mkubwa hususan kwenye pato la taifa, ajira na upatikanaji wa fedha za kigeni. Sekta hii inajumuisha hifadhi na mbuga za wanyamapori, maeneo tengefu, mimea, milima, mabonde, maporomoko na ukanda wa bahari. Serikali inaendelea na jitihada za kukuza sekta hii kwa kuendeleza mazao mapya ya utalii pamoja na kuendeleza kanda ya utalii ya kusini mwa Tanzania. Miradi iliyotekelezwa kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na:

i. **Miradi ya Uendelezaji wa Utalii: Mradi Na. 5203:**

Usimamizi wa Maliasili na Kuendeleza Utalii Kanda ya Kusini; na Mradi Na. 4812: Kukabiliana na Ujangili na Biashara Haramu ya wanyamapori.Utekelezaji wa miradi hii itawezesha kuzidi kuvutia watalii kutokana na kuongezeka kwa bidhaa mpya za utalii, kusaidia kukuza sekta nyingine ikiwemo uchukuzi, biashara, utamaduni, sanaa, michezo na afya, kuendeleza wajasiriamali pamoja na utunzaji wa utamaduni na mazingira. Vile vile, miradi hii pamoja na jitihada nyingine katika sekta zinatarajiwa kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni na kusaidia katika uagizaji wa bidhaa nje ya nchi katika sekta za huduma na biashara.

ii. **Miradi ya Kuongeza Bidhaa za Utalii: Mradi Na. 4651:**

Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki – BEVAC. Utekelezaji wa mradi huu utasaidia kupunguza kiwango cha uharibifu wa misitu na shughuli za ujasiriamali hususan kwa vijana. Aidha, mradi huu utasaidia kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya utalii hususan katika ujenzi wa migahawa na mahoteli yanayozingatia masuala asilia pamoja na kusaidia shughuli za kujifunza kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi hiyo ni pamoja na: kuongezeka kwa mapato yatokanayo na watalii kutoka Dola za Marekani bilioni 2.6 mwaka 2019/2020 hadi dola za Marekani bilioni 3.4 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 23 ya lengo la Dola za Marekani bilioni 6 kwa mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya watalii 1,527,230 mwaka 2019/20 hadi kufikia watalii 1,808,205 Mwaka 2023 sawa na

asilimia 8.09 ya lengo la watalii 5,000,0000 ifikapo 2025/26; na kuongezeka kwa ajira za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja na kufikia takriban ajira milioni 3.6 mwaka 2023/24.

### 2.2.11. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

Hifadhi ya mazingira ni muhimu katika kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kutokana na athari zake katika maendeleo ya kiuchumi kijamii na maisha ya viumbe hai. Aidha, sekta hii ina mchango mkubwa katika sekta nyingine hususan za uzalishaji na huduma kama vile sekta ya kilimo, maliasili na utalii na huduma za usafirishaji, uchukuzi na nishati. Hivyo, jitihada za kimkakati za kuhakikisha mazingira yanahifadhiwa ni muhimu, kwa maendeleo endelevu na matumizi bora ya rasilimali. Miradi iliyotekelezwa kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na:

i. **Miradi ya uhifadhi wa mazingira: Programu Na. 6571:**

Utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004 inayojumuisha miradi ya Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Nyasa, na Mradi wa Ujenzi wa miundombinu ya kuzuia maji ya bahari kujaa na kuathiri maeneo ya makazi na kilimo katika fukwe za Swipwese- Pemba na Mikindani- Mtwara.

Uwekezaji katika uhifadhi wa mazingira ni kichocheo cha shughuli za utalii wa misitu, utunzaji wa vyanzo vya maji hivyo kuimarisha hali ya upatikanaji wa maji na uzalishaji wa umeme utokanao na maji, pamoja na kuweka makazi bora ya viumbe hai mbalimbali. Aidha, masuala ya ulinzi na usalama katika rasilimali maji yataimarika na hivyo kuchochea shughuli za uvuvi, kilimo cha umwagiliaji pamoja na kuimarisha usalama wa mali na maisha ya jamii kutokana na hali ya mazingira.

ii. **Miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi: Programu Na. 5301:**

Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi yenye miradi ya Mradi wa Kuhimili Athari ya Mabadiliko ya Tabia Nchi Kupitia Mifumo ya Ikolojia, Mradi wa Kurejesha Ardhi Iliyoharibika na Kuongeza Usalama wa Chakula katika Maeneo Kame ya Tanzania, na Mradi wa Usimamizi Jumuishi wa Mfumo Ikolojia na Urejeshwaji wa Uoto Asili na Hifadhi ya Bioanuai Tanzania. Miradi mingine ni pamoja na Mradi Na. 5305: Mpango wa Kitaifa wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu, na Mradi Na. 5304: Mradi wa Kujenga Uwezo wa Kutekeleza Mkataba wa Montreal Kuhusu Udhibiti wa Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni

Utekelezaji wa miradi hii umesaidia kuongeza kiwango cha uzalishaji katika sekta za uzalishaji hususan kilimo na hivyo kuchochea shughuli za uuzaji nje na uchakataji katika viwanda. Vile vile, miradi hii itaongeza uwezo wa uhifadhi wa nafaka, pamoja na shughuli za utalii wa misitu. Vile vile, utawezesha mabadiliko ya namna binadamu wanavyotekeleza shughuli zao kwa kuhimiza matumizi njia rafiki kwa mazingira katika shughuli mbalimbali za maendeleo kama vile matumizi ya nishati safi na upandaji miti.

### iii. Miradi ya usimamizi wa Maafa Nchini: Mradi Na. 6327:

Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali - Ujenzi wa Kituo cha Usimamizi wa Maafa Nchini, na Mradi Na. 6575: Kuimarisha Uwezo wa Kujiandaa na Kukabili Maafa. Miradi hii imewezesha kujenga uwezo wa mtu mmoja mmoja kukabiliana na maafa, utolewaji wa misaada wakati wa maafa pamoja na kujenga uwezo wa kukabiliana na mafia kabla hayajatokea.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi ya sekta ya uhifadhi wa mazingira na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi ni pamoja na: kuongezeka kwa mchango wa matumizi endelevu ya misitu, maji na rasilimali za bahari katika Pato la Taifa kutoka asilimia 4 mwaka 2019/20 hadi asilimia 5 mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo la asilimia 7; na ongezeko la matumizi ya nishati mbadala kutoka tani 100 mwaka 2019/20 kufikia tani 300 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 20 ya lengo la tani 100,000 kwa mwaka 2025/26.

## 2.2.12. Biashara, Uwekezaji na Diplomasia ya Uchumi

Biashara na uwekezaji ni sekta muhimu katika kukuza uchumi shindani na shirikishi pamoja na kuchangia pato la taifa na utoaji ajira. Kutokana na umuhimu huo, Serikali inaendelea na utekelezaji wa programu zitakazoimarisha mazingira ya uwekezaji, masoko ya ndani na kutumia fursa za masoko ya kikanda na kimataifa katika kukuza biashara. Aidha, masoko yanayolengwa ni yanayotoa fursa kwa bidhaa zinazozalishwa nchini.

Katika kipindi cha utekelezaji mwaka 2023/24, miradi ifuatayo imeendelea kutekelezwa: Mradi Na. 6260: Mradi wa Kuwezesha Taasisi zinazojihusisha na masuala ya biashara na masoko ya bidhaa; Mradi Na. 6391: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Vitega Uchumi, Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini; Mradi Na. 6389: Ujenzi wa Majengo ya Ofisi na Mradi Na. 6317: Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu.

Utekelezaji wa miradi hii umewezesha kukuza na kuboresha mazingira yakufanya biashara na uwekezaji; kukuza ushiriki wa watanzania na kampuni za ndani katika miradi ya kimkakati ambapo miradi ya uwekezaji inayomilikiwa na watanzania imeongezeka; kuongezeka kwa huduma za uwekezaji mahala pamoja (One Stop Facilitation Centre -OSC); kuongezeka kwa kasi ya utoaji leseni za viwanda vipya; kuongezeka kwa kasi ya ushirikiano kati ya sekta ya umma na binafsi; na kuongezeka kwa ushirikiano na nchi za nje katika Kidiplomasia uchumi.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango ni pamoja na: Mchango wa sekta ya biashara katika Pato la Taifa uliongezeka na kufikia asilimia 8.3 mwaka 2023; kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya bidhaa kwenda katika Soko la Ulaya hadi kufikia kiasi cha shilingi trilioni 3.8 mwaka 2023; kuongezeka kwa idadi ya miradi mipya ya kampuni iliyosajiliwa kutoka 269 mwaka 2019/20 hadi kampuni 509 mwaka 2023/24 ikiwa ni ongezeko la asilimia 88.6 ya lengo la kampuni 540 ifikapo 2025/26; kuongezeka kwa miradi mipya iliyosajiliwa na TIC kutoka 207 mwaka 2019/20 hadi miradi 469 mwaka 2023/24.

### 2.2.13. Sekta ya Afya

Sekta ya afya ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuchochea maendeleo ya jamii, uchumi pamoja na ustawi wa maendeleo ya watu. Sekta hii inajumuisha miundombinu, wataalamu, vifaa na vifaa tiba, dawa, na bima ya afya. Uwekezaji katika huduma za afya utawezesha kuongezeka nguvukazi itakayochochea ukuaji wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa msingi huo, kuwekeza katika sekta ya afya ni muhimu kwa kuboresha maisha ya watu yanayohusiana na afya na ustawi wa jamii.

Katika mwaka 2023/24, Serikali imeendelea kutekeleza miradi ya sekta ya afya kama ifuatavyo:

i. **Mradi wa uboreshaji wa hospitali ya taifa ni: Mradi Na. 5487:**

Hospitali ya Taifa ya Muhimbili. Kutekelezwa na kukamilika kwa mradi huu utasaidia katika kuhakikisha huduma za Kibingwa na Bingwa bobezi zinazotolewa kwa wananchi ni zenye ubora, kupunguza msongamano wakati wa utoaji huduma na hivyo kusaidia wananchi kupata huduma kwa uharaka zaidi ambapo utaongeza muda katika shughuli za uzalishaji. Vile vile, kuboresha hospitali ya taifa itasaidia katika kuvutia watalii wa afya kutoka sehemu mbalimbali za dunia na hivyo kuchochea mapato ya Serikali kupitia utalii.

ii. **Miradi ya uboreshaji wa hospitali maalumu ni: Mradi Na. 5491:**

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Mradi Na. 5412: Taasisi ya Saratani Ocean Road, na Mradi Na. 5424: Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi – Kibong'oto (Kilimanjaro). Kukamilika kwa miradi hii kutachochea utoaji wa huduma bora na wenye ufanisi kwa wagonjwa wanaosumbuliwa na magonjwa mbalimbali na hivyo kupunguza vifo vinavyohusiana na magonjwa husika. Aidha, kuboreshwa kwa hospitali maalumu utasaidia kuongeza ufanyaji wa tafiti za kisayansi na kutoa mafunzo kwa wataalamu wa afya.

iii. **Miradi ya uboreshaji wa hospitali za Rufaa za Kanda ni pamoja na: Mradi Na. 5428:**

Hospitali ya Benjamin Mkapa; Mradi Na. 5408: Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Ziwa – Chato; na Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa. Kukamilika kwa uboreshaji wa hospitali za rufaa za kanda zitawezesha kupunguza msongamano katika hospitali ya rufaa ya taifa kwa kuchukua baadhi ya majukumu ambayo yangetekelezwa na hospitali ya taifa na kutoa huduma za kitaalamu katika ngazi ya kanda. Vile vile, kukamilika kwa maboresho ya hospitali hizi kutaongeza uwezo wa kutoa huduma za dharura kwa uharaka zaidi na hivyo kusaidia kuokoa maisha ya watanzania wengi ambao wanategemewa katika kutekeleza shughuli mbalimbali za kiuchumi na kijamii.

iv. **Miradi ya Upatikanaji wa Dawa, Vifaa na Vifaa tiba: Mradi Na. 5444:**

Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa na Bidhaa za Afya; Mradi Na. 5432: Uimarishaji wa Huduma za Chanjo. Kukamilika kwa miradi hii kutarahisisha upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba na hivyo kupunguza vifo hususan vifo vya kina mama wajawazito na watoto na magonjwa yanayoweza kudhibitiwa. Vile vile, upatikanaji wa dawa, vifaa na vifaa tiba na kupunguza gharama za matibabu kwa wagonjwa.


**v. Miradi ya kudhibiti magonjwa (yanayoambukizwa na yasiyoambukizwa): Mradi Na. 5492:**

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP); Mradi Na. 5498: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma; na Mradi Na. 5403: Kudhibiti Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza. Kukamilika kwa Miradi hii kutasaidia kupunguza kuenea kwa magonjwa hatarishi ambayo yanaweza kusababisha vifo. Vile vile, kutaimarisha ustawi na ukuaji wa uchumi kutokana wananchi kuwa na afya bora ya kufanya kazi kwa ufanisi.

**vi. Mradi wa kujenga uwezo wa rasilimali watu: Mradi Na. 2204:**

Mafunzo na Maendeleo ya Wataalamu. Kukamilika kwa Mradi huu kutawezesha kuwa na watoa huduma wenye ujuzi na uledi wa kutosha na hivyo kuboresha utoaji wa huduma za afya.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango ni pamoja na: idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano, kwa kila vizazi hai 1000 imepungua kutoka vifo 50 mwaka 2019/20 hadi kufikia vifo 43 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 88.9 ya lengo la kufikia vifo 40 ifikapo 2025/26; idadi ya vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kwa kila vizazi hai 100,000 vimepungua kutoka vifo 220 mwaka 2019/20 hadi kufikia vifo 104 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 290 ya lengo la vifo 180 kufikia 2025/26; umri wa kuishi umeongezeka kutoka miaka 66 mwaka 2019/20 hadi kufikia miaka 66.7 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 11 ya lengo la kufikia miaka 68 mwaka 2025/26; na kiwango cha ueneaji wa UKIMWI kitaifa kimepungua kutoka asilimia 4.7 mwaka 2019/20 hadi kufikia asilimia 4.4 (kwa watu wenye umri wa zaidi ya miaka 15) mwaka 2023/24 ikilinganishwa na lengo kwa kufikia asilimi 3.1 ifikapo mwaka 2025/26



| 2019/20 | 2023/24 |
|---|---|
| 50 | 43 |

*idadi ya vifo vya watoto chini ya miaka mitano kwa mwaka imepungua*



| 2019/20 | 2023/24 |
|---|---|
| 220 | 104 |

*idadi ya vifo vya kina mama wajawazito wakati wa kujifungua imepungua.*

## 2.2.14. Ustawi na Maendeleo ya Jamii

Maendeleo na Ustawi wa Jamii unajumuisha uwezeshaji wananchi kiuchumi, ushirikishwaji wananchi katika shughuli za uzalishaji mali; na uboreshaji wa mazingira ya watu wenye mahitaji maalumu ili kupunguza umaskini wa kipato na utegemezi. Vile vile, masuala ya ustawi na maendeleo ya jamii yanahusisha masuala ya Jinsia katika kuleta usawa wa kijinsia kwa wanawake na wasichana, kukabiliana na ubaguzi wa kijinsia pamoja na unyanyasaji dhidi ya wanawake unaotokana mila na tamaduni zinazomkandamiza mwanamke. Katika kipindi cha Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/24 miradi inayoendelea kutekelezwa ni:

i. **Miradi ya Vyuo vya Maendeleo ya Jamii: Mradi Na. 6330:**

Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kukuza ujasiriamali na ustawi wa jamii kiuchumi kwa kutoa mafunzo ya vitendo na stadi za maisha na hivyo kusaidia kupunguza pengo la elimu, kuongeza fursa za ajira na kutoa fursa sawa za maendeleo kwa jamii.

ii. **Miradi ya Uwezeshaji wa Wanawake na Wajasiriamali:**

Mradi Na. 6259: Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango ya Maendeleo; Mradi Na. 6279: Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake; na Mradi Na. 6280: Mfuko wa Kuwezesha Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga). Kutekelezwa kwa miradi hii kutawezesha kutoa fursa sawa za elimu, ajira, na uongozi kwa wanawake na wasichana ambapo itasaidia kuongeza ushiriki wao kikamilifu katika maendeleo ya kiuchumi, kisiasa, na kijamii; kupunguza visa vya ukatili wa kijinsia na kuhakikisha haki za wanawake zinalindwa; kuwezesha wafanyabiashara ndogo ndogo kusaidia katika kuongeza fursa za ajira na kupunguza ukosefu wa ajira hususan kwa vijana pamoja na kukuza soko la ndani ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya uchumi wa ndani na kusaidia kupunguza utegemezi kwa bidhaa kutoka nje.

iii. **Miradi ya Huduma za Ustawi wa Jamii: Mradi Na. 5451:**

Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii na Mradi Na. 5414: Uhai na Maendeleo ya Mtoto. Utekelezaji wa miradi hii utawezesha kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama wa watoto walio katika mazingira hatarishi.

Mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa mpango ni pamoja na: kuongezeka kwa Idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa kutoka vituo 1,543 mwaka 2019/20 hadi kufikia vituo 3,862 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 38.9 kufikia lengo la vituo 7,500 ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya wazee wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure kutoka wazee 166,866 mwaka 2019/20 hadi kufikia wazee 365,284 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 59.9 ya lengo la wazee 500,000 ifikapo mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano kutoka watoto 12,068 mwaka 2019/20 hadi kufikia watoto 46,473 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 90.7 ya lengo la watoto 50,000 ifikapo mwaka 2025/26.

### 2.2.15. Sekta ya Elimu

Sekta ya Elimu ni sekta inayopewa kipaumbele ili kuinua ubora wa elimu na mafunzo na kuweka mifumo na taratibu zitakazowezesha kupata idadi kubwa ya Watanzania walioelimika na wanaopenda kujielimisha na wenye maarifa na ujuzi ili waweze kuchangia katika maendeleo ya Taifa na kuhimili ushindani. Ili kufikia azma hiyo Serikali imeendelea kutoa msukumo katika kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia. Katika kipindi cha mwaka 2023/24, miradi ifuatayo imeendelea kutekelezwa:

i. **Miradi ya Ugharamiaji wa elimu: Mradi Na. 4322 na 4393:**

Elimumsingi na Sekondari Bila Ada. Utekelezaji wa mradi huu umeongeza idadi ya wanafunzi wapya wanaoandikishwa katika ngazi mbalimbali za elimu na kuhakikisha wanafunzi wote wenye umri wa kwenda shule wanaenda.

ii. **Miradi ya Elimu ya awali, msingi, sekondari na vyuo vya kati: Mradi Na. 6327:**

Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali (ujenzi wa maboma na vyumba vya madarasa katika shule za awali, msingi, sekondari na elimu maalum); Mradi Na. 3280: Programu ya Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni – SWASH; Mradi Na. 4312: Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R); Mradi Na. 4390: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP); Mradi Na. 6390: Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA; Mradi Na. 4319: Kuboresha Elimu ya Awali na Msingi (Boost Primary Student Learning); na Mradi Na. 6352: Tume ya Nguvu za Atomiki – TAEC. Utekelezaji wa miradi hii umeboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia, upatikanaji wa vitabu vya kiada na ziada, kuimarisha ufundishaji na ujifunzaji, kuongezeka kwa kiwango cha usajili katika vyuo vya kati, kuimarisha upatikanaji wa maji shuleni na usafi wa mazingira, na kuongeza fursa ya elimu kwa wanafunzi wenye mahitaji maalum.

iii. **Miradi ya Utafiti: Mradi Na. 6345:**

Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH. Mradi huu utasaidia kupatikana kwa bidhaa, teknolojia na ubunifu utakaowezesha wananchi kuongeza ufanisi katika shughuli za maendeleo ya kichumi na kijamii.

iv. **Miradi ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Mafunzo ya Amali): Mradi Na. 4397:**

Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi; na Mradi Na. 6229: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi – FDC. Utekelezaji wa miradi hii kumeimarisha miundombinu ya kufundishia na kujifunzia katika Taasisi za Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi nchini. Hivyo, kuwezesha wanafunzi kujifunza kwa vitendo na kuongezeka kwa udahili.

v. **Miradi ya Elimu ya Juu: Mradi Na. 6321:**

Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA); Mradi Na. 4341: Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K Nyerere Cha Kilimo na Teknolojia; Mradi Na. 6206: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP); Mradi namba 6327: Ujenzi na ukarabati wa majengo wa Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA); Mradi Na. 4315: Mradi wa kuendeleza Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation Project - HEET); Mradi Na. 4340: Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu; na Mradi Na. 6322: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM). Utekelezaji wa miradi hii umesaidia kuongeza kiwango cha udahili, kuimarisha utoaji huduma katika vyuo vikuu na kuongeza wigo wa upatikanaji wa mikopo kwa wanafunzi wenye sifa.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango ni pamoja na: Idadi ya wastani ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya ufundi imeongezeka kutoka wanafunzi 160,000 mwaka 2019/20 hadi kufikia wanafunzi 235,804 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 14.0 ya lengo la kudahili wanafunzi 700,000 ifikapo mwaka 2025/26; Idadi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya ufundi imeongezeka kutoka wanafunzi 118,270 mwaka 2019/20 hadi kufikia wanafunzi 167,980 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 56 ya lengo la kufikia wanafunzi 207,518 ifikapo 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya wakufunzi kutoka wakufunzi 10,072 mwaka 2019/20 hadi kufikia 10,948 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 17.8 ya lengo la kufikia wakufunzi 15,000 ifikapo mwaka 2025/26; Kuongezeka kwa idadi ya wahitimu wa ufundi na mafunzo kutoka 118,270 mwaka 2019/20 hadi kufikia 154,765 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 40.9 ya lengo la wahitimu 207,518 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa Idadi ya walio katika mafunzo mahali pa kazi kutoka 46,200 mwaka 2019/20 hadi kufikia watu 123,890 sawa na asilimia 42 ya lengo la kufikia watu 231,000 ifikapo 2025/26; kuongezeka kwa idadi wa walimu wenye sifa katika shule za msingi hadi kufikia walimu 278,873 mwaka 2023/24; na kuongezeka kwa idadi wa walimu wenye sifa katika shule za sekondari hadi kufikia walimu 94,919 mwaka 2023/24.

### 2.2.16. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Matumizi bora ya ardhi ni msingi wa maendeleo endelevu kiuchumi, kijamii na uhifadhi wa mazingira na maliasili. Ardhi iliyopimwa na kupangwa kwa uthabiti uchochea shughuli za uwekezaji, pamoja na mpangilio bora wa makazi ya watu hivyo kurahisisha maendeleo ya uwekaji wa miundombinu wezeshi ya kijamii na kiuchumi kama vile vituo vya afya, shule, maji, barabara, na umeme. Aidha, rasilimali ardhi iliyopimwa na kumilikishwa, ni moja ya chanzo cha mapato kwa Serikali. Hili kuhakikisha ardhi inapangwa na kupimwa na kuongeza mchango wa sekta ya ardhi katika sekta za uzalishaji pamoja na ukuaji wa sekta husika, miradi, programu, na shughuli mbalimbali za maendeleo zilizotekelezwa kwa mwaka 2023/24 ni kama ifuatavyo:

i. **Miradi ya Upangaji na Upimaji wa Ardhi: Mradi Na. 2326:**

Programu ya Kupanga, Kupima na Kumilikisha; Mradi Na. 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi; Mradi Na 2329: Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani; Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali. Utekelezaji wa miradi hii utachochea shughuli za uwekezaji kupitia uanishaji wa ardhi ambayo imepimwa kwa ajili ya



2023/24

**278,873**

*kuongezeka kwa idadi ya walimu wenye sifa shule za msingi*



2023/24

**10,948**

*kuongezeka kwa idadi ya wakufunzi*

wawekezaji, kuhamasha makazi bora na yasiyo holela hali itakayochangia utulivu na amani katika jamii na kitaifa kwa ujumla. Aidha mafanikio yaliyopatikana kutokana na utekelezaji wa miradi hii ni pamoja na uandaaji wa mipango kina ya matumizi ya ardhi ya vijiji na mipango ya matumizi ya ardhi katika shoroba za mradi ya kielelezo ya SGR, Bomba la Mafuta (EACOP) na mradi wa uzalishaji wa Umeme wa Mwalimu Nyerere (JNHPP).

**ii. Miradi ya Umilikishaji:**

Eneo hili linajumuishsa miradi iliyolenga kuongeza kiwango cha umiliki wa ardhi kupitia utoaji wa haki za hati miliki za ardhi, pamoja na uwekaji wa mipaka ya kimataifa ambapo miradi iliyotekelezwa ni Mradi Na. 2324: na Mradi wa Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa; Mradi Na. 495: Uboreshaji wa Milki za Ardhi. Utekelezaji wa miradi hii utapanua wigo wa mapato ya kodi kwa Serikali, pamoja na kuimalisha usalama wan chi hsuusan kwa jamii zinazoishi maeneo ya mipakani.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango ni pamoja na: kuongezeka kwa idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyo rasmi kutoka 1,496,357 mwaka 2019/20 hadi kufikia 1,796,357 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asimilia 37.5 ya lengo la mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya mabaraza ya ardhi ya Wilaya yanayofanya kazi kutoka mabaraza 57 mwaka 2019/20 hadi 104 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 57 ya lengo la mabaraza 139 ifikapo 2025/26; kupungua kwa maeneo ya ardhi yenye makazi yasiyo rasmi kutoka asilimia 70 mwaka 2019/20 hadi asilimia 55 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 33.3 ya lengo la maeneo ya asilimia 25 mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohuishwa kutoka miji 24 mwaka 2019/20 hadi miji 28 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 13.3 ya lengo lengo la miji 54 mwaka 2025/26.

### 2.2.17. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira

Sekta ya maji ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuchochea shughuli za kiuchumi na kijamii, hususan upatikanaji na usambazaji wa maji safi na salama na utunzaji wa vyanzo vya maji na mazingira. Sekta hii inawezesha uwekezaji katika sekta za uzalishaji kwa kuhakikisha upatikanaji wa maji ya kutosha. Miradi iliyotekelezwa kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na:

**i. Miradi ya Kuboresha Huduma za Maji Vijijini: Mradi Na. 3280:**

Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini. Utekelezaji wa mradi huu na mingine ya kupeleka maji vijijini itasaidia kupunguza muda wa utafutaji maji kwa wananchi hususan wanawake na watoto, kupunguza magonjwa ya mlipuko vijijini, na kusaidia upatikanaji wa elimu katika muda unaotakiwa kutokana na watoto kuhudhuria masomo kwa wakati. Aidha, miradi hii kwa ujumla itasaidia kuboresha shughuli za umwagiliaji wa mazao katika maeneo ya vijijini na kukuza shughuli za ujasiriamali unaotokana na bidhaa za kilimo.

**ii. Miradi ya Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji Mijini na katika Miji Mikuu ya Mikoa: Mradi Na. 3306:**

Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa (ujenzi na ukarabati wa miundombinu katika miji ya Dodoma, Mwanza, Morogoro,

Shinyanga na Mbeya; ujenzi na upanuzi wa miundombinu ya majitaka katika miji ya Musoma, Babati na Bukoba); mradi Na. 3307: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa; mradi Na. 3341: Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe; mradi Na. 3403: Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga na Miji Mingine. Kukamilika kwa miradi hii itasaidia kuboresha utoaji wa huduma za maji majumbani na uendelezaji wa sekta za uzalishaji hususan viwanda, upatikanaji wa ajira na uboreshaji wa shughuli za biashara.

iii. **Miradi ya Kuboresha Huduma za Maji Katika Jiji la Dar es Salaam: Mradi Na. 3437:**

Kuboresha Huduma za Maji Katika Jiji la Dar es Salaam; na mradi Na. 3438: Mradi wa Bwawa la Kidunda. Kukamilika kwa miradi hii kutawezesha uboreshaji wa usambazaji maji na usafi wa mazingira katika maeneo ya Dar es Salaam na Pwani pamoja na huduma za majitaka kwa kushirikiana na sekta binafsi. Aidha, miradi hii inatarajiwa kuongeza shughuli za uzalishaji viwandani, kujenga imani kwa wawekezaji, kuongeza mchango wa sekta ya maji katika pato la Taifa kupitia mapato ya ankara za maji kutokana na kuwa na watumiaji wengi na kupunguza athari za mafuriko katika mto Ruvu na pamoja kuwezesha upatikanaji wa maji ya uhakika katika Jiji kutokana na uhifadhi wa maji katika bwawa.

iv. **Miradi ya Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini: mradi Na. 3435:**

Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia; na mradi Na. 6545: Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini. Utekelezaji wa Miradi hii utachagiza katika kukuza kilimo cha umwagiliaji kutokana na kuwa na maji ya uhakika (uhakika wa chakula), uendelezaji wa utalii kupitia mabonde na uzalishaji wa nishati ya umeme kupitia mitambo ya kufua umeme kwa maji.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango ni pamoja na: Kuongezeka kwa uwiano wa kaya za vijijini nchini zinazopata maji safi na salama kutoka katika vyanzo vilivyoboreshwa kutoka asilimia 36 mwaka 2019/20 hadi asilimia 56.1 mwaka 2022 sawa asilimia 52 ya kufikia lengo la asilimia 75 ifikapo 2025/26; na kuongezeka kwa asilimia ya watu mijini wanaopata maji safi na salama kutoka katika vyanzo vilivyoboreshwa kutoka asilimia 84 mwaka 2019/20 hadi kufikia asilimia 91.5 mwaka 2022 sawa na asilimia ya 68 kufikia lengo la asilimia 95 mwaka 2025/26.

### 2.2.18. Utawala Bora na Utawala wa Sheria

Serikali imeendelea kuimarisha mifumo ya kitaasisi na kiutendaji ya utawala bora, utawala wa Sheria na utoaji haki ili kudumisha amani, utulivu na usalama. Eneo hili linajumuisha mifumo ya Mahakama, mifumo ya utoaji haki, vyombo vya ulinzi na usalama, Utumishi wa Umma na Utawala Bora na Bunge. Miradi iliyotekelezwa kwa mwaka 2023/24 ni pamoja na:

i. **Miradi ya Kupambana na rushwa: Mradi Na. 5502:**

Kujenga Mfumo Endelevu wa Mpango Kazi wa Kupambana na Rushwa Tanzania. Utekelezaji wa mradi huu utawezesha kupungua kwa rushwa na kuimarisha upatikaji wa huduma za kijamii kwa haki na usawa.

ii. **Miradi ya Kuimarisha Shughuli za Bunge: Mradi Na. 6360:**

Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge, Mradi Na.6318: Ukarabati wa Majengo ya Bunge; Mradi Na. 6360: Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge; Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi ya Bunge; Mradi Na. 6251: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP). Utekelezaji wa miradi hii utawezesha kuboresha shughuli za Bunge ikiwemo utungaji wa sheria na kuishauri Serikali.

iii. **Miradi ya Mahakama:**

Mradi Na. 6310: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Wilaya; Mradi Na. 6312: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo; Mradi Na 6314 - Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama kuu; Mradi Na. 6215: Mradi wa uboreshaji wa huduma za Mahakama (Citizen Centic Judiciary Modernisation Project). Kukamilika kwa miradi hii kutachangia kupungua kwa mashauri mahakamani kutokana na kuwepo kwa huduma za mahakama katika jamii. Hivyo, kurahisisha upatikanaji wa haki na kuongeza muda katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo ya kichumi

iv. **Miradi ya Utawala Bora:**

Mradi Na. 5502: Kujenga Mfumo Endelevu wa Mpango Kazi wa Kupambana na Rushwa Tanzania; Mradi Na. 5507: Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake na Watoto wa Kike; Mradi Na. 5508: Program ya Upatikanaji Haki kwa Maendeleo Endelevu; na Mradi Na. 6201: Haki Mtandao; Mradi Na. 6517: Kuimarisha Haki za Mtoto; Mradi Na. 6501: Vitambulisho vya Taifa. Kukamilika kwa miradi hii kutaimarisha mifumo ya upatikanaji wa haki na huduma za kijamii. Hivyo, kuwezesha kulindwa kwa haki za watoto na wanawake katika jamii na kuwawezesha kuwa na afya njema ya akili itakayochangia katika uzalishaji kwa kufanya kazi kwa tija.

v. **Miradi ya Majengo ya Serikali: Mradi Na. 6389:**

Ujenzi wa Majengo ya Ofisi unaojumuisha ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Viongozi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Viongozi katika Tawala za Mikoa; Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu; Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; na Ujenzi wa Mji wa Serikali – Mtumba. Kukamilika kwa mradi huu kutachangia kuimarika kwa miundombinu ya utoaji wa huduma kwa umma.

vi. **Miradi ya Usalama wa Raia:**

Mradi Na. 6302: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Tanzania Bara; Mradi Na. 6303: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Zanzibar; Mradi Na. 6305: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi; Mradi Na. 2330: Upimaji wa Maeneo na Ulipaji Fidia; Mradi Na. 4491: Kuboresha upatikanaji wa Maji safi Magerezani; Mradi Na. 6582: Upanuzi wa Huduma za Zimamoto; na Mradi Na. 6301: Ujenzi wa Ofisi za Mikoa za Uhamiaji. Kutekelezwa kwa miradi hii kutachangia kuimarika kwa amani na usalama nchini.

vii. **Miradi ya Utumishi wa Umma: Mradi Na. 6284:**

Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu; Mradi Na. 6315: Ujenzi wa Makazi ya Viongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa; Mradi Na.

6339 Ukarabati wa Nyumba za Serikali. Utekelezaji wa mradi hii utaisaidia katika kuimarisha utendaji wa watumishi katika utoaji wa huduma pamoja na kuimarisha hali ya utawala nchini na hivyo kuimarisha shughuli za kiuchumi na kijamii.

Mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa mpango wa mwaka 2023/24 ni pamoja na: Kuongezeka kwa asilimia ya raia wanaoishi katika mikoa yenye Mahakama Kuu inayofanya kazi kutoka asilimia 69 mwaka 2019/20 hadi asilimia 80 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 35 ya lengo la mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya majengo ya mahakama za wilaya yaliyojengwa kutoka majengo 64 mwaka 2019/20 hadi majengo 124 mwaka 2023/24 sawa na asilimia 80 ya lengo la mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa idadi ya majengo ya mahakama za mwanzo yaliyojengwa kutoka majengo 649 mwaka 2019/20 hadi majengo 721 mwaka 2023/24 sawa na 50.7 ya lengo la mwaka 2025/26. Mafanikio haya yamepelekea kuimarika kwa utoaji haki nchini na kuimarika kwa utawala bora na wa sheria.

### 2.2.19. Ujuzi na Uwezeshaji

Ujuzi na uwezeshaji rasilimali watu ni nyenzo muhimu katika kufikia maendeleo ya Uchumi kwa kutoa fursa za ajira, kukuza uzalishaji na ubunifu, kuvutia uwekezaji na kupunguza umaskini.

Katika kipindi cha utekelezaji mwaka 2023/24, miradi ifuatayo imeendelea kutekelezwa: Mradi Na.6581: Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi nchini; Mradi Na.4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; Mradi Na.6205: Programu ya Taifa ya Kukuza kazi za Staha; na Mradi Na.4954: Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu.

Utekelezaji wa miradi hii umesaidia vijana kuajiriwa na kujiajili kutokana na mafunzo ya kukuza ujuzi kwa njia ya uanagenzi (Apprenticeship) katika fani mbalimbali za ufundi stadi; kuongezeka kwa bidhaa zinazotengenezwa na vikundi vya vijana vilivyohitimu mafunzo ya ufundi stadi katika ngazi za halmashauri; kuongezeka kwa idadi ya vikundi vya vijana wenye ujuzi wanaokopesheka na kurejesha mikopo; na kuongezeka kwa wajasiriamali waliopatiwa mafunzo ya ufundi na ufundi stadi katika maeneo yasiyo rasmi.

Mafaniko yaliyopatikana katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kukuza ujuzi na uwezeshaji rasilimali watu nchini ni kama ifuatavyo: kuongezeka kwa idadi ya wastani ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya ufundi kutoka wanafunzi 160,000 mwaka 2019/20 hadi wanafunzi 235,840 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 14.01 ya lengo la wanafunzi 700,000 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya wastani ya udahili katika vyuo vya ufundi na mafunzo kutoka wanafunzi 4,890 mwaka 2019/20 hadi wanafunzi 454,937 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 45.2 ya lengo la wanafunzi 1,000,000 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya ufundi kutoka wanafunzi 135,200 mwaka 2019/20 hadi wanafunzi 167,980 mwaka 2023/24 sawa na ongezeko la asilimia 6 ya lengo la wanafunzi 680,000 mwaka 2025/26; kuongezeka kwa asilimia

ya wafanyakazi wenye viwango vya juu vya ujuzi kufikia asilimia 5.2 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 3.3 mwaka 2019/20 ikiwa ni ongezeko la asilimia 1.9 ya lengo la asilimia 12.1 mwaka 2025/26; na kuongezeka kwa asilimia ya wafanyakazi wenye viwango vya kati vya ujuzi kufikia asilimia 42 mwaka 2023/24 kutoka asilimia 33.7 mwaka 2019/20 ikiwa ni ongezeko la asilimia 8.3 ya lengo la asilimia 12.1 mwaka 2025/26.

**2023/24**

**235,840**

*idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya ufundi*

**2023/24**

**454,937**

*idadi ya wastani ya udahili katika vyuo vya ufundi na mafunzo kwa wanafunzi*

**2023/24**

**5.2%**

*kuongezeka kwa idadi ya wafanyakazi wenye viwango vya juu vya ujuzi*

**2023/24**

**167,980**

*idadi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya ufundi imeongezeka*

### 2.2.20. Sekta ya Fedha

Sekta ya fedha iliyo imara ni miongoni mwa vichocheo muhimu vya ukuaji wa uchumi na ustawi wa jamii, ambapo inawezesha sekta ya umma na sekta binafsi kupata vyanzo vya mitaji kwa ajili ya uwekazaji na biashara. Katika mwaka 2023/24 Serikali imeendelea kutelekeza miradi ya Benki ya Maendeleo TIB, Benki ya Maendeleo ya Kilimo – TADB, Huduma za Bima, na huduma ndogo za fedha. Kutekelezwa kwa miradi hii kutawezesha wananchi hususani wa maeneo ya vijijini kuweza kupata huduma za kifedha ikiwemo mikopo na hivyo kuongeza ufanisi katika shuguli zao kiuchumi na kijamii. Mafanikio yaliyopatika katika utekelezaji wa miradi mbalimbali ya kuboresha sekta ya fedha ni pamoja na: kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya jumla ya shilingi bilioni 161.1 katika sekta ya kilimo na benki ya TADB; Kutolewa kwa leseni 884 kwa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo (SACCOS); na kutolewa kwa mikopo yenye thamani ya shilingi bilioni 7.18 katika sekta mbalimbali za kiuchumi na kijamii na Benki ya Maendeleo – TIB. Utolewaji wa mikopo uliwezesha kuimarisha shughuli za kilimo ikiwemo matumizi ya zana bora za kilimo na pembejeo, hivyo kuongeza uzalishaji. Vile vile, mikopo hii ilichangia kuongezeka kwa uwekezaji katika sekta za uzalishaji na huduma.

**161.1 bil.**
**thamani ya mikopo**

*kutolewa kwa mikopo katika sekta ya kilimo*

**884**
**jumla ya leseni**

*kutolewa kwa leseni kwa vyama vya ushirika wa akiba na mikopo*

### 2.2.21. Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Serikali inaendelea kuweka mazingira wezeshi na salama ili kuvutia uwekezaji na mitaji kutoka sekta binafsi. Aidha, Serikali imekuwa ikishirikiana na sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi na programu mbalimbali za maendeleo kupitia utaratibu wa PPP na Joint Venture. Katika kuleta ufanisi wa utekelezaji wa miradi ya maendeleo utaratibu wa PPP, Serikali imeasha Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi (PPP Centre).

Hatua za kimkakati zilizoainishwa katika Mpango Wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano Mpango wa maendeleo wa taifa katika kuendeleza ubia kati ya sekta binafsi na umma ni pamoja na: kutumia vyanzo binafsi vilivyopo na kuwekeza kupitia utaratibu wa Joint Venture (JV) na ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP); na kuendelea kutumia rasilimali binafsi kuwekeza katika shughuli mbalimbali za uzalishaji ambazo ni za kibiashara na hazihitaji rasilimali za umma.

Katika utekelezaji wa Mpango, Serikali imeendelea kutekeleza miradi mbalimbali kama ifuatavyo: ujenzi wa barabara ya tozo kutoka Kibaha - Chalinze (km 78.9) na Chalinze – Morogoro (km 126.1); ujenzi wa Kituo cha Mazoezi Tiba Mbweni Dar es Salaam; uendeshaji wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Pili na ya Tatu; Mradi wa Hosteli za wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi Dar es Salaam; Mradi wa Kuimarisha Huduma za Saratani nchini kwa kujenga Kituo cha Ubingwa Bobezi wa Tiba ya Saratani eneo la Mloganzila (Ultra - Modern Oncology Centre - UMOC) na Kituo cha Saratani Mbeya (Mbeya Cancer Centre - MCC) eneo la Iwambi- Mbeya.

## 2.2.22. Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Uhamasishaji Uwekezaji Nchini

### *2.2.22.1. Uboreshaji Mazingira ya Biashara*

Serikali imeendelea kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Kufanya Biashara na Uwekezaji nchini (MKUMBI). Katika mwaka 2023, utekelezaji wa Mpango uliwezesha kufutwa au kupunguzwa kwa tozo na ada 66 ikilinganishwa na tozo na ada 39 zilizofutwa au kupunguzwa mwaka 2022. Aidha, mfumo wa Government Enterprises Service Bus (GovESB) umeendelea kuwezesha mifumo ya Serikali kuwasiliana kwa urahisi na kubadilishana taarifa na hivyo kuokoa gharama, muda pamoja na kurahisisha utoaji wa huduma kwa mwananchi na wawekezaji kwa kuwa taarifa zote zinapatikana katika dirisha moja. Hadi Desemba 2023, mifumo 90 ya taasisi 83 za umma iliunganishwa katika mfumo wa Government Enterprises Service Bus (GovESB) ikilinganishwa na mifumo 50 ya taasisi za umma 45 iliyounganishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022.Kwa upande mwingine, Mfumo wa Kieletroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini - GePG ambao umerahisisha taratibu za ulipaji wa ada na tozo mbalimbali za Serikali, kuondoa usumbufu wa watu kutembea ofisi mbalimbali kwa ajili ya kufanya malipo, kuongeza uwazi katika ukusanyaji wa mapato, na kupunguza muda wa kufanya malipo uliendelea kuboreshwa. Hadi Desemba 2023, watoa huduma 983 waliunganishwa katika mfumo wa GePG kutoka watoa huduma 900 waliounganishwa katika kipindi kama hicho mwaka 2022, sawa na ongezeko la asilimia 9.2.

Mwaka 2023, Serikali ilifanya marekebisho ya sheria mbalimbali zilizolenga kuweka unafuu katika mazingira ya biashara na uwekezaji zilizoidhinishwa na Bunge kupitia Sheria ya Fedha ya mwaka 2023 na Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Miscellaneous Amandements) za mwaka 2023. Sheria zilizofanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Fedha ya Mwaka 2023 na kuleta unafuu katika mazingira ya biashara ni: Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani, SURA 148; Sheria ya Kodi ya Mapato, SURA 332; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147; Sheria ya Usimamizi wa Kodi, SURA 438; Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa, SURA 290; Sheria ya Mifumo ya Malipo ya Taifa, 2015; Sheria ya Posta na Mawasiliano ya Kielektroniki, SURA 306; Sheria ya Ardhi, SURA 113;Sheria ya Madini, SURA 123; Sheria ya Kuendeleza Ufundi Stadi, SURA 82; Sheria ya Michezo ya Kubahatisha, SURA 41; Sheria ya Usafirishaji Bidhaa Nje ya Nchi, SURA 196; na Sheria ya Mamlaka ya Mapato Tanzania, Sura 399.

Sheria zilizofanyiwa marekebisho kupitia Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali (Miscellaneous Amandements) ni: Sheria ya Maendeleo ya Biashara Sura ya 155; Sheria ya Wakala wa Vipimo Sura Na. 340; Sheria ya Taifa ya Leseni za Viwanda Sura ya 46; Sheria ya Viwanda Vidogo na Biashara Ndogo Sura ya 112; Sheria za EPZA Sura ya 373; Sheria ya SEZ Sura ya 420; Sheria ya Tume ya Mionzi Sura ya 188; Sheria ya TIRDO Sura ya 159; Sheria ya Ushuru wa Bidhaa, SURA 147; Sheria ya Kodi ya Mapato Sura ya 332; Sheria ya Mamlaka ya Mapato Sura ya 399; Sheria ya Fidia kwa Wafanyakazi Sura ya 263, na Sheria ya VAT Sura ya 148. Maboresho ya haya kisheria ni hatua muhimu katika kuhakikisha mazingira ya biashara na uwekezaji yana imarika.

Katika hatua nyingine ya kuboresha mazingira ya biashara hasa kufanya malipo kwenye mamlaka za urekebu, serikali imechukua za kurekebisha mifumo ya taasisi ambazo zina sura moja ya utoaji wa huduma za malipo na kuanza kulipa kwa kutumia Namba Moja ya Malipo (Control Number). Baadhi ya maeneo ambayo yameanza kutumia Control Number moja kwa malipo ya ni katika biashara za mifugo minadani ambapo taasisi zilizokuwa zinahusika na ukusanyaji mapato yaani Mamlaka za Serikali za Mitaa (Halmashauri) na Wizara ya Mifugo kwa kila moja kutoa Control Namba yake. Hivi sasa taasisi hizi mbili zinatumia control number moja na hivyo kuwapunguzia wafanyabiashara usumbufu wa kulipa malipo ya Serikali kwa mamlaka zaidi ya moja. Serikali inaendelea kuchukua hatua taasisi zingine zikiwepo Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na Mamlaka ya Bandari (TPA) ili mifumo yake ya malipo inayohusiana iweze kutumia Control Number moja. Utaratibu huu utakapokamilika, Serikali inatarajia kutoa mwongozo maalumu ya ulipaji kwa kutumia utaratibu wa dirisha moja la malipo (Single Window Payment System).

Serikali imekamilisha taarifa ya tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI) kuanzia mwaka 2019 - 2023, tathmini hii imeonyesha mambo yaliyofanyika na namna ambavyo yameweza kuwezesha sekta binafsi hasa wawekezaji wa ndani na nje kuwa na mazingira bora ya ufanyaji shughuli zao za uwekezaji na biashara yenye ushindani na ufanisi.

### *2.2.22.2. Uhamasishaji Uwekezaji Nchini*

**i. Kuanzisha Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji:**

Katika mwaka 2023/24, Serikali imekamilisha ujenzi wa Mfumo wa Kielektroniki wa Kuhudumia Wawekezaji (Tanzania Electronic Investment Window - TeIW) ambao umeunganishwa na mifumo ya Taasisi saba (7) ambazo ni Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), Idara ya Uhamiaji, Idara ya Kazi, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA), Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi na TIC. Mfumo huo, unamwezesha mwekezaji kusajili mradi popote ndani na nje ya nchi na kupata vibali vya uwekezaji ndani ya siku 3 ikiwa ametimiza vigezo. Awamu ya pili ya ujenzi wa mfumo huo itahusisha uunganishaji wa Taasisi nyingine saba (7) ambazo ni Shirika la Umeme Tanzania (TANESCO), Shirika la Viwango Tanzania (TBS), Mamlaka ya Dawa na Vifaa Tiba (TMDA), Baraza la Usimamizi wa Mazingira (NEMC), Wizara ya Kilimo, Tume ya Madini na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA).

**ii. Uanzishwaji na Uendelezaji wa Maeneo Maalum ya Kiuchumi na Miradi ya Kimkakati:**

Serikali imeendelea kuratibu uanzishwaji na uendelezaji wa miradi ya maeneo maalum ya kiuchumi na miradi ya uwekezaji ya kimkakati inayotekelezwa na sekta binafsi na sekta ya umma ikiwemo kongani ya viwanda ya Modern Industrial Park (KAMAKA) iliyopo Kikongo, Mlandizi, Wilaya ya Kibaha mkoa wa Pwani yenye

ukubwa wa ekari 1,077. Kongani hiyo itakapokamilika itavutia viwanda 210 vitakavyozalisha ajira mpya za moja kwa moja 30,000 na zisizo za moja kwa moja 200,000. Jumla ya uwekezaji unaotarajiwa katika mradi huu ni dola za Marekani milioni 51 ikihusisha ujenzi wa miundombinu ya kongani na dola za Marekani bilioni 1.3 ikihusisha uwekezaji wa viwanda ndani ya kongani; Ujenzi wa Sino Industrial Park unaotekelezwa na Kampuni ya Group VI International katika eneo la Kwala mkoani Pwani yenye ukubwa wa ekari 2,500 ambapo uendelezaji wake utagharimu dola za Marekani milioni 327.4. Aidha, mradi huo unatarajia kuvutia viwanda vikubwa 200 na viwanda vidogo 300 vitakavyowekeza mtaji wa dola za Marekani bilioni 3 na kutoa ajira 100,000 za moja kwa moja na 500,000 zisizo za moja kwa moja. Hadi kufikia Machi, 2024, kampuni ya SINO-TAN imesaini jumla ya Hati za Makubaliano 15 na wawekezaji 50 walioonesha utayari wa kuwekeza katika eneo la kongani hiy; na ujenzi wa kongani ya viwanda ya Elsewedy Industrial Park inatarajiwa kujengwa eneo la Kikongo, Mlandizi mkoa wa Pwani itakayokuwa na ukubwa wa ekari 650. Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Elsewedy Eletric na inahusisha eneo lenye ukubwa wa ekari 500 ambapo uendelezaji wake utagharimu dola za Marekani milioni 460. Mradi utavutia ujenzi na viwanda takribani 150 vitakavyowekezwa na kuzalisha ajira mpya za moja kwa moja na zisizo za moja kwa moja 50,000.

Aidha, miradi mingine mikubwa ya kimkakati iliyoanza ujenzi na uzalishaji yenye matokeo chanya ya kiuchumi katika kuvutia mitaji, ajira, fedha za kigeni na teknolojia mpya ni pamoja na kiwanda cha Sapphire Float Glass kilichopo Mkuranga, Pwani chenye thamani ya dola za Marekani milioni 311 (sawa na shilingi bilioni 700) chenye uwezo wa kuzalisha tani 700 za kioo na ajira za moja kwa moja 1,655 na zisizo za moja kwa moja 6,000; kiwanda cha mbolea cha Itracom Fertilisers kilichopo Nala Jijini Dodoma; kiwanda cha sukari cha Mkulazi Holdings Limited kilichopo Mbigiri, Morogoro; kiwanda cha kuchakata gesi asilia kwa ajili ya nishati ya magari cha kampuni ya Taqa Dalbit, Jijini Dar es Salaam; mradi mkubwa wa kilimo cha miwa na kiwanda cha sukari cha Kasulu sugar project kilichopo Kasulu, Mkoani Kigoma; upanuzi wa viwanda vya kuzalisha sukari kwa viwanda vya Kagera Sugar, Kilombero Sugar na Mtibwa Sugar; na kiwanda cha uzalishaji wa kioo kwa ajii ya majengo cha Keda Tanzania Ceramics Limited kilichopo Mkuranga, Mkoani Pwani.

**$51 mil.**
**thamani ya uwekezaji**

*ujenzi wa miundombinu ya viwanda vya Kongani*

TZS

**2500**
**ukubwa wa ekari**

*ujenzi wa Sino Industrial Park katika eneo la Kwala - Pwani*


**600,000**
**idadi ya ajira.**

*mradi wa viwanda vikubwa na vidogo takribani 500.*


## 2.3. Changamoto na Hatua za kukabiliana nazo katika utekelezaji wa Mpango wa 2023/24

### 2.3.1. Changamoto za Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Mwaka 2023/24

Kutokana na zoezi la ufuatiliaji na tathmini lililofanyika katika vipindi vya robo ya kwanza na ya pili ya mwaka 2023/24, changamoto mbalimbali zilijitokeza katika utekelezaji wa Mpango.




### 2.3.2. Hatua Zilizochukuliwa Kukabiliana na Changamoto



# VIPAUMBELE NA MALENGO KWA MWAKA 24/25

## 03

# 3.1 UTANGULIZI

Sura hii inaelezea malengo na shabaha zitakazofikiwa katika utekelezaji wa miradi na programu kwa mwaka 2024/25. Utekelezaji wa miradi na programu hizo unatarajiwa kuleta matokeo makubwa ya kiuchumi na kijamii ikiwemo kuongeza fursa za ajira, upatikanaji wa fedha za kigeni na kuongeza mauzo nje. Ujumuishaji wa miradi na programu hizo umezingatia hatua za ukamilishaji hususan kwenye sekta wezeshi na upatikanaji wa rasilimali fedha. Aidha, miradi na programu imejumuisha miradi ya kielelezo na ile ya kimkakati ambayo imeainishwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano (2021/22 – 2025/26). Vile vile, Serikali imeweka kipaumbele katika miradi na programu za kuchochea uchumi jumuishi utakaopunguza umaskini na kuleta maendeleo vijijini. Msukumo utawekwa katika kutekeleza programu na miradi ambayo itachochea kufikiwa kwa viashiria ya mafanikio vilivyowekwa katika Mpango wa Tatu wa Maendeleo ya Taifa 2020/21 – 2025/26. Muhtasari wa idadi ya programu na miradi kisekta umeoneshwa katika Jedwali Na 3.1.

**Jedwali Na 3.1 Muhtasari wa Idadi ya Programu na Miradi Itakayotekelezwa kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Sekta | Idadi ya Programu/Miradi |
|---|---|---|
| 1 | Miundombinu ya Usafiri na Usafirishaji | 49 |
| 1.1 | Reli | 2 |
| 1.2 | Bandari | 6 |
| 1.3 | Barabara na madaraja | 41 |
| 1.4 | Usafiri wa anga na viwanja vya ndege | 9 |
| 2 | Nishati | 8 |
| 3 | TEHAMA | 9 |
| 4 | Uzalishaji Viwandani | 8 |

| Na. | Sekta | Idadi ya Programu/Miradi |
|---|---|---|
| 5 | Kilimo | 5 |
| 6 | Mifugo | 1 |
| 7 | Uvuvi | 5 |
| 8 | Madini | 2 |
| 9 | Sanaa, Utamaduni na Michezo | 8 |
| 10 | Utalii | 3 |
| 11 | Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabia Nchi | 7 |
| 12 | Biashara, Uwekezaji na Utekelezaji wa Diplomasia ya Uchumi | 2 |
| 13 | Afya | 12 |
| 14 | Ustawi na Maendeleo ya Jamii | 6 |
| 15 | Elimu | 18 |
| | **Jumla** | **193** |

## 3.2. Mwelekeo wa Utekelezaji wa Miradi na Programu za Maendeleo kwa Mwaka 2024/25

Mpango wa Taifa wa Maendeleo wa Mwaka 2024/25 utalenga kutekeleza miradi na programu za maendeleo kupitia sekta za kiuchumi na kijamii zenye thamani ya shilingi bilioni 15,944.36. Kati ya fedha hizo, shilingi bilioni 12,303.52 ikijumuisha shilingi bilioni 1,189.08 za ruzuku ya maendeleo kwa ajili ya elimu ya elimumsingi bure na Higher Education Students' Loans Board ni fedha za ndani na shilingi bilioni 3,640.84 ni fedha za nje. Jumla ya programu na miradi 193 imepangwa kutekelezwa kupitia sekta 20 katika mwaka 2024/2025. Maelezo ya programu na miradi hii ni kama ifuatavyo:

### 3.2.1. Sekta ya Uchukuzi

Sekta ya uchukuzi ni muhimu katika kuchachua na kukuza uchumi kwa kuunganisha maeneo ya uzalishaji na masoko, kupunguza gharama za kufanya biashara, na kuongeza uzalishaji na ushindani nchini. Sekta hii inajumuisha miundombinu na huduma mbalimbali kama vile usafiri wa nchi kavu (reli na barabara), usafiri wa anga, na usafiri wa majini.

Katika mwaka wa 2024/25, Serikali imepanga kutekeleza shughuli mbalimbali zikiwemo: kuendelea na ujenzi wa reli mpya na ukarabati wa miundombinu ya reli iliyopo; ununuzi na ukarabati wa vitendea kazi ikiwa ni pamoja na vichwa vya treni, injini, mabehewa, na mitambo ya ukaguzi wa reli; kuendelea na ujenzi wa meli mpya na ukarabati wa meli zilizopo katika Maziwa Makuu na bahari; kuimarisha usafiri, usalama na mawasiliano katika Maziwa Makuu; kuboresha miundombinu na huduma katika bandari za bahari na Maziwa Makuu; kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika uendelezaji na uendeshaji wa bandari nchini; kuendelea na ujenzi wa bandari kavu; ununuzi wa ndege mpya; ukarabati na upanuzi wa karakana za matengenezo ya ndege; kuendelea na uimarishaji wa miundombinu katika viwanja vya ndege vilivyopo na kujenga viwanja vipya; na uimarishaji wa usalama wa usafiri wa anga. Kwa kuzingatia umuhimu wa sekta hii, miradi itakayotekelezwa kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na:

### A Reli

i. **Mradi Na. 4281: Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway - SGR):**

Utekelezaji wa mradi huu unazingatia umuhimu wa mchango wake katika uchumi wa nchi na nchi jirani za Burundi, Rwanda, DRC and Uganda. Mradi unahusisha ujenzi wa kilomita 2,561. Aidha, mradi huu utaongeza kasi ya usafirishaji ya treni kutoka kasi ya kilomita 30-56 kwa saa hadi kilomita 160 kwa saa kwa mabehewa ya abiria na kilomita 120 kwa saa kwa mabehewa ya mizigo, kuongezwa kwa ukomo wa mizigo kutoka tani 13 - 20 hadi tani 35 na jumla ya mzigo kutoka tani 214,987 hadi tani milioni 17 kwa mwaka.

Shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kukamilisha ujenzi wa reli ya Standard Gauge kwa kipande cha Dar es Salaam - Morogoro (km 300) na Morogoro - Makutupora (km 422); kuendelea na ujenzi wa njia ya reli kwa kipande cha Mwanza - Isaka (km 341), Makutupora – Tabora (km 368), Tabora - Isaka (Km 165), Tabora- Kigoma(506), Uvinza- Musongati (km 156.6); na kuendelea na ununuzi wa vitendea kazi (vichwa vya treni, mabehewa, mitambo na mashine, na mashine za matengenezo ya njia).

ii. **Uboreshaji wa miundombinu ya reli iliyopo: Mradi Na. 4216: Ukarabati wa Njia Kuu za Reli; na Uboreshaji wa Reli ya TAZARA.**

Utekelezaji wa miradi hii utawezesha kufikiwa kwa malengo ya shabaha kama ilivyoainishwa katika Jedwali 3.1.

**Jedwali 3.1 : Shabaha ya Viashiria vya Reli kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Nafasi ya reli katika mpangilio wa kidunia | 63 | 70 |
| 2. | Urefu wa reli ya kati ya mwendo-kasi (SGR) kwa kilometa | 1,219 | 1,219 |
| 3. | Kiasi cha shehena kinachosafirishwa na reli (tani) | 1,272,682 | 2,162,258 |
| 4. | Idadi ya abiria wanaosafirishwa na reli | 992,258 | 2,272,682 |

## B. Bandari na Usafiri Majini:

Mradi Na. 4295: Ujenzi na Ukarabati wa Meli; Mradi Na. 4201: Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria; Mradi Na. 4125: Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko; Mradi Na. 4139: Ujenzi wa Vivuko Vipya; Mradi Na. 4144: Ukarabati wa Vivuko; Mradi Na. 4227: Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Mbambabay, Kigoma, Bukoba, Ndumbi, Kemondo Bay, Mtwara, Bandari ya Bagamoyo na Bandari Kavu katika Eneo la Ruvu.

Utekelezaji wa miradi hii utawezesha kufikiwa kwa malengo ya shabaha kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 3.2.

**Jedwali Na. 3.2 Shabaha za Viashiria vya Usafiri katika Maziwa Makuu na Bandari kwa Mwaka 2024/25**

| Na | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Muda wa meli kurejea kituoni kwake (siku) | 7.9 | 2 |
| 2. | Idadi ya meli zinazoingia bandarini kwa mwaka | 5,642 | 3050 |
| 3. | Muda wa makasha kukaa bandarini (siku) | 6 | 5 |
| 4. | Muda wa meli kukaa bandarini (siku) | 6 | 2 |
| 5. | Idadi ya bandari kavu | 3 | 3 |
| 6. | Idadi ya meli zinazohudumiwa | 4500 | 4,000 |
| 7. | Mizigo inayotoka nje kuelekea nchi za jirani (tani milioni) | 10,000,000 | 18,000,000 |
| 8. | Mizigo ya kwenda nje toka kwa nchi jirani (tani milioni) | 10,000,000 | 10,000,000 |

## B. Bandari na Usafiri Majini:

Mradi Na. 4295: Ujenzi na Ukarabati wa Meli; Mradi Na. 4201: Uboreshaji wa Usalama wa Usafiri katika Ziwa Victoria; Mradi Na. 4125: Ujenzi wa Maegesho ya Vivuko; Mradi Na. 4139: Ujenzi wa Vivuko Vipya; Mradi Na. 4144: Ukarabati wa Vivuko; Mradi Na. 4227: Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam, Tanga, Mbambabay, Kigoma, Bukoba, Ndumbi, Kemondo Bay, Mtwara, Bandari ya Bagamoyo na Bandari Kavu katika Eneo la Ruvu.

Utekelezaji wa miradi hii utawezesha kufikiwa kwa malengo ya shabaha kama ilivyoainishwa katika Jedwali Na. 3.2.

## C. Usafiri wa Anga

### i. Mradi Na. 4294: Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania (ATCL):

Shirika la Ndege Tanzania – ATCL ni moja ya miradi ya kielelezo lilolowekewa mikakati ya kufufuliwa na kuweza kufikia hadhi ya shirika la ndege la kimataifa. Kutokana na maboresho yaliyofanywa na Serikali shirika limeweza kuaminiwa na wadau wake na hivyo kuzidi kusaidia ukuaji wa sekta mbalimbali za kiuchumi hususan utalii.

Katika kufikia malengo hayo, shughuli zitakazotekelezwa kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na: Kufanya malipo kwa ajili ya ununuzi wa ndege tatu (3) moja (1) ya masafa ya kati, moja (1) ya masafa mafupi na moja (1) ya mizigo yenye uwezo wa kubeba tani 23; ununuzi wa injini moja ya ziada kwa ajili ya ndege aina ya Boeing 737-9 Max; kuwezesha malipo ya gharama za awali za uendeshaji wa ndege moja aina ya Dash 8 Q400; ukarabati wa karakana za JNIA na KIA (KIMAFA); ujenzi wa karakana mpya za ndege za JNIA; ukarabati wa ofisi za ATCL zilizopo Terminal I; ujenzi wa jengo la ofisi za ATCL Dodoma; kukamilisha ukarabati wa nyumba 38 zilizopo KIA; ukarabati wa nyumba za ATCL zilizoko Johannesburg na Lusaka; na ujenzi wa jengo la kuhifadhi mizigo katika uwanja wa JNIA, KIA na Mbeya.

### ii. Mindombinu ya Usafiri wa Anga: Mradi Na. 4209:

Kiwanja cha Ndege cha Mwanza; Mradi Na. 4206: Kiwanja cha Ndege cha Songwe; Mradi Na. 4226: Viwanja vya Ndege vya Mikoa; Mradi Na. 4286: Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato; Mradi Na. 4221: Kiwanja cha Ndege cha Sumbawanga; Mradi Na. 4222: Kiwanja cha Ndege cha Shinyanga; Mradi Na. 4156: Kiwanja cha Ndege cha Kigoma; Mradi Na. 4290: Mradi wa Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa; na Mradi Na. 4159: na Kiwanja cha Ndege cha Tabora.

Utekelezaji wa miradi hii utawezesha kufikiwa kwa malengo ya shabaha kama ilivyoainishwa katika **Jedwali Na. 3.3.**

Jedwali 3.3 : Shabaha za Viashiria vya Usafiri wa Anga kwa Mwaka 2024/25

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya ndege zilizonunuliwa | 17 | 19 |
| 2. | Idadi ya viwanja vya ndege vyenye vifaa | 10 | 10 |
| 3. | Idadi ya ndege za mizigo zilizonunuliwa | 2 | 1 |
| 4. | Idadi ya ndege za abiria za masafa marefu zilizonunuliwa | 4 | 3 |
| 5. | Idadi ya ndege za abiria za masafa ya kati (kanda) zilizonunuliwa | 8 | 8 |
| 6. | Idadi ya ndege za ATCL zinazofanya kazi | 17 | 19 |
| 7. | Idadi ya wanaanga waliofunzwa | 1,359 | 1,359 |
| 8. | Idadi ya Viwanja vya ndege vyenye mifumo ya usimamizi wa taarifa za viwanja vya ndege | 6 | 14 |
| 9. | Idadi ya mitambo ya ulinzi kwenye viwanja vya ndege | 36 | 71 |
| 10. | Viwanja vya ndege vyenye uzio kuzunguka kiwanja | 15 | 27 |
| 11. | Idadi ya rada za hali ya hewa zilizonunuliwa | 5 | 7 |

### 3.2.2. Sekta ya Ujenzi

Sekta ya ujenzi ni muhimu katika kukuza na kuimarisha uchumi kwa kuwezesha shughuli za kiuchumi na kijamii. Sekta hii inajumuisha barabara, madaraja, vivuko, nyumba na majengo ya Serikali. Katika kuendeleza sekta ya ujenzi kwa mwaka wa 2024/25, Serikali itajikita katika kutekeleza vipaumbele vifuatavyo: Kuboresha miundombinu ya mtandao wa barabara na madaraja; ujenzi na ukarabati wa nyumba na majengo ya Serikali; na ujenzi na ukarabati vivuko na miundombinu yake.

i. **Mradi Na. 4015: Daraja la JPM - Kigongo – Busisi (Mwanza):**

Daraja la Kigongo - Busisi (J.P Magufuli) lipo katika Mkoa wa Mwanza likiunganisha Wilaya ya Misungwi na Sengerema kupitia Ziwa Victoria katika Barabara ya Usagara - Sengerema - Geita. Mradi unahusisha ujenzi wa daraja lenye urefu wa mita 3,200 na upana wa mita 28.45 pamoja na barabara unganishi zenye urefu wa km 1.66. Kukamilika kwa daraja hili kutachochea shughuli za kiuchumi na kuboresha huduma za usafiri na usafirishaji kwenda nchi jirani ikiwemo Burundi, DRC, Rwanda na Uganda na kuongeza usalama kwa watumiaji wa daraja hilo katika Ziwa Victoria. Katika mwaka 2024/25, Serikali imepanga kukamilisha utekelezaji wa mradi huu.

ii. **Barabara za Lami Zinazofungua Fursa za Kiuchumi: Mradi Na. 4147:**

Barabara ya Kidatu – Ifakara – Lupilo - Malinyi – Londo – Lumecha/Songea (km 499);Mradi Na.4149: Barabara ya Makutano – Natta – Mugumu/Loliondo – Mto wa Mbu (km 235); Mradi Na. 4190: Barabara ya Itoni – Ludewa - Manda (km 211);Mradi Na. 4193: Barabara ya Handeni – Kiberashi – Kijungu – Kibaya – Njoro – Olboloti – Mrijo Chini – Dalai – Bicha – Chambalo – Chemba – Kwa Mtoro - Singida (km 460); Mradi Na. 4188: Barabara ya Mbeya – Makongolosi – Manyoni - Mkiwa (km 528); Mradi Na. 4112: Barabara ya Kigoma – Kidahwe – Uvinza – Kaliua – Tabora (km 389.7); Mradi Na. 4041: Barabara ya Kitai – Lituhi (km 90) na Daraja la Mnywamaji; Mradi Na. 4024: Barabara ya Nanganga - Ruangwa - Nachingwea (km 145); Mradi Na. 4101: Barabara ya Tanga - Pangani – Makurunge (km 174.5); Mradi Na. 4014: Barabara ya Kibaoni - Majimoto - Muze - Kilyamatundu (km 240) ; na Mradi Na. 4022: Barabara ya Njombe - Makete - Isyonje (km 157.4);

iii. **Barabara Zinazounganisha Tanzania na Nchi Jirani: Mradi Na. 4124:**

Barabara ya Sumbawanga - Matai - Kasanga Port (km 117); Mradi Na. 4115: Barabara ya Marangu - Tarakea - Rongai – Kamwanga/ Sanya Juu (km 271); Mradi Na. 4154: Barabara ya Sumbawanga - Mpanda - Nyakanazi (km 432.56); Mradi Na. 4164: Barabara ya Kidahwe - Kasulu – Kibondo - Nyakanazi (km 341.25); na Mradi Na. 4128: Barabara ya Kyaka – Bugene – Kasulo (km 183.1).

iv. **Barabara za Mikoa na Kupunguza Msongamano: Mradi Na. 4138:**

Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 138.5); Mradi Na. 4145: Kasulu – Manyovu pamoja na barabara za kuingia Kasulu mjini (km 68); Mradi Na. 4285 Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka (Dar es Salaam); na Mradi Na. 4146: Barabara ya Mzunguko katika Jiji la Dodoma.

v. **Barabara za Vijijini na Mijini:**

Mradi Na. 4170: Matengenezo na Ukarabati wa Barabara; Mradi Na. 4169: Mradi wa Uboreshaji wa Barabara maeneo ya Uzalishaji wa Mazao ya Kilimo (Agri-Connect Programme); Mradi Na. 6370: Mradi wa Kuboresha Miundombinu Shindanishi katika Miji Tanzania (Tanzania Cities Transforming Infrastructure and Competitiveness-TACTIC); Mradi Na. 4021: Programu ya Kuongeza Fursa za Kiuchumi na Kijamii Nchini (RISE); Mradi Na. 6209: Mfuko wa Kuchochea Maendeleo ya Jimbo; Mradi Na. 6244: Miradi ya Kimkakati ya Kuongeza Mapato katika Halmashauri; na Mradi Na. 6507: Uboreshaji wa Bonde la Mto Msimbazi.

vi. Madaraja Makubwa: Mbangala, Mbambe; Kirumi, Sukuma, Simiyu, Mtera, Lower Malagarasi, Lower Mpiji, Godegode, na daraja la Mkenda pamoja na barabara unganishi katika daraja la Sibiti.

vii. Ujenzi wa Nyumba za Serikali na Madaraja: Mradi Na. 4126: Ujenzi wa Madaraja Makubwa; na Mradi Na. 6327: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali.

Utekelezaji wa miradi ya barabara na madaraja iliyoainishwa itachangia kufikiwa kwa shabaha ya viashiria vya barabara na madaraja kama ilivyoanishwa katika Jedwali 3.4.

**Jedwali 3.4: Shabaha ya Viashiria vya Barabara kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Miundombinu (Nafasi katika mpangilio, kati ya nchi 189 kimataifa | 50 | 45 |
| 2. | Nafasi ya barabara katika mpangilio wa kimataifa | 45 | 55 |
| 3. | Urefu wa mtandao wa Barabara za Lami (Kilometa) | 13,000 | 13,500 |
| 4. | Uwiano wa barabara za lami katika mfumo wa barabara zote (%) | 10 | 12 |

### 3.2.3. Sekta ya Nishati

Sekta ya nishati ni msingi wa shughuli za kiuchumi na kijamii. Upatikanaji wa nishati ya uhakika husaidia kukuza viwanda, biashara, na huduma za kijamii kama vile elimu na afya. Kwa kuzingatia umuhimu huo, katika mwaka 2024/25 utekelezaji wa sekta hii utaongozwa na vipaumbele mbalimbali ikiwemo: miradi ya uzalishaji, usafirishaji na usambazaji wa umeme; kupeleka nishati vijijini; shughuli za utafiti na uendelezaji wa mafuta na gesi asilia katika vitalu vya kimkakati; usambazaji wa gesi asilia viwandani katika taasisi na majumbani na kuimarisha matumizi ya CNG katika magari. Katika kuhakikisha kuwa mikakati iliyoainishwa inafikiwa kikamilifu, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

i. **Mradi Na. 3172: Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere – MW 2,115**

Utekelezaji wa mradi huu wa kielelezo utahakikisha kuwa nchi inakuwa na umeme wa kutosha kwa kuzingatia mahitaji ya sasa na baadae kulingana na kasi ya ukuaji wa uchumi na maendeleo ya kijamii. Katika mwaka 2024/25

shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na kukamilisha ujenzi wa jengo la mitambo (power house) na ufungaji wa mitambo saba (7) ambayo ipo katika hatua mbalimbali za ukamilishaji.

ii. **Mradi Na. 3155: Kuchakata na Kusindika Gesi Asilia kuwa Kimiminika (Liquefied Natural Gas - LNG) – Lindi**

Mradi huu wa kielelezo una lengo la kuchakata na kusindika gesi asilia iliyogunduliwa katika Vitalu Na.1, 2 na 4 vilivyopo katika kina kirefu baharini ili kuwa kimiminika na kuweza kuuzwa katika soko la dunia. Mradi huu utasaidia kuongeza upatikanaji, uzalishaji na usambazaji wa gesi asilia kwa matumizi ya ndani ya nchi. Katika mwaka 2024/25 shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha majadiliano ya Mikataba ya mradi huu na Wawekezaji, ikiwemo Mkataba wa Nchi Hodhi (HGA) na Mkataba wa Ugawanaji Mapato (APSA); kuelimisha wananchi kuhusu umuhimu na manufaa ya mradi; kushiriki katika shughuli za ufuatiliaji na tathmini za mradi; utafiti; na utoaji elimu ya upatikanaji wa huduma na bidhaa za ndani.

iii. **Mradi Na. 3176: Ujenzi wa Bomba la Mafuta Ghafi kutoka Hoima (Uganda) hadi Tanga (Tanzania) lenye urefu wa km 1,443**

Kukamilika kwa utekelezaji wa Mradi huu wa kielelezo kutachochea uwekezaji na ukuaji wa kiuchumi kwa kuchangia mapato ya Serikali, fursa za ajira pamoja na ukuaji wa sekta zinazohusiana na ujenzi na huduma. Katika mwaka 2024/25 shughuli zitakazotekelezwa ni pamoja na: Kuendelea kupokea shehena za mabomba; kuendelea na ujenzi wa bomba la mafuta; ujenzi wa matenki ya kuhifadhia mafuta na jeti katika eneo la Chongoleani; kuendelea kutoa elimu kwa jamii kuhusu utekelezaji wa mradi na fursa zilizopo kwa maeneo yanayopitiwa na mradi; na kuendelea kuchangia mtaji na kushirikiana na Wanahisa wengine kukamilisha taratibu za upatikanaji wa fedha za mkopo.

iv. **Miradi ya kufua umeme: Mradi Na. 3174: Kufua Umeme wa Maji wa Malagarasi (MW 49.5); Mradi Na. 3173: Kufua Umeme wa Maji wa Kakono (MW 87.8); na Mradi Na. 3102: Kuzalisha Umeme Jua Shinyanga (Kishapu Solar – MW 150).**

v. **Miradi ya Usafirishaji umeme: Mradi Na. 3111:**

Mradi wa uimarishaji wa Gridi ya Taifa (National Grid Stabilization); Mradi Na. 3179: Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 kutoka Chalinze – Dodoma na Chalinze – Kinyerezi - Mkuranga, Chalinze – Segera, Mtwara – Somangafungu na Segera – Tanga (Kv 220); Mradi Na. 3166: Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 400 – North West Grid Extension (Iringa – Mbeya – Sumbawanga – Mpanda – Kigoma – Nyakanazi); na Mradi Na. 3181: Njia ya Kusafirisha Umeme Msongo wa kV 220 Benaco – Kyaka.

Aidha, Serikali itaendelea na utekelezaji wa mradi wa kusambaza umeme vijijini, pamoja na mradi wa kusambaza Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Pwani na Lindi, na kuendeleza miradi ya nishati jadidifu (jotoardhi, upepo na umeme-jua). Utekelezaji wa miradi ya sekta ya nishati iliyoainishwa itachangia kufikiwa kwa shabaha ya viashiria vilivyoanishwa katika Jedwali 3.5.

Jedwali 3.5: Shabaha za Viashiria vya Nishati kwa Mwaka 2024/25

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Uzalishaji wa Umeme (MW) | 4268 | 4,915 |
| 2. | Idadi ya Mikoa Iliyounganishwa na Gridi | 24 | 26 |
| 3. | Urefu wa Gridi ya Taifa (km) | 8,625.4 | 9,351 |
| 4. | Matumizi ya mtu mmoja (KWh) | 96.815 | 220 |
| 5. | Kupungua kwa Upotevu wa Umeme (%) | 8.9 | 7.9 |
| 6. | Asilimia ya Watu waliofikiwa na Umeme | 78.4 | 85 |
| 7. | Idadi ya Vituo CNG | 9 | 35 |

### 3.2.4. Sekta ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari

Miundombinu ya TEHAMA ni muhimu katika kurahisisha na kupunguza gharama za uendeshaji na ufanyaji biashara na kuwezesha utoaji wa huduma za kijamii ikiwemo mawasiliano ya simu, huduma za fedha, shughuli za utawala na huduma za masoko.

Katika mwaka 2024/25 vipaumbele vya Serikali katika kuendeleza sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari ni pamoja na: kuendelea na ujenzi wa Mkongo wa Taifa; kuwezesha kujenga mfumo wa Taifa wa anuani za makazi na postikodi;kuboresha miundombinu kwa ajili ya matumizi ya teknolojia ikiwemo mageuzi ya kidigitali; kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu pamoja na ununuzi wa vitendea kazi vya sekta ndogo ya habari; na kuanzisha vituo vya umahiri vya TEHAMA. Ili kufikia matarajio hayo katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ifuatayo:

i. **Miradi ya Miundombinu ya Mawasiliano: Mradi Na. 4283: Ujenzi wa Mkongo wa Mawasiliano wa Taifa, Mradi Na. 4234: Mfumo wa Anwani za Makazi na Mradi Na. 4280: Tanzania ya Kidijitali.**

ii. **Miradi ya Uhabarishaji na Ubunifu: Mradi Na. 4279:**

Upanuzi wa Usikivu wa Shirika la Utangazaji, Mradi Na. 6567: Habari kwa Umma, Mradi Na. 4292: Ujenzi wa Kituo Kikuu na Vituo vidogo vya Kuendeleza Ubunifu katika TEHAMA (ICT Park), Mradi Na. 6505: Kufunga Mtambo Mpya wa Kisasa wa Uchapaji, Mradi Na. 4937:

Ujenzi wa Kiwanda cha Kupiga Chapa (Government Press Development Programme), na Mradi Na. 6226: Kuendeleza Ubunifu na Utengenezaji wa Vifaa vya TEHAMA.

Utekelezaji wa miradi ya sekta ya mawasiliano na teknolojia ya habari iliyoainishwa itachangia kufikiwa kwa shabaha ya viashiria vilivyoanishwa katika Jedwali Na.3.6.

**Jedwali Na. 3.6 : Shabaha za Viashiria vya Mawasiliano kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | % ya watumiaji wa mtandao wa intanet | 85 | 80 |
| 2. | Eneo la masafa ya mawasiliano (Broadband coverage – Idadi ya watu waliofikiwa na masafa) | 3G – 94<br>4G – 86 | 80 |
| 3. | Eneo la masafa ya mawasiliano (Broadband coverage – Maeneo yaliofikiwa na Masafa) | 3G -75<br>4G - 67 | 80 |
| 4. | % ya taasisi za Serikali zilizoungwa na Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano | 100 | 70 |
| 5. | %Kaya zenye angalau mwanakaya mmoja anayemiliki simu ya mkononi | 84 | 87.8 |
| 6. | Idadi ya watu wanaomiliki simu za mkononi (milioni) | 39 | 28.6 |
| 7. | Idadi ya Kaya zinazotumia mfumo wa anwani za makazi na misimbo ya posta | 13,261,285 | 1,975,000 |
| 8. | % ya idadi ya watu wanaopata mtandao wa simu za mkononi | 98 | 98 |

### 3.2.5. Sekta ya Uzalishaji Viwandani

Sekta ya uzalishaji viwandani ni sekta wezeshi katika kufikia malengo ya uchumi shindani na viwanda kama ilivyoainishwa katika Dira ya Taifa ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Uwepo wa viwanda vikubwa na vya kimkakati vyenye kuzalisha bidhaa zinazohitajika kwenye soko la ndani na nje utasaidia kuongeza thamani kwa bidhaa, kuongeza mauzo nje, kuchochea shughuli za biashara na kuongeza upatikanaji wa ajira.

Katika mwaka 2024/25, kipaumbele cha Serikali ni kuendelea kuboresha mazingira wezeshi kwa ajili ya kuimarisha uwezo wa uzalishaji viwandani na uwekezaji katika maeneo maalumu ya kiuchumi. Hivyo, katika kufikia matokeo tarajiwa Serikali itaendelea kutekeleza hatua mbalimbali zikiwemo: Kuhawilisha teknolojia na kuendeleza uzalishaji wa vipuri vitakavyotumika katika sekta za uchukuzi, nishati, kilimo na viwanda ikiwemo kutengeneza majiko ya nishati safi ya kupikia; kuwezesha na kuimarisha maabara za utafiti katika maeneo ya uzalishaji na kufanya tafiti za uundaji wa magari na vipuri mbalimbali; kuimarisha uzalishaji wa bidhaa za viwandani kwa kutumia malighafi zinazopatikana nchini na vifaa vya kisasa; kuweka mazingira wezeshi ya uwekezaji wa viwanda ambazo bidhaa zake zina mahitaji makubwa nchini ikiwemo viwanda vya madawa, nguo na saruji; kuboresha na kuongeza ustawi na tija ya viwanda nchini; kufanya tafiti na kutoa huduma za kitaalamu viwandani zenye lengo la kuongeza uzalishaji wa bidhaa bora; na kuimarisha vituo vya uendelezaji teknolojia na vituo vya uzalishaji na mafunzo kwa wajasiriamali. Katika mwaka 2024/25 Serikali itatekeleza miradi ifuatayo:

i. **Mradi Na. 1122: Magadi Soda Engaruka**

Mradi wa Magadi Soda Engaruka ni mradi wa kielelezo ambapo utekelezaji wake unatarajiwa kuwa na manufaa makubwa kwa nchi, ikiwemo kuokoa kiasi kikubwa cha matumizi ya fedha za kigeni kinachotumika kuagiza magadi soda kutoka nje, kukidhi mahitaji ya soko la ndani ya nchi na katika ukanda wa Afrika Mashariki na soko la kimataifa, kuongeza mapato ya Serikali na kutoa fursa za ajira. Katika mwaka 2024/25 shughuli zitakazotekelezwa ni: kufanya majadiliano na mwekezaji ili kuingia mkataba wa ubia; na kulipia leseni za uchimbaji.

ii. **Mradi Na. 3171: Makaa ya Mawe Mchuchuma na Mradi Na. 3161: Chuma Liganga**

Miradi ya Makaa ya Mawe Mchuchuma na Chuma Liganga ni kati ya miradi ya kielelezo yenye uwezo wa kuiongezea nchi akiba ya fedha za kigeni kwa kuuza bidhaa za makaa ya mawe nje ya nchi. Aidha, utekelezaji wa miradi hii utasaidia kupunguza uagizaji wa chuma kutoka nje na kupunguza matumizi ya fedha za kigeni wakati wa utekelezaji wa mairadi ya maendeleo. Katika mwaka 2024/25 shughuli zitakazotekelezwa ni: Kukamilisha majadiliano na wawekezaji; na kulipia leseni za uchimbaji

**iii. Kanda Maalumu za Kiuchumi: Mradi Na. 4920: Eneo Maalumu la Uwekezaji Bagamoyo na Benjamini William Mkapa**

Serikali itaendelea kuweka mkazo katika uendelezaji wa viwanda nchini pamoja na kuvutia uwekezaji kutoka nje. Katika mwaka 2024/25 shughuli zitakazotekelezwa ni: Kuendelea na ukamilishaji wa ujenzi wa miundombinu ya barabara yenye urefu wa kilomita tatu (3) kwa kiwango cha lami katika eneo lililo na viwanda; kuendelea na ulipaji wa fidia katika eneo lililothaminiwa; kuanza ujenzi wa miundombinu wezeshi kwa ajili ya kongani ya viwanda; na Kufanya urasimishaji wa makazi yasiyopangwa ya Mlingotini, Zinga na Kiromo kwa kuyapanga ili kuweka miundombinu ya msingi na huduma za jamii. Aidha, kwa upande wa Benjamini SEZ shughuli zitakazotekelezwa ni kutengeneza na kukarabati miundombinu chakavu ya ndani ili kuboresha huduma kwa wawekezaji.

**iv. Miradi ya Kimkakati katika sekta ya uzalishaji viwandani.**

Mradi Na. 6103: Kuboresha kituo cha kuendeleza teknolojia ya magari Tanzania – TATC; Mradi Na. 6260: Kuwezesha Taasisi ambao unajumuisha kiwanda cha mashine na vipuri KMTC, eneo la kongano ya viwanda – TAMCO, mradi wa makaa ya mawe wa Katewaka, CAMARTEC, TEMDO, SIDO, Chuo cha Elimu ya Biashara – CBE, kuendeleza biashara kupitia Wakala wa Vipimo (WMA), Shirika la Utafiti na Maendeleo ya Viwanda Tanzania – TIRDO, na Bodi ya Stakabadhi za Ghala – WRRB; Mradi Na. 4486: uzalishaji viwandani kupitia Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II); na Mradi Na. 4901: MKUMBI – BEGIN.

Utekelezaji wa miradi ya sekta ya viwanda iliyoainishwa itachangia kufikiwa kwa shabaha ya viashiria vilivyoanishwa katika Jedwali Na. 3.7.

**Jedwali Na. 3.7: Matarajio ya Shabaha za Viashiria vya Uzalishaji Viwandani kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa, bei za sasa (%) | 8.5 | 8.5 |
| 2. | Kiwango cha Ukuaji Halisi wa Pato la Taifa (%) | 6.8 | 6.8 |
| 3. | Mchango katika Ajira zote (%) | 12.8 | 12.8 |
| 4. | Mchango katika Mapato ya Mauzo Nje (%) | 19 | 19 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 5. | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya kati katika mauzo nje (%) | 42 | 39 |
| 6. | Mchango wa bidhaa zilizozalishwa viwandani kwa teknolojia ya juu katika mauzo nje (%) | 39 | 10 |
| 7. | Mchango katika Mauzo yote Nje (%) | 24 | 24 |

### 3.2.6. Sekta ya Kilimo

Sekta ya kilimo ni nguzo muhimu ya maendeleo ya vijiji na ustawi wa maisha ya wananchi. Aidha, kilimo kinaendelea kutoa takribani asilimia 66 ya ajira zote nchini na hivyo ni muhimu kuwekewa mkazo katika kuwekeza kwenye sekta hii. Vilevile sekta hii ni muhimu katika kuendeleza sekta nyingine ikiwemo viwanda kwa kuwa huchangia upatikanaji wa malighafi za uzalishaji. Kwa kuzingatia umuhimu huo, katika mwaka 2024/25, vipaumbele vya Serikali ni pamoja na: Kuongeza tija na uzalishaji kwa kufanya utafiti wa mbegu bora; kuongeza ajira zenye staha na ushiriki wa vijana na wanawake kwenye kilimo ikiwemo kuwezesha upatikanaji wa ardhi ya kilimo na uanzishaji wa mashamba makubwa; kutoa ruzuku ya mbolea na viuatilifu; kuimarisha usalama wa chakula na lishe; kuimarisha upatikanaji wa masoko, mitaji na mauzo ya mazao nje ya nchi; kuimarisha maendeleo ya ushirika; na kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika uendelezaji wa sekta ya kilimo.

Katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ifuatayo: Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili - ASDP II inayojumuisha utekelezaji wa BBT; Mradi 4408: Programu ya Mifumo Himilivu ya Chakula (TFSRP); Mradi 4430: Programu ya kuwezesha upatikanaji wa Pembejeo za Kilimo; Mradi Na. 4499: Kudhibiti Sumukuvu; na Mradi Na. 4427: Kuendeleza Kilimo na Uvuvi – AFDP. Jedwali Na. 3.8 linaonesha shabaha za viashiria vya sekta ya kilimo kwa mwaka 2024/25.

**Jedwali Na. 3.8 : Shabaha za Viashiria vya Sekta ya Kilimo kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1 | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 5.1 | 6.1 |
| 2 | Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa) | 24.5 | 23.4 |
| 3 | Asilimia katika Mapato ya Mauzo Nje | | 19.0 |
| 4 | Asilimia ya Jumla ya Ajira | 61 | 60 |
| 5 | Tija (asilimia) ya ukuaji | 4.5 | 4.7 |
| | **Mazao** | | |
| 6 | Wastani wa Ukuaji (%) | 4.7 | 5.7 |
| 7 | Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa) | 13 | 12.3 |
| 8 | Asilimia katika Mapato yote ya Mauzo Nje | 41.5 | 19 |
| 9 | Hekta za Umwagiliwa | 983,465.46 | 1,200,000 |
| 10 | Idadi ya maafisa ugani | 13,000 | 20,538 |
| 11 | Mbegu zilizoidhinishwa na zilizozalishwa | 80,000 | 140,000 |
| 12 | Asilimia ya upotevu wa mavuno (postharvest loss) | 20 | 17.5 |
| 13 | Akiba ya taifa ya chakula | 1,150,000 | 700,000 |
| 14 | Kiasi cha mazao ya bustani yaliyozalishwa (tani) | 9,000,000 | 14,600,000 |
| 15 | Kiasi cha uzalishaji wa mazao ya biashara ya asili (traditional) (tani). | 1,610,000 | 1,583,200 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 16 | Asilimia ya ardhi ya kilimo inayotumia zana za kisasa (mechanization services) katika mnyororo wa thamani | 60 | 75 |
| 17 | Idadi yaa mashamba makubwa (Block Farms) | 160 | 200 |
| 18 | Idadi ya viwanda vinavyomilikiwa na vyama vya ushirika | 165 | 183 |
| 19 | Idadi ya vyama vya ushirika vinavotumia mfumo wa soko rasmi | 7,522 | 4,039 |
| 20 | Idadi ya wanachama wa vyama vya ushirika (milioni) | 6,000,000 | 14,500,000 |
| 21 | Kiwango cha utoshelevu wa chakula (asilimia) | 127 | 130 |

### 3.2.7. Sekta ya Mifugo

Sekta ya mifugo ni muhimili muhimu katika maendeleo ya uchumi nchini. Katika mwaka 2024/25, kipaumbele cha Serikali ni kuendelea na kuimarisha upatikanaji wa mbegu bora za mifugo ili kuboresha mbari za mifugo; kuimarisha upatikanaji wa malisho, vyakula vya mifugo na maji kwa ajili ya mifugo; kuongeza fursa ya mafunzo ya ufugaji wa vitendo na ajira kwa vijana na wanawake kupitia programu ya BBT; kuimarisha afya ya mifugo; kuboresha huduma za ugani; kuwezesha na kuhamasisha ujenzi wa masoko ya mifugo, machinjio za kisasa na ujenzi wa vituo vya kukusanyia maziwa; kuanzisha na kuendeleza vituo atamizi vya uwekezaji vya vijana; kuimarisha huduma za utafiti na mafunzo ya taaluma za mifugo; na kuwezesha uongezaji thamani na biashara ya mifugo na mazao yake; kuimarisha Kampuni ya Ranchi za Taifa (NARCO); kuongeza idadi na uwezo wa viwanda vya kuchakata mazao ya mifugo (ngozi, maziwa na nyama) kwa kuhamasisha uwekezaji wa sekta binafsi; na kuwezesha utambuzi, usajili na kuhamasisha mauzo ya bidhaa za mifugo nje.

Katika kuhakikisha kuwa vipaumbele vilivyoainishwa vinafikiwa kikamilifu katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea na utekelezaji wa Mradi Na. 4486: Programu ya kuendeleza Sekta ya Kilimo Awamu ya Pili (ASDP II). Jedwali Na. 3.9 linaonesha shabaha za viashiria vya sekta ya mifugo kwa mwaka 2024/25.

**Jedwali Na. 3.9: Shabaha za Viashiria vya Sekta ya mifugo kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1 | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 5.0 | 7.1 |
| 2 | Asilimia katika Pato la Taifa (bei za sasa) | 7.0 | 6.6 |
| 3 | Kiwango cha Vifo vya Mifugo | 10 | 12 |
| 4 | Kiwango cha Magonjwa ya Mifugo | 2.0 | 3 |
| 5 | Kiwango cha Uogeshaji Mifugo | 82 | 85 |
| 6 | Kiwango cha Chanjo ya Mifugo | 60 | 50 |
| 7 | Kiwango cha Uzalishaji Maziwa, Ng'ombe wa Asili (Lita) | 2.86 | 4 |
| 9 | Asilimia ya Ngozi Nzuri | 40 | 50 |
| 10 | Uzalishaji wa Maziwa (Lita, kwa billion) | 4.5 | 4.3 |
| 11 | Uchakataji wa Nyama (Tani) | 388 | 500 |
| 12 | Mauzo ya Nyama Nje (Tani) | 14,628 | 7200 |
| 13 | Mauzo Nje ya Ngozi Safi (Tani) | 45 | 92 |

### 3.2.8. Sekta Ndogo ya Uvuvi

Sekta ya uvuvi ni moja ya sekta muhimu katika maendeleo ya uchumi nchini. Katika mwaka 2024/25, kipaumbele cha Serikali ni kuendelea: Kuimarisha uwezo wa uvuvi katika bahari kuu; kuimarisha taasisi za uvuvi ili kuongeza ushiriki katika uchumi wa buluu (blue economy); Kuwezesha na kuhamasisha uwekezaji katika miundombinu ya uvuvi, vifaa na ufugaji wa kibiashara wa samaki; kuimarisha huduma za ugani wa uvvuvi na ukuzaji viumbe maji; kuwezesha upatikanaji wa mitaji, utaalamu, ujuzi, maarifa na zana za kisasa za uvuvi kwa wavuvi wadogo na wanawake kupitia vikundi vya kijamii; na kuhifadhi na kulinda maeneo tengefu ya bahari na maji baridi. Katika kuhakikisha kuwa mikakati iliyoainishwa inafikiwa kikamilifu katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

### i. Mradi Na. 4702: Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi – Kilwa Masoko

Mradi wa Ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa Masoko ni moja ya miradi ya kielelezo inayolenga kuongeza uwekezaji katika uchumi wa bluu. Uwekezaji huu unatarajiwa kuongeza fursa za ajira kwa wananchi, mapato ya Serikali na kuongeza upatikanaji wa fedha za kigeni kupitia mauzo nje. Shughuli zitakazotekelezwa ni: kukamilisha ujenzi wa bandari ya uvuvi katika eneo la Kilwa Masoko.

### ii. Miradi ya kuendeleza Sekta Ndogo ya Uvuvi

Mradi Na. 4703: Ufufuaji wa Shirika la Uvuvi Tanzania (TAFICO); Mradi Na. 4486: Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo (ASDP II); Mradi Na. 4427: Kuendeleza Kilimo na Uvuvi – AFDP; na Mradi Na. 4429: Programu ya Kuendeleza Kilimo na Uvuvi. Jedwali Na. 3.10 linaonesha shabaha za viashiria vya sekta ya uvuvi kwa mwaka 2024/25.

**Jedwali Na. 3.10: Shabaha za Viashiria vya Sekta ya Uvuvi kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1 | Kiwango cha Wastani wa Ukuaji (%) | 4.5 | 5.7 |
| 2 | Asilimia katika Pato la Taifa (Bei za sasa) | 2 | 3 |
| 3 | Asilimia katika Mapato yatokanayo na Mauzo Nje | 4.5 | 4.5 |
| 4 | Ulaji kwa kila Mtu | 9 | 10.5 |
| 5 | Mchango katika Ulaji wa Protini ya Wanyama Kitaifa | 33 | 35 |
| 6 | Uzalishaji wa samaki (tani) | 550,000 | 600,000 |
| 7 | Idadi ya viwanda vya kusindika samaki | 17 | 17 |
| 8 | Idadi ya vituo vya kilimo majini (Aquaculture Development Centres - ADC) | 9 | 12 |
| 9 | Uzalishaji wa chakula cha samaki (tani) | 2,500 | 2,500 |
| 10 | Idadi ya maafisa ugani wa uvuvi | 850 | 1,850 |

### 3.2.9. Sekta ya Madini

Sekta ya madini ni muhimu katika kukuza uchumi, kutoa ajira, kuchochea uwekezaji, kukuza sekta nyingine na kusaidia maendeleo ya jamii. Katika mwaka 2024/25, kipaumbele cha Serikali ni pamoja na: kuimarisha ukusanyaji wa maduhuli na kuongeza mchango wa Sekta ya Madini kwenye Pato la Taifa; kuhamasisha uwekezaji na uongezaji thamani ya madini; kuimarisha uwekezaji na teknolojia katika sekta ya madini ili kuendeleza madini muhimu na madini mkakati; kuendelea kufanya utafiti na ugani wa jiosayansi ikiwemo utafiti wa kina wa jiofizikia; na kuwaendeleza wachimbaji wadogo na kuwasogezea huduma za ugani. Katika kuhakikisha kuwa vipaumbele viliyoainishwa katika sekta vinafikiwa kikamilifu katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

i. **Miradi ya kuendeleza rasilimali, mafunzo na utafiti wa sekta ya madini**

Mradi Na. 1119: Usimamizi Endelevu wa Rasilimali za Madini na Mradi Na. 1120: Kituo cha Jemolojia Tanzania. Jedwali Na. 3.11 linaonesha shabaha za viashiria vya sekta ya uvuvi kwa mwaka 2024/25

**Jedwali Na. 3.11: Shabaha ya Viashiria vya Sekta ya Madini kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Wastani wa Ukuaji (%) | 11.0 | 11.6 |
| 2. | Mchango kwenye Pato la Taifa (%) | 10.7 | 11.2 |
| 3. | Jumla ya Mapato ya Fedha za Nje (Dola za Marekani milioni) | 3,654.4 | 3,760.4 |
| 4. | % ya mauzo ghafi nje | 7 | 5 |
| 5. | % ya zilizoongezwa thamani | 93 | 95 |
| 6. | % Mchango katika mapato yote ya fedha za nje | 50.2 | 51.7 |

### 3.2.10. Sekta ya Sanaa, Utamaduni na Michezo

Utamaduni, sanaa na michezo ni moja ya sekta ya huduma ambayo inakua kwa kasi nchini na inavutia nguvu kazi ya vijana. Hivyo, uimarishaji wa sekta hii ni muhimu kwa kuwa itasaidia kutoa fursa za ajira, kuvutia watalii na kuchangia katika pato la taifa.

Katika mwaka 2024/25, kipaumbele cha Serikali ni: Kuendelea na ujenzi na ukarabati wa miundombinu ya msingi ya michezo na kazi za sanaa na ubunifu; Kutambua, kukusanya, kuendeleza, kulinda na kuhifadhi kumbukumbu na taarifa za Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika unaoshikika na usioshikika ndani na nje ya nchi; Kuratibu utoaji wa mikopo na mafunzo kwa wadau wa sekta ya utamaduni na Sanaa; na kuimarisha, kukuza na kubidhaisha Kiswahili Kitaifa, Kikanda na Kimataifa.

Katika kuhakikisha kuwa vipaumbele vilivyoainishwa vinafikiwa kikamilifu, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine katika mwaka 2024/25 itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

**i. Miradi ya Utamaduni:**

Mradi Na. 6521 - Kuimarisha Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA) na Kukiuza Kiswahili Kikanda na Kimataifa na Mradi Na. 6293: Programu ya Urithi wa Ukombozi wa Bara la Afrika.

**ii. Miradi ya Sanaa: Mradi Na. 4353:**

Ukarabati wa Chuo cha Sanaa Bagamoyo (TaSUBa), na Mradi Na. 6502: Mfuko wa Utamaduni na Sanaa Tanzania.

**iii. Miradi ya Michezo: Mradi Na. 6523**

Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dar es Salaam, Mradi Na. 6504 - Ujenzi wa Vituo vya Mazoezi na Kupumzikia Wananchi (Dar es Salaam na Dodoma); Mradi Na. 6503 - Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Dodoma; na Mradi Na. 6586 – Ujenzi wa Eneo Changamani la Michezo Arusha.

Jedwali Na. 3.12, linaonesha shabaha za viashiria vya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa mwaka 2024/25

**Jedwali Na. 3.12: Shabaha za Viashiria vya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1 | Idadi ya miundombinu ya michezo na iliyoboreshwa nchini kote | 20 | 72 |
| 2 | Majengo mawili changamani ya Sanaa na Michezo Makao Makuu ya Nchi, Dodoma na Dar es Salaam. | 2 | 2 |
| 3 | Idadi ya miundombinu iliyojengwa/ kukarabatiwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya na Taasisi ya Sanaa na Utamaduni Bagamaoyo (TaSUBa). | 6 | 40 |
| 4 | Idadi ya filamu na muziki zilizoidhinishwa, kusambazwa na kutumika | 1,000 | 19,301 |
| 5 | Idadi ya wasanii waliosajiliwa katika tasnia ya ubunifu | 1,500 | 8,666 |
| 6 | Eneo Changamani la Sanaa, Kiromo, Bagamoyo | 1 | 1 |
| 7 | Idadi ya wataalamu katika tasnia ya ubunifu waliopata mafunzo | 150 | 4297 |
| 8 | Idadi ya michezo na mashindano ya kimataifa yaliyoandaliwa na Tanzania kushiriki | 110 | 350 |
| 9 | Idadi ya vibali vilivyotolewa kwa vyama vya michezo na wanamichezo binafsi | 90 | 400 |
| 10 | Jumba Changamani la Filamu. | 1 | 1 |
| 11 | Idadi ya wanariadha wanaocheza nje ya nchi | 30 | 150 |
| 12 | Idadi ya wageni wanaoendesha shughuli za kuzalisha filamu nchini Tanzania. | 1,200 | 1059 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 13 | Idadi ya wasanii/wataalamu katika tasnia ya ubunifu/makundi yanayofanya maonesho yao nje ya nchi | 200 | 1755 |
| 14 | Idadi ya wasanii wa nje/wataalamu katika tasnia ya ubunifu wanaofanya maonesho yao nchini Tanzania | 100 | 2,312 |
| 15 | Idadi ya wataalamu wa Kiswahili wanaofanya kazi nje ya Tanzania | 150 | 656 |
| 16 | Idadi ya machapisho ya Kiswahili yaliyouzwa nje ya nchi | 250 | 700 |
| 17 | Idadi ya tuzo za kimataifa zilizoandaliwa na kutolewa kwenye utamaduni, sanaa na tasnia ya ubunifu | 5 | 130 |
| 18 | Idadi ya vikundi vya utamaduni na sanaa kutoka nje ya nchi vilivyoshiriki katika matamasha ya Kimataifa yanayoandaliwa kila mwaka na TaSUBa. | 10 | 20 |
| 19 | Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Chuo cha Kuendeleza Michezo Malya | 250 | 1300 |

### 3.2.11. Sekta ya Utalii

Sekta ya Utalii imeendelea kukua na kupewa msukumo ili iweze kuchangia zaidi katika uchumi ambapo kwa mwaka 2024/25 vipaumbele vya sekta vitakuwa: kuendeleza mazao ya utalii ya kimkakati ikiwemo fukwe; Kuimarisha na kuboresha miundombinu ya kitalii katika maeneo ya malikale na makumbusho; Kuelimisha na kuhamasisha jamii kuhusu uhifadhi na usimamizi endelevu wa rasilimali za wanyamapori, Misitu na Ufugaji nyuki; na kuendeleza kanda ya utalii ya kusini mwa Tanzania ikiwa ni mbadala wa kanda nyingine. Katika kuhakikisha kuwa mikakati iliyoainishwa inafikiwa kikamilifu, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

**i. Miradi ya Uendelezaji wa Utalii:**

Mradi Na. 5203: Usimamizi wa maliasili na kuendeleza utalii kanda ya kusini (Resilient Natural Resources Management for Tourism and Growth Project - REGROW); na Mradi Na. 4812: Kukabiliana na ujangili na biashara haramu ya wanyamapori.

**ii. Miradi ya Kuongeza Bidhaa za Utalii: Mradi Na. 4651:**

Kuwezesha Mnyororo wa Thamani wa Mazao ya Nyuki – BEVAC. Utekelezaji wa mradi huu utasaidia kupunguza kiwango cha uharibifu wa misitu na shughuli za ujasiriamali hususan kwa vijana. Aidha, mradi huu utasaidia kuongeza uwekezaji katika miundombinu ya utalii hususan katika ujenzi wa migahawa na mahoteli yanayozingatia masuala asilia pamoja na kusaidia shughuli za kujifunza kwa watafiti wa ndani na nje ya nchi.

Jedwali Na 3.13, linaonesha shabaha za viashiria vya sekta ya utalii kwa mwaka 2024/25.

**Jedwali Na. 3.13: shabaha za viashiria vya sekta ya Utalii kwa mwaka 2024/25.**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (bei za sasa) (%) | 17.2 | 17.9 |
| 2. | Kiwango cha ukuaji halisi (%) | 8.7 | 9.1 |
| 3. | Idadi ya Watalii | 2,062,431 | 5,000,000 |
| 4. | Wastani wa idadi ya siku za kulala mtalii. | 10 | 14 |
| 5. | Wastani wa Matumizi ya Mtalii kwa Siku (USD) | 260 | 276 |
| 6. | Kifurushi (package)(USD) | 450 | 467 |
| 7. | Kisicho cha kifurushi(non-package) (USD) | 185 | 326 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 8. | Mchango katika Mapato ya Fedha za Kigeni (%) | 26 | 27 |
| 9. | Mapato yatokanayo na Watalii (Dola za Marekani bilioni) | 4.1 | 6.0 |

### 3.2.12. Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi

Uhifadhi na utunzaji wa mazingira ni suala mtambuka linalopashwa kutiliwa mkazo katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Katika mwaka 2024/25, vipaumbele katika uhifadhi na utunzaji wa mazingira vitakuwa ni pamoja na: kuendelea kuboresha miundombinu ya uhifadhi na usimamizi wa mazingira; kuratibu utekelezaji wa Sera, mipango na sheria za usimamizi wa mazingira; kuendelea kushirikiana na sekta binafsi katika uhifadhi na usimamizi wa mazingira; kuratibu utekelezaji wa shughuli za uchumi wa buluu Nchini; kuendelea kuhamasisha matumizi ya nishati jadidifu; kuimarisha na kuhamasisha matumizi endelevu ya maliasili asilia kwa maendeleo ya kiuchumi na kijamii; kupunguza uchafuzi wa mazingira pamoja na athari zake; na kuongeza mchango wa sekta ndogo ya ufugaji nyuki kwenye uchumi. Katika kuhakikisha kuwa mikakati iliyoainishwa inafikiwa kikamilifu, miradi ifuatayo itatekelezwa:

i. **Miradi ya uhifadhi wa mazingira: Programu Na. 6571:**

Utekelezaji wa Sheria na Usimamizi wa Hifadhi ya Mazingira ya Mwaka 2004 inayojumuisha miradi ya Usimamizi Endelevu wa Matumizi ya Ardhi ya Bonde la Nyasa, na Mradi wa Ujenzi wa miundombinu ya kuzuia maji ya bahari kujaa na kuathiri maeneo ya makazi na kilimo katika fukwe za Swipwese- Pemba na Mikindani- Mtwara. Mradi Na. 4651: Kuwezesha mnyororo wa thamani wa mazao ya Nyuki – BEVAC.

ii. **Miradi ya kukabiliana na mabadiliko ya Tabianchi:**

Programu Na. 5301: Kuhimili Athari za Mabadiliko ya Tabianchi; Mradi Na. 5304: Kudhibiti Kemikali Zinazomong'onyoa Tabaka la Ozoni; na Mradi Na. 5305: Kutekeleza Mpango wa Kitaifa wa Utekelezaji wa Mkataba wa Stockholm Unaohusu Kemikali Zinazodumu katika Mazingira kwa Muda Mrefu.

iii. **Miradi ya usimamizi wa Maafa Nchini: Mradi Na. 6327:**

Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali - Ujenzi wa Kituo cha Usimamizi wa Maafa Nchini, na Mradi Na. 6575: Kuimarisha Uwezo wa Kujiandaa na Kukabili Maafa.

Jedwali Na 3.14, linaonesha shabaha za viashiria vya Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa mwaka 2024/25.

**Jedwali Na 3.14: Shabaha za Viashiria vya Hifadhi ya Mazingira na Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi kwa mwaka 2024/25.**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Wastani wa Ukuaji (%) | 6 | 7 |
| 2. | Mchango katika Pato la Taifa kutokana na matumizi endelevu ya misitu, maji na rasilimali za bahari | 6 | 7 |
| 3. | Eneo la msitu chini ya jamii (Area under Community Plantations) (Ha)) | 190,000 | 160,000 |
| 4. | Kiwango cha kupungua kwa uharibifu wa misitu (Reduced Deforestation Rate) (Ha.) | 469,420 | 234,710 |
| 5. | Maeneo ya misitu ya kibishara (commercial forest Plantation) yaliyoanzishwa (Ha) | 510,000 | 550,000 |
| 6. | Matumizi ya nishati mbadala ya mkaa (tani) | 500 | 7 |
| 7. | Asilimia ya miradi mikubwa inayokidhi uchambuzi wa athari kwa mazingira (EIA) na kanuni za ukaguzi | 93 | 95 |

### 3.2.13. Biashara, Uwekezaji na Diplomasia ya Uchumi

Katika mwaka 2024/25, Serikali itajielekeza katika kuboresha mazingira ya uwekezaji na kukuza uwekezaji, kukuza uwezeshaji wananchi kiuchumi, kukuza sekta binafsi, kuimarisha huduma za biashara na masoko pamoja na ushirikiano na nchi za nje na uchumi wa kidiplomasia; kuweka mfumo Madhubuti wa kisheria na kitaasisi wa kusimamia mashirika na taasisi za umma ili kuongeza tija katika uwekezaji wa umma ndani na nje ya nchi kwa kukamilisha utungaji wa Sheria ya Uwekezaji wa Umma na Kanuni zake; kuanzisha mfuko wa uwekezaji wa umma utakaokuwa chanzo cha uhakika na endelevu cha mitaji kwa mashirika ya umma hivyo kuwezesha Serikali kutumia fursa za uwekezaji zinazojitokeza kwa wakati; na kufanya Stadi ya Kizio (Baseline Study) kwa ajili ya mapendekezo ya kuandaa Sera ya Uwekezaji wa Umma itakatoa mwongozo wa uwekezaji katika Sekta ya Umma Miradi itakayotekelezwa kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na:

**i. Kuboresha Mazingira ya Uwekezaji, na Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi:**

Miradi ya Baraza la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi – NEEC na Kukuza Sekta Binafsi;

**ii. Huduma za Biashara na Masoko: Mradi Na. 6260:**

Mradi wa Kuwezesha Taasisi zinazojihusisha na masuala ya biashara na masoko ya bidhaa. Jedwali Na. 3.15, linaonesha Shabaha za Viashiria vya Biashara, Uwekezaji na Diplomasia ya Uchumi kwa Mwaka 2024/25

**Jedwali Na 3.15: Shabaha za Viashiria vya Biashara, Uwekezaji na Diplomasia ya Uchumi kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| | **Mauzo Nje** | | |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 10 | 28 |
| 2. | Mchango wa huduma katika Mauzo Nje (%) | 42 | 50 |
| 3. | Mchango katika nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (%) | 21 | 15 |
| 4. | Mchango katika Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (%) | 21 | 30 |
| | **Uagizaji Bidhaa kutoka Nje** | | |
| 1. | Mchango katika Pato la Taifa (%) | 20 | 13 |
| 2. | Mchango wa Uagizaji Bidhaa kutoka nchi za Jumuiya ya Afrika ya Mashariki (%) | 36 | 11 |
| 3. | Mchango wa Uagizaji Bidhaa kutoka Nchi za Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (%) | 4.5 | 10 |

**iii. Ushirikiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia: Mradi Na. 6391:**

Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Vitega Uchumi, Ofisi na Makazi ya Watumishi Balozini; Mradi Na. 6317: Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama ya Afrika ya Haki za Binadamu na Watu; na Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi.

**Jedwali Na. 3.16 : Shabaha za Viashiria vya Mahusiano na Nchi za Nje na Uchumi wa Kidiplomasia kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya mikutano kati ya Tanzania na nchi moja moja, ya kikanda na kimataifa iliyoshiriki | 121 | 250 |
| 2. | Idadi ya watanzania walioshiriki katika ulinzi wa amani nje ya nchi | 1,600 | 3,500 |
| 3. | Idadi ya ofisi mpya za ubalozi zilizofunguliwa | 4 | 10 |
| 4. | Idadi ya ofisi ndogo mpya za ubalozi zilizofunguliwa | 2 | 6 |
| 5. | Idadi ya mikutano ya Tume za Kudumu za Pamoja iliyofanyika | 15 | 30 |
| 6. | Idadi ya Hati za Makubaliano ya Pamoja zilizosainiwa kati ya Tanzania na nchi nyingine | 85 | 150 |
| 7. | Idadi ya Mikutano ya Pamoja na nchi jirani iliyofanyika | 60 | 100 |
| 8. | Idadi ya taasisi zinazofundisha lugha ya Kiswahili Kikanda na Kimataifa | 6 | 10 |
| 9. | Idadi ya watanzania walioshiriki katika maonesho na majukwaa ya kibiashara. | 900 | 1200 |
| 10. | Idadi ya maonesho na majukwaa ya biashara ambayo Tanzania ilishiriki | 60 | 100 |
| 11. | Idadi ya wawekezaji wa nje | 250 | 430 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 12. | Idadi ya watalii wa nje | 2,000,000 | 2,100,000 |
| 13. | Idadi ya ofisi na nyumba za kuishi zilizokarabatiwa | 12 | 20 |
| 14. | Idadi ya viwanja vilivyoendelezwa ambavyo vinamilikiwa na Serikali nje ya nchi katika maeneo muhimu ya kibiashara | 13 | 20 |

### 3.2.14. Sekta ya Afya

Utoaji wa huduma bora za afya utawezesha kuboresha ustawi na ubora wa maisha ya wananchi pamoja na kukuza nguvukazi yenye afya na ufanisi. Katika mwaka 2024/25,vipaumbele vya Serikali ni pamoja na: kuratibu na kusimamia shughulli za utoaji huduma za afya ya msingi, lishe na ustawi wa jamii; kuboresha miundombinu ya kutokea huduma za afya msingi kuanzia ngazi ya zahanati, vituo vya afya na hospitali za halimashauri, kuimarisha ubora wa huduma za afya katika vituo vya umma na kuongeza utolewaji wa huduma za ubingwa na ubigwa bobezi. Katika kufikia malengo yaliyoainishwa, Serikali itaendelea kutekeleza miradi ya sekta ya afya kama ifuatavyo:

i. **Mradi wa uboreshaji wa Hospitali ya Taifa ni: Mradi Na. 5487: Hospitali ya Taifa ya Muhimbili.**

ii. **Miradi ya uboreshaji wa Hospitali Maalumu ni: Mradi Na. 5491:**

Taasisi ya Mifupa Muhimbili (MOI), Mradi Na. 5412: Taasisi ya Saratani Ocean Road, na Mradi Na. 5424: Hospitali ya Taifa ya Magonjwa Ambukizi – Kibong'oto (Kilimanjaro).

iii. **Miradi ya uboreshaji wa Hospitali za Rufaa za Kanda ni pamoja na: Mradi Na. 5428:**

Hospitali ya Benjamin Mkapa; Mradi Na. 5408: Ujenzi wa Hospitali ya Kanda ya Ziwa – Chato; na Mradi Na. 5411: Mradi wa Kuboresha Hospitali za Rufaa za Mikoa.

iv. **Miradi ya Upatikanaji wa Dawa, Vifaa na Vifaa Tiba: Mradi Na. 5444:**

Mradi wa Kuboresha Upatikanaji wa Dawa na Bidhaa za Afya; Mradi Na. 5432: Uimarishaji wa Huduma za Chanjo.

v. **Miradi ya kudhibiti magonjwa (yanayoambukizwa na yasiyoambukizwa): Mradi Na. 5492:**

Mpango wa Taifa wa Kudhibiti UKIMWI (NACP); Mradi Na. 5498: Mpango wa Taifa wa Kudhibiti Kifua Kikuu na Ukoma; na Mradi Na. 5403: Kudhibiti Magonjwa Yasiyo ya Kuambukiza.

vi. **Mradi wa kujenga uwezo wa rasilimali watu: Mradi Na. 2204: Mafunzo na Maendeleo ya Wataalamu.**

**Jedwali Na. 3.17: Shabaha ya Viashiria vya Afya kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya vifo vya watoto wachanga kwa kila vizazi hai 1000 | 15 | 30 |
| 2. | Idadi ya vifo vya watoto wenye umri chini ya miaka mitano kwa kila vizazi hai 1000 | 38 | 40 |
| 3. | Uzazi uliohudumiwa na mfanyakazi wa afya mwenye ujuzi | 85 | 100 |
| 4. | Wastani wa umri wa kuishi (miaka) | 69.42(Wanaume)<br>76.9 (Wanawake) | 68 |
| 5. | Kiwango cha maambukizi ya VVU kitaifa (%) | 4.4 | 3.1 |
| 6. | Matumizi ya Serikali katika huduma za afya (%) | 9 | 12.2 |
| 7. | Idadi ya vifo vya akina mama wajawazito wakati wa kujifungua kwa kila akina mama 100,000 | 100 | 180 |

## 3.2.15. Ustawi na Maendeleo ya Jamii

Ustawi na Maendeleo ya Jamii ni msingi katika kuhakikisha kuwa jamii inakuwa na maendeleo jumuishi na yenye ujuzi katika ngazi zote. Uwekezaji katika sekta hii huzingatia usawa wa jamii ili kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii kwa wote yanayoendana na kasi ya ukuaji wa uchumi. Vipaumbele vya Serikali katika eneo la maendeleo ya jamii kwa mwaka 2024/25 ni pamoja na: Kukuza usawa wa kijinsia na uwezeshaji wanawake kiuchumi (Generation Equality Forum - GEF); kuhamasisha utokomezaji wa ukatili dhidi ya wanawake na watoto; kuwezesha wafanyabiashara ndogondogo (machinga) kiuchumi; na kuboresha mazingira ya kufundisha na kujifunzia katika Taasisi za Ustawi wa Jamii na vyuo vya Maendeleo ya Jamii. Ili kufikia malengo hayo, Serikali itatekeleza miradi ifuatayo:

i. **Miradi ya vyuo vya Maendeleo ya Jamii: Mradi Na. 6330: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Jamii.**

ii. **Miradi ya uwezeshaji wa Wanawake na wajasiriamali: Mradi Na. 6259**:

Ujumuishaji wa Masuala ya Jinsia katika Mipango ya Maendeleo; Mradi Na. 6279: Usawa wa Jinsia na Uwezeshaji wa Wanawake; na Mradi Na. 6280: Mfuko wa Kuwezesha Wafanyabiashara Ndogondogo (Machinga).

iii. **Miradi ya huduma za Ustawi wa Jamii: Mradi Na. 5451:**

Kuwezesha Huduma za Ustawi wa Jamii  na Mradi Na. 5414: Uhai na Maendeleo ya Mtoto

**Jedwali Na. 3.18: Shabaha za Viashiria vya sekta ya ustawi na maendeleo ya jamii kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya vituo vya malezi ya watoto vilivyosajiliwa | 4,800 | 7,500 |
| 2. | Idadi ya wazee wasiojiweza wanaopata huduma za bima ya afya bure | 432,642 | 500,000 |
| 3. | Idadi ya watoto wanaolelewa baada ya mapatano | 50,000 | 50,000 |
| 4. | Ufikiwaji wa Kinga ya Jamii | 25 | 30 |

## 3.2.16. Sekta ya Elimu

Sekta ya elimu ni muhimu katika kuchochea ukuajiwa wa rasilimali watu iliyoelimika na yenye mtizamo chanya katika kuleta maendeleo ya Taifa. Vipaumbele katika sekta hii katika mwaka 2024/25 vitajielekeza katika: uratibu wa elimu msingi na sekondari bila ada; kuboresha miundombinu ya kutolea huduma za elimu na sekondari; na kuimarisha mifumo ya usimamizi wa utoaji elimu na mafunzo katika ngazi zote za elimu nchini. Katika kuhakikisha kuwa vipaumbele vilivyoainishwa vinafikiwa kikamilifu katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

i. **Miradi ya Ugharamiaji wa Elimu: Mradi Na. 4322 na 4393: Elimumsingi na Sekondari Bila Ada.**

ii. **Miradi ya Elimu ya Awali, Msingi, Sekondari na Vyuo vya Kati: Mradi Na. 6327:**

Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali (ujenzi wa maboma na vyumba vya madarasa katika shule za awali, msingi, sekondari na elimu maalum); Mradi Na. 3280: Programu ya Huduma ya Maji, Elimu ya Afya na Usafi wa Mazingira Shuleni – SWASH; Mradi Na. 4312: Programu ya Lipa Kulingana na Matokeo katika Elimu (EP4R); Mradi Na. 4319: Mradi wa Kuboresha Elimu

ya Awali na Msingi (Boost Primary Student Learning); Mradi Na. 4390: Mradi wa Kuboresha Elimu ya Sekondari (SEQUIP); Mradi Na. 6390: Mamlaka ya Elimu Tanzania – TEA; na Mradi Na. 6352: Tume ya Nguvu za Atomiki – TAEC.

iii. **Miradi ya Utafiti: Mradi Na. 6345: Mfuko wa Utafiti na Maendeleo wa COSTECH.**

iv. **Miradi ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Ufundi Stadi (Mafunzo ya Amali): Ujenzi na Ukarabati wa Vyuo vya Ufundi Stadi; na Mradi Na. 6229: Ukarabati wa Vyuo vya Maendeleo ya Wananchi – FDC.**

v. **Miradi ya elimu ya juu: Mradi Na. 6321:**

Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Uhasibu Arusha (IAA); Mradi Na. 4341: Chuo Kikuu cha Mwalimu Julius K Nyerere Cha Kilimo na Teknolojia; Mradi Na. 6206: Upanuzi na Ukarabati wa Chuo cha Mipango ya Maendeleo Vijijini (IRDP); Mradi namba 6327: Ujenzi na ukarabati wa majengo wa Chuo cha Uhasibu Tanzania (TIA); Mradi Na. 4315: Mradi wa kuendeleza Elimu ya Juu kwa Mabadiliko ya Kiuchumi (Higher Education for Economic Transformation Project - HEET); Mradi Na. 4340: Mikopo kwa Wanafunzi wa Elimu ya Juu; na Mradi Na. 6322: Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Usimamizi wa Fedha (IFM). Jedwali Na. 3.19 linaonesha shabaha za viashiria vya sekta ya elimu kwa mwaka 2024/25.

**Jedwali Na. 3.19: Shabaha za Viashiria vya sekta ya Elimu kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya wakufunzi | 1,800 (VETA) | 15,000 |
| 2. | Idadi ya taasisi za TVET mpya zilizosajiriwa zimefikia | 489 | 545 |
| 3. | Idadi ya taarifa za tathmini ya soko la ajira kwa wahitimu wa vyuo vya ufundi na mafunzo | 12 | 15 |
| 4. | Idadi ya Vituo Atamizi vilivyoanzishwa kwa wahitimu wa ufundi na mafunzo | 25 | 30 |
| 5. | idadi ya wahitimu wa ufundi na mafunzo | 208,546 | 207,518 |
| 6. | Idadi ya walio katika mafunzo ya kazi kabla ya ithbati | 102,300 | 150,000 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 7. | Idadi ya walio katika mafunzo mahali pa kazi | 198,876 | 231,000 |
| 8. | Idadi ya watu wenye ujuzi unaotambulika uliopatikana awali | 85,000 | 100,000 |
| 9. | Kiwango cha uandikishaji jumla (% ya wanaostahili) -Awali | 90 | 91 |
| 10. | Idadi ya walimu wenye sifa - Msingi | 283,873 | 284,000 |
| 11. | Idadi ya walimu wenye sifa - Sekondari | 98,919 | 100,000 |
| 12. | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa mwalimu - Msingi | 1:61 | 1:60 |
| 13. | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa kitabu - Msingi | 1:2 | 1:1 |
| 14. | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa kitabu - Sekondari | 1:3 | 1:2 |
| 15. | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa - Msingi | 1:70 | 1:60 |
| 16. | Uwiano wa idadi ya wanafunzi kwa darasa - Sekondari | 1:37 | 1:37 |

### 3.2.17. Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi

Katika mwaka 2024/25 Serikali itajielekeza katika: kuendelea na upangaji, upimaji na umilikishaji wa ardhi nchini; kuimarisha mifumo ya utatuzi wa migogoro ya ardhi; kuimarisha matumizi ya mifumo ya TEHAMA katika utunzaji wa kumbukumbu, utoaji wa huduma na upatikanaji wa taarifa za ardhi; kuendelea na miradi ya kuendeleza makazi ili kukabiliana na upungufu wa nyumba bora nchini; kuratibu na kusimamia maeneo ya ardhi ya uwekezaji; na kuimarisha mipaka ya kimataifa.

Katika kuhakikisha kuwa malengo yaliyoainishwa yanafikiwa kikamilifu Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo: Mradi Na. 2324: Mradi wa Kuimarisha Mipaka ya Kimataifa, Mradi Na 2329: Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Upimaji na Ramani, Mradi Na. 4953: Uboreshaji wa Milki za Ardhi, na Mradi Na. 4951: Upangaji wa Matumizi ya Ardhi. Jedwali 3.20 linaonesha shabaha za viashiria vya sekta ya Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2024/25.

**Jedwali Na. 3.20: Shabaha za viashiria vya Ardhi, Mipango Miji, Nyumba na Maendeleo ya Makazi kwa mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyo rasmi | 2 296,357 | 2,496,357 |
| 2. | Asilimia ya eneo la ardhi yenye makazi yasiiyo rasmi | 45 | 25 |
| 3. | Eneo la ardhi lilitengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma (ekari) | 1,100 | 1,452,415 |
| 4. | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohishwa | 2 | 54 |

## 3.2.18. Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira

Katika kuboresha sekta ya maji na usafi wa mazingira, kwa mwaka 2024/25 Serikali itajielekeza katika vipaumbele vifuatavyo: ujenzi, ukarabati na upanuzi wa miradi ya majisafi na usafi wa mazingira katika maeneo ya vijijini na mijini; kuimarisha programu za uhifadhi na utunzaji wa mazingira na vyanzo vya maji; kuendelea na ujenzi wa mabwaa ya kimkakati ukubwa wa kati na mdogo kwa ajili ya kuongeza uhifadhi wa rasilimali za maji ili kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabia ya nchi. Katika kuhakikisha kuwa mikakati iliyoainishwa inafikiwa kikamilifu, Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

i. **Kuboresha Huduma za Maji Vijijini: Mradi Na. 3280: Huduma za Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini.**
ii. **Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji Mijini na katika Miji Mikuu ya Mikoa: Mradi Na. 3306:**

Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji Mikuu ya Mikoa, Mradi Na. 3307: Ujenzi, Ukarabati na Upanuzi wa Miradi ya Maji katika Miji mikuu ya Wilaya, Miji Midogo na Miradi ya Kitaifa, Mradi Na. 3341: Mradi wa Maji Same – Mwanga – Korogwe, Mradi Na. 3403: Mradi wa Maji wa Ziwa Victoria - Kahama – Shinyanga na Miji Mingine.

iii. **Kuboresha Huduma za Maji Katika Jiji la Dar es Salaam: mradi Na. 3437: Kuboresha Huduma za Maji Katika Jiji la Dar es Salaam; na mradi Na. 3438: Mradi wa Bwawa la Kidunda.**
iv. **Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini: Mradi Na. 3435:**

Ufuatiliaji wa Ubora wa Maji na Usimamizi wa Mfumo wa Ikolojia, Mradi Na. 3437: Kusimamia na Kuendeleza Rasilimali za Maji Nchini.

Jedwali Na. 3.21, linabainisha Viashiria vya Usambazaji wa Maji na Huduma za Usafi wa Mazingira.

**Jedwali Na. 3.21: Viashiria vya Usambazaji wa Maji na Huduma za Usafi wa Mazingira**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya mali zilizorasimishwa katika makazi yasiyo rasmi | 2 296,357 | 2,496,357 |
| 2. | Asilimia ya eneo la ardhi yenye makazi yasiiyo rasmi | 45 | 25 |
| 3. | Eneo la ardhi lilitengwa na kulindwa kwa matumizi ya umma (ekari) | 1,100 | 1,452,415 |
| 4. | Idadi ya miji yenye mipango kabambe ya upimaji iliyohishwa | 2 | 54 |
| 5. | Asilimia ya upotevu wa maji (NRW) katika makao makuu ya mikoa | 30 | 20 |
| 6. | Asilimia ya watu katika makao makuu ya wilaya na miji midogo wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji yaliyolindwa kama chanzo kikuu | 80 | 85 |
| 7. | Asilimia ya watu katika jiji la Dar es Salaam wanaopata huduma ya maji ya bomba au maji salama kama chanzo chao kikuu | 93 | 95 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 8. | Asilimia ya kaya katika jiji la Dar es Salaam waliounganishwa kwenye mfumo rasmi wa maji-taka | 16 | 30 |
| 9. | Kiwango cha upotevu wa maji (NRW) katika jiji la Dar es Salaam | 35 | 20 |
| 10. | Idadi ya vyanzo vya maji vilivyotengwa na kutangazwa kwa ajili ya ulinzi na uhifadhi | 80 | 200 |

### 3.2.19. Utawala Bora na Utawala wa Sheria

Utawala Bora na Utawala wa Sheria ni miongoni mwa nguzo muhimu katika kufikia malengo ya ustawi wa jamii. Katika mwaka 2024/25, Serikali imepanga kuendelea kuboresha mfumo wa Utawala Bora na Utawala wa Sheria kwa kutekeleza hatua mbalimbali za kimkakati zikiwemo: Kuboresha mifumo na miundombinu ya utoaji haki; kuhamasisha matumizi ya TEHAMA katika utoaji na upatikanaji wa haki; kuimarisha mifumo ya utunzaji wa taarifa na kumbukumbu utoaji haki; kuimarisha taratibu na miongozo ya utoaji wa msaada wa kisheria nchini; na kuendelea kudumisha usalama, utulivu na amani; kuratibu uboreshaji wa miundombinu ya huduma katika maeneo ya utawala ya Mikoa, Wilaya na Halmashaur; kuendelea na jitihada za kupunguza kiwango cha umasikini pamoja na kuongeza ajira nchini; na kuimarisha usajili wa matukio muhimu ya kibinadamu nchini. Katika mwaka 2024/25, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

i. **Kuimarisha Shughuli za Mfuko wa Bunge:**

Miradi itakayotekelezwa ni pamoja na: Mradi Na. 6360: Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge, Mradi Na.6318: Ukarabati wa Majengo ya Bunge; Mradi Na. 6360: Ujenzi wa Miundombinu ya Bunge; Mradi Na. 6318: Ukarabati wa Majengo ya Ofisi ya Bunge; Mradi Na. 6251: Programu ya Maboresho ya Usimamizi wa Fedha za Umma (PFMRP).

ii. **Maboresho ya Mahakama:**

Miradi itakayotekelezwa ni: Mradi Na. 6310: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Wilaya; Mradi Na. 6312: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama za Mwanzo; Mradi Na 6314 - Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Mahakama kuu; Mradi Na. 6215: Mradi wa uboreshaji wa huduma za Mahakama.

iii. **Utawala Bora: Mradi Na. 5502:**

Kujenga Mfumo Endelevu wa Mpango Kazi wa Kupambana na Rushwa Tanzania; Mradi Na. 5507: Upatikanaji wa Haki kwa Wanawake na Watoto wa Kike; Mradi

Na. 5508: Program ya Upatikanaji Haki kwa Maendeleo Endelevu; na Mradi Na. 6201: Haki Mtandao; Mradi Na. 6517: Kuimarisha Haki za Mtoto; Mradi Na. 6501: Vitambulisho vya Taifa.

iv. **Majengo ya Serikali: Mradi Na. 6389:**

Ujenzi wa Majengo ya Ofisi unaojumuisha ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Viongozi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa; Ujenzi wa Ofisi na Makazi ya Viongozi katika Tawala za Mikoa; Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Mwanasheria Mkuu; Ujenzi wa Majengo ya Ofisi ya Taifa ya Mashtaka; na Ujenzi wa Mji wa Serikali – Mtumba.

v. **Usalama wa Raia: Mradi Na. 6302:**

Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Tanzania Bara; Mradi Na. 6303: Ujenzi wa Ofisi na Nyumba za Makazi Zanzibar; Mradi Na. 6305: Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Ofisi; Mradi Na. 2330: Upimaji wa Maeneo na Ulipaji Fidia; Mradi Na. 4491: Kuboresha upatikanaji wa Maji safi Magerezani; Mradi Na. 6582: Upanuzi wa Huduma za Zimamoto; na Mradi Na. 6301: Ujenzi wa Ofisi za Mikoa za Uhamiaji.

vi. **Utumishi wa Umma: Mradi Na. 6284:**

Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma Awamu ya Tatu; Mradi Na. 6315: Ujenzi wa Makazi ya Viongozi Wakuu Wastaafu wa Kitaifa; Mradi Na. 6339 Ukarabati wa Nyumba za Serikali.

Jedwali Na. 3.22, linaonesha shabaha za viashiria vya Utawala Bora na Utawala wa Kisheria kwa mwaka 2024/25

**Jedwali Na. 3.22: Shabaha za viashiria vya Utawala Bora na Utawala wa Kisheria kwa mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya majengo ya Mahakama za Wilaya yaliyojengwa | 2 296,357 | 2,496,357 |
| 2. | Idadi ya Majengo ya Mahakama za Mwanzo yaliyojengwa | 45 | 25 |
| 3. | Idadi ya Ofisi za Mwanasheria Mkuu wa Serikali zilizojengwa katika Mikoa | 1,100 | 1,452,415 |
| 4. | Idadi ya Ofisi za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka zilizojengwa katika Mikoa | 2 | 54 |
| 5. | Idadi ya Ofisi za Ofisi ya Taifa ya Mashtaka zilizojengwa katika Wilaya | 30 | 20 |
| 6. | Idadi ya Ofisi za Wakili Mkuu wa Serikali zilizojengwa katika Mikoa | 80 | 85 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 7. | Idadi ya Wilaya zenye Watoa Huduma ya Msaada wa Kisheria | 93 | 95 |
| 8. | Idadi ya Taasisi zinazotoa huduma za utoaji haki kwa kutumia TEHAMA | 7 | 8 |
| 9. | Asilimia ya Watoto wenye umri chini ya miaka mitano waliosajiliwa na kupatiwa cheti cha kuzaliwa | 65 | 100 |
| 10. | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa shauri na kutolewa hukumu | 280 | 350 |
| 11. | Asilimia ya watu walioridhishwa na huduma za mahakama. | 80 | 80 |
| 12. | Wastani wa idadi ya siku tangu kufunguliwa kwa shauri na kutolewa hukumu katika Mahakama ya Biashara | 310 | 350 |
| 13. | Asilimia ya mlundikano wa mashauri kwa jumla ya mashauri yote yanayosubiri maamuzi | 6 | 2 |
| 14. | Idadi ya Sheria zilizofanyiwa mapitio | 5,000 | 1,410 |
| 15. | Idadi ya Sheria zilizotafsiriwa kutoka lugha ya Kiingereza kuwa lugha ya Kiswahili. | 188 | 250 |
| 16. | Wastani wa Muda wa kujibu Malalamiko juu ya ukiukwaji wa haki za binadamu kitaifa na kimataifa | Mwaka mmoja (1) | Miezi 6 |
| 17. | Wastani wa muda katika kuidhinisha mikataba ya uwekezaji (siku) | 7 | 14 |
| 18. | Asilimia ya maamuzi ya Mahakama Kuu na Mahakama ya Rufaa yaliyowekwa kwenye mtandao wa TEHAMA | 80 | 25 |

### 3.2.20 Ujuzi na Uwezeshaji

Ujuzi wa rasilimali watu ni nyenzo muhimu katika kuleta maendeleo ya nchi. Katika mwaka 2024/25 Serikali itajikita katika kuwezesha ujuzi wa rasilimali watu kwa kuendelea na: Programu ya kukuza ujuzi na kuchochea ukuzaji wa fursa za ajira kwa vijana na watu wenye ulemavu; kuimarisha mafunzo ya utarajai (internship training) na mafunzo ya uanagenzi (apprenticeship) ili kuwajengea uwezo wa kushindana katika soko la ajira kwa kushirikiana na sekta binafsi; kukuza kazi za staha nchini; kutoa mikopo kwa vijana; na kuimarisha vituo vya ufundi stadi vya Watu Wenye Ulemevu. Katika kuhakikisha kuwa mikakati hiyo inatekelezwa kwa mwaka 2024/25, Serikali itaendelea na utekelezaji wa miradi ifuatayo:

i. **Kukuza rasilimali yenye ujuzi: Mradi Na.6581:**

Programu ya Taifa ya Kukuza Ujuzi nchini; Mradi Na.4952: Mfuko wa Maendeleo ya Vijana; Mradi Na. 6205:Programu ya Taifa ya Kukuza za Staha; na Mradi Na.4954:Ujenzi na Ukarabati wa Vituo vya Ufundi kwa Watu Wenye Ulemavu. Jedwali 3.23 linaonesha shabaha za viashiria vya Kuendeleza Rasilimali Watu kwa Mwaka 2024/25.

Jedwali 3.23 linaonesha shabaha za viashiria vya Kuendeleza Rasilimali Watu kwa Mwaka 2024/25.

**Jedwali Na.3.23 Shabaha za Viashiria vya Kuendeleza Rasilimali Watu kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Idadi ya wastani ya wanafunzi waliodahiliwa katika vyuo vya ufundi | 678,900 | 700,000 |
| 2. | (%) ya wanawake/wasichana | 45 | 50 |
| 3. | (%) ya wenye ulemavu | 0.087 | 0.1 |
| 4. | Udahili wa jumla katika elimu ya ufundi (%) | 4 | 6.9 |
| 5. | Idadi ya wanafunzi wanaohitimu elimu ya ufundi | 678,900 | 680,000 |
| 6. | % ya wanafunzi wa sayansi na uhandisi | 20 | 40 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 7. | % ya wanawake/wasichana | 40 | 50 |
| 8. | % ya wanafunzi wa elimu ya ufundi wanaopata mikopo ya wanafunzi | 15 | 35 |
| 9. | Idadi ya wakufunzi | 12,789 | 15,000 |
| 10. | % ya wakufunzi wa kike | 50 | 50 |
| 11. | Idadi ya taarifa za utafiti katika soko la ajira zilizotolewa | 20 | 25 |
| 12. | Idadi ta taarifa za tafiti za ufuatiliaji wahitimu wa Mpango wa TVET (Training and Vocational Education and Training) | 4 | 4 |
| 13. | Idadi ya Vituo Atamizi vilivyoanzishwa | 15 | 30 |
| 14. | % ya shughuli za TVET zinazojiendesha zenyewe | 30 | 60 |
| 15. | Idadi ya taasisi za TVET zinazofuatiliwa kuhakiki ubora | 450 | 800 |
| 16. | Idadi ya taasisi za TVET mpya zilizosajiriwa | 489 | 545 |
| 17. | Uwiiano wa wahandisi-mafundi-wasaidizi | | 1:5:25 |
| 18. | Idadi ya wahitimu | 99,000 | 99,529 |
| 19. | Wahitimu wa kiume | 49,500 | 49,892 |
| 20. | Wahitimu wa kike | 49,500 | 49,637 |
| 21. | Idadi ya wastani ya udahili katika Vyuo vya Ufundi na Mafunzo | 470,000 | 1,000,000 |
| 22. | % ya wanawake/wasichana | 45 | 45 |

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 23. | % ya wenye ulemavu | 0.04 | 0.05 |
| 24. | Idadi ya wakufunzi | 11,345 | 12,321 |
| 25. | % ya wakufunzi wa kike | 45 | 47 |
| 26. | Idadi ya taarifa za tathmini ya soko la ajira zilizotolewa | 10 | 15 |
| 27. | Idadi ya Vituo Atamizi vilivyoanzishwa | 25 | 30 |
| 28. | Idadi ya wahitimu | 208,546 | 207,518 |
| 29. | Kati yao, wanaume | 114,700 | 128,195 |
| 30. | Kati yao, wanawake | 93,846 | 79,323 |
| 31. | Watu wenye ujuzi uliopatikana kutoka mfumo usio rasmi, kwa sekta sita za kipaumbele (kwa mwaka) | 85,000 | 100,000 |
| 32. | Mafunzo kazini kabla ya ithbati kwa wahitimu wa vyuo vikuu (kwa mwaka) | 3,987 | 5,000 |
| 33. | Wafanyakazi wenye viwango vya juu vya ujuzi (%) | 9 | 12.1 |
| 34. | Wafanyakazi wenye viwango vya kati vya ujuzi (%) | 50 | 54.0 |
| 35. | Idadi ya walio katika mafunzo ya kazi kabla ya ithbati | 112,000 | 150,000 |
| 36. | Idadi ya walio katika mafunzo mahali pa kazi | 240,00 | 231,000 |
| 37. | Idadi ya watu wenye teknolojia ya kisasa ya kilimo | 178,900 | 200,000 |
| 38. | Idadi ya watu wenye ujuzi unaotambulika uliopatikana awali | 87,876 | 100,000 |

### 3.2.21 Sekta ya Fedha

Huduma za kifedha ni muhimu katika ukusanyaji wa akiba na uhawilishaji wa mitaji katika sekta mbalimbali za uchumi. Sekta hii inachochea tija, ushindani na utangamano wa shughuli za uzalishaji, uchakataji, na biashara kwa usalama na ufanisi.

Katika mwaka 2024/25, vipaumbele vya Serikali ni: kuhamasisha na kuendesha programu za elimu ya huduma jumuishi za kibenki na malipo kwa umma; kupunguza gharama za matumizi ya huduma rasmi za benki na malipo; kuimarisha usimamizi wa kanuni za kitaalamu na viwango vya kimataifa; kuanzisha mfumo madhubuti wa kushughulikia madai, malipo na malalamiko ya wateja; kuhamasisha na kuendesha programu jumuishi za elimu ya bima kwa umma; kuanzisha na kuhamasisha bidhaa za bima zinazohitajika katika soko; na kuhamasisha na kutekeleza programu za kujenga uelewa na uanzishaji wa masoko ya mitaji.

Katika kuhakikisha kuwa vipaumbele vilivyoainishwa vitafikiwa kikamilifu Serikali kwa kushirikiana na wadau wengine kwa mwaka 2024/25 itaendelea na: uendelezaji wa shughuli zinazotekelezwa na Benki ya Maendeleo TIB na TADB; kuimarisha huduma jumuishi, huduma ndogo za fedha na Soko la Bidhaa Tanzania – TMX; na kuboresha huduma za bima. Jedwali 3.24 linaonesha shabaha za viashiria vya Huduma za Benki na Malipo pamoja na Sekta Ndogo ya Bima kwa mwaka 2024/25.

**Jedwali Na.3.24: Shabaha za Viashiria vya Sekta ya Fedha kwa Mwaka 2024/25**

| Na. | Kiashiria | Shabaha | |
|---|---|---|---|
| | | 2024/25 | 2025/26 |
| 1. | Watu wazima wanaotumia huduma za benki (%) | 23 | 33 |
| 2. | Uwiano wa amana za benki kwa Pato la Taifa (%) | 15 | 21 |
| 3. | Uwiano wa mali za benki kwa Pato la Taifa (%) | 30 | 33 |
| 4. | Mchango wa bima katika Pato la Taifa (%) | | 2 |
| 5. | % ya watu waliowekeza katika Soko la Mitaji | 2.66 | 3 |
| 6. | Idadi ya kampuni zilizo orodheshwa katika Soko la Mitaji | 28 | 35 |
| 7. | Uwiano wa mtaji wa Soko la Mitaji kwa Pato la Taifa (%) | 8.04 | 10 |
| | | | |

### 3.2.22 Ubia kati ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi

Ushiriki wa Sekta binafsi katika utekelezaji wa Mpango utachangia kufikiwa kwa malengo yaliainishwa katika Mpango wa tatu Maendeleo ya Taifa wa miaka mitano. Ushiriki huu nikupitia ubiya kati ya Serikali na sekta binafsi na uwekezaji wa moja kwa moja wa sekta binafsi katika miradi ya maendeleo. Katika kujenga Uchumi Shindani wa Viwanda kwa Maendeleo ya Watu, Serikali inaendelea kutekeleza Miradi kwa ubia kati ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP) kwa lengo la kujenga miundombinu, kuimarisha huduma za Jamii ili kukuza Uchumi, kukuza Sekta Binafsi ambayo ndiyo injini ya ukuaji wa uchumi na kunaongeza wigo wa bajeti katika kutekeleza miradi ya maendeleo.

Katika mwaka 2024/25 kipaumbele katika ubia wa sekta ya umma na sekta binafsi vitajikita katika shughuli zifuatazo: kukamilisha ununuzi wa mbia wa mradi wa ujenzi wa barabara ya tozo kutoka Kibaha - Chalinze (km 78.9); kuendelea na upembuzi yakinifu wa kipande cha Chalinze – Morogoro (km 126.1); kukamilisha mandalizi ya nyaraka za zabuni na kuanza ununuzi wa Mbia wa mradi wa ukaguzi wa lazima wa Vyombo vya Moto; kuandaa taarifa ya upembuzi yakinifu wa mradi wa ujenzi wa Kituo cha Mazoezi Tiba Mbweni Dar es Salaam; na kushirikisha washauri elekezi katika kuandaa upembuzi yakinifu nyaraka za zabuni na rasimu ya mikataba ya PPP kwa miradi ya Mabasi yaendayo haraka Jijini Dar es Salaam Awamu ya Pili na ya Tatu, mradi wa Hosteli za wanafunzi wa Chuo cha Elimu ya Biashara katika Kampasi Dar es Salaam na mradi wa Kuimarisha Huduma za Saratani nchini kwa kujenga Kituo cha Ubingwa Bobezi wa Tiba ya Saratani eneo la Mloganzila, na Kituo cha Saratani eneo la Iwambi Mbeya.

### 3.2.23 Uboreshaji wa Mazingira ya Biashara na Uhamasishaji Uwekezaji Nchini

Katika mwaka 2024/25 vipaumbele katika kuboresha mazingira ya biashara na uhamasishaji uwekezaji nchini ni pamoja na:

i. **Kurejea mpango wa Kuboresha Mazingira ya Biashara na Uwekezaji (MKUMBI) ili kuendana na mazingira ya sasa ya mahitaji hali ya uwekezaji na Biashara na maendeleo ya sekta binafsi kwa ujumla**
ii. **Kuandaa na kutekeleza programu ya kujenga uwezo wa Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa katika kusimamia utekelezaji wa Sera na Miongozo ya Uwekezaji Binafsi na uboreshaji mazingira ya biashara ya ujumla;**
iii. **Kufanya mapitio ya Sheria zinazohusu masuala ya madini, ardhi, kilimo, utalii na biashara kwa ajili ya kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini;**

iv. **Kuanza hatua za awali za kuendeleza Maeneo ya SEZ: Kufanya upembuzi yakinifu (Feasibility Study), kuandaa mpango kabambe wa uendelezaji (Master Plan), Survey na kufanya usanifu wa miundombinu ya ndani (Design of onsite Infrastructure) Nala; Kuweka mipaka pamoja na mabango katika Maeneo Maalum ya Kiuchumi (SEZ); na Kuandaa mchoro wa mpango mji na upimaji wa viwanja vya uwekezaji katika eneo la Nala;**

v. **Kukamilisha ujenzi wa kanzidata ya uwekezaji; na Kuandaa Mikakati ya kuhimiza na kuwezesha uwekezaji nchini; na**

vi. **Kufanya mapitio na kuhakiki vipande 326 vya ardhi katika Kanzidata ya Kituo vyenye makadirio ya Hekta 69,408.944 yaliyowasilishwa kutoka Wizara, Idara na Wakala, Serikali za Mitaa na Watu binafsi katika Mikoa (05).**

# UFUATILIAJI, TATHMINI NA VIHATARISHI.

# 04

# 4.1 UTANGULIZI

Sura hii inaainisha mfumo wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa mwaka 2024/2025 na mikakati itakayochukuliwa kuhakikisha malengo yanafikiwa kama yalivyopangwa. Sura hii pia inabainisha vihatarishi vya utekelezaji wa Mpango pamoja na hatua za kukabiliana navyo ili kupunguza athari zinazoweza kujitokeza.

## 4.2 Ufuatiliaji na Tathmini

Ufuatiliaji na Tathmini (U&T) wa Mpango wa Maendeleo ya Taifa wa mwaka 2024/25 utazingatia Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo wa Mwaka 2022; Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26; Mwongozo wa Maandalizi ya Mpango na Bajeti ya Serikali kwa Mwaka 2024/25; Mwongozo wa Usimamizi wa Uwekezaji wa Umma Toleo la Mwaka 2022; Sheria ya Bajeti, Sura 439; Mpango Kazi na Mtiririko wa Mahitaji ya Fedha; Waraka Na. 5 wa Hazina wa Mwaka 2020/21 kuhusu matumizi ya Mfumo wa Kitaifa wa Kusimamia Miradi ya Maendeleo (NPMIS); na Waraka Na. 1 wa Hazina kuhusu Utekelezaji wa Bajeti 2023. Ufuatiliaji na Tathmini utalenga kutoa fursa ya kujifunza kupitia uzoefu wa utekelezaji wa mpango (development learning) ili kuboresha utoaji maamuzi (better decision-making), kuongeza uwazi (transparency) na uwajibikaji (accountability) kwa wadau wa mpango wa maendeleo.

## 4.3 Ufuatiliaji na Tathmini ya Programu na Miradi ya Maendeleo kwa mwaka 2023/24

Katika mwaka 2023/24 Serikali ilipanga kutekeleza miradi na programu za maendeleo katika maeneo yote matano (5) ya kipaumbele kama ilivyoainishwa katika Sura ya nne (4) ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2023/24. Aidha, hadi kufikia robo ya tatu ya mwaka 2023/24, jumla ya miradi na programu za maendeleo 95 inayotekelezwa katika mikoa ya Dar es Salaam, Pwani, Lindi, Morogoro, Iringa, Dodoma, Manyara, Simiyu, Mara, Mwanza, Tanga, Kilimanjaro na Arusha ilifuatiliwa. Orodha ya miradi na programu hizo imeambatishwa katika Jedwali Na.4.1.

Masuala yaliyobainika katika zoezi la ufuatiliaji na tathmini lililofanyika:

i. Uendeshaji usio na ufanisi wa Mradi wa Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya I kutokana na kukosa Mwendeshaji mkuu hivyo kusababisha UDART kuendesha mradi kama mwendeshaji mkuu tofauti na lengo la awali la kuwa mwendeshaji msaidizi (sub operator). Hivyo, DART ifanye tathmini mfumo wa usimamizi wa mradi uliopo na kuweka mfumo madhubuti wa usimamizi na uendeshaji wa mradi.

ii. Kuendelea kutekelezwa kwa miradi mikubwa bila kufungamanisha na miradi mingine inayofanana. Mfano mradi wa kufua umeme wa JNHPP ambao ulipaswa kufungamanishwa na mradi wa kusafirisha umeme wa North East Grid. Katika kukabiliana na hali hii Tume ya Mipango itahakikisha miradi inayoibuliwa inafungamanishwa na miradi mingine inayoendelea. Ili kuhakikisha miradi inafungamanishwa, Tume ya Mipango imeandaa Mwongozo wenye vigezo mahsusi ili kuhakikisha miradi inayoibuliwa inafungamanishwa na miradi mingine na hivyo kutekelezwa kama program. Hii itapunguza miradi kurudufiwa (duplication) na kupunguza gharama za utekelezaji.

iii. Ongezeko la gharama za mradi kutokana na mabadiliko ya viwango vya kubadilisha fedha kigeni pamoja na bei za vifaa. Katika kukabiliana na hali hii, mkazo utawekwa kwenye uchambuzi wa mikataba ili kuepuka kuingiza vifungu vya kimkataba ambayo vina athari hasi kwa Taifa.

iv. Uwepo wa mkinzano wa sheria ya msamaha wa kodi inayosimamiwa na Wizara ya Fedha pamoja na sheria ya fedha ya Mamlaka za Serikali za Mitaa inayoruhusu kutoza ushuru wa huduma (service levy) kwa wakandarasi waliopewa msamaha wa kodi ya ongezeko la thamani (VAT) wanaotekeleza miradi katika Halmashauri husika. Hali hiyo imesababisha migogoro ya kikodi kati ya taasisi za umma katika baadhi ya maeneo na kusababisha kuchelewa kwa utekelezaji wa miradI. Ili kuepesha matokeo hasi ya suala hili, Serikali itafanya mapitio ya Sheria husika ili kuepusha mkinzano wa kisheria unaoendelea.

v. Baadhi ya miradi kutekelezwa pasipo kufanyiwa uchambuzi wa kina. Katika kukabiliana na hali hii, Wizara na Taasisi zote za Serikali zinaelekezwa kuwasilisha Tume ya Mipango maandiko yote kwa ajili ya uchambuzi na idhini.

vi. Usanifu hafifu wa baadhi ya miradi inayoendelea, na hivyo kusababisha mabadiliko ya mawanda, ongezeko la gharama na muda wa utekelezaji. Katika kukabiliana na hili, Wizara na Taasisi za Umma zinaelekezwa kuhakikisha usanifu wa kina unafanywa kwa kuzingatia vigezo vyote vilivyoainishwa kwenye mwongozo wa uchambuzi wa miradi.

vii. Baadhi ya wawekezaji ambao hawana mitaji ya kutosha hivyo kusababisha baadhi ya miradi kutotekelezwa kwa wakati. Ili kukabiliana na hali hii, upekuzi wa kina ufanyike kwa kampuni zinazowania zabuni ili kupata kampuni zenye sifa stahiki.

viii. Kutokuwa na mpango endelevu wa utekelezaji wa miradi (sustainability plan). Katika kukabiliana na hili, Tume ya Mipango inazielekeza Wizara na Taasisi zote za Umma zinazohusika na utekelezaji wa miradi ya kielelezo na kimkakati kuandaa mpango wa matumizi endelevu (Sustainability Plan) ya miradi husika na kuiwasilisha Tume ya Mipango kwa ajili ya uchambuzi na idhini.

## 4.4. Ufuatiliaji na Tathmini kwa Mwaka 2024/25

Katika mwaka 2024/2025, Serikali kupitia Tume ya Mipango kwa kushirikiana na Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa na itafanya Ufuatiliaji, Tathmini na kutoa wa taarifa kupitia NPMIS. Serikali inapanga kufuatilia na kutathmini miradi 150 ambayo itatengewa fedha katika mwaka wa fedha 2024/25. Taarifa zitakazowasilishwa zitajumuisha: taarifa za utekelezaji wa miradi na program za maendeleo za kila robo mwaka; taarifa za mwaka za utekelezaji wa viashiria vilivyoainishwa kwenye Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Pili wa Maendeleo wa miaka Mitano; na taarifa za ufuatiliaji na tathmini. Taarifa za ufuatiliaji na Tathmini zitaandaliwa kwa kuzingatia viashiria vilivyoainishwa katika Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Miaka Mitano 2021/22 - 2025/26. Aidha, Wizara zitapaswa kuwasilisha mipango ya mwaka ya ufuatiliaji, mpango kazi wa mwaka pamoja na mpango wa matumizi ya fedha.

Kwa mwaka 2024/2025, Serikali kupitia Tume ya Mipango imepanga kusimamia kikamilifu zoezi la Ufuatiliaji na Tathmini ya Mpango wa Maendeleo kuleta ufanisi na thamani ya uwekezaji. Kuhakikisha ufuatiliaji na tathmini unaleta matokeo yaliyopangwa, Serikali kupitia Tume ya Mipango inatarajia kufanya yafuatayo:

i. Kuendelea kuboresha Mfumo wa kielekroniki wa Kitaifa wa Usimamizi wa Miradi ya maendeleo (National Project Management Information System - NPMIS) ili uweze kujumuisha moduli zote zinazohusu miradi ya maendeleo hususan moduli za ufuatiliaji na tathmini;

ii. Kuendelea kutoa mafunzo kwa watekelezaji na waratibu wa Miradi kuhusu mbinu na nyenzo za ufuatiliaji na tathmini pamoja na matumizi ya mfumo wa NPMIS

iii. kuhakikisha Sekta zote zinatumia mfumo huu ipasavyo ili kutimizia malengo ya miradi na shabaha zilizowekwa kwa ngazi zote (yaani; process, output na outcome);

iv. Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya robo mwaka na mwaka mzima kwa miradi na programu za maendeleo zinazoanza na zinazoendelea ambazo zitapewa fedha za utekelezaji wake katika mwaka 2024/25;
v. Kutoa mafunzo kwa lengo la kujenga uwezo kwa watekelezaji wa miradi na programu za maendeleo wa kuchambua miradi ili kuongeza ufanisi katika uandaaji wa nyaraka za miradi;
vi. Kuendelea kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo na kufuatilia na kutathmini mchango wake;
vii. Kufanya mapitio ya Mpango wa Tatu wa Maendeleo wa Taifa wa Miaka Mitano 2021/22 – 2025/26.

### 4.4.1. Misingi na Mbinu za Ufuatiliaji na Tathmini katika Mwaka 2024/2025

Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo wa Mwaka 2022 unazitaka Wizara, Idara zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi na Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa kuzingatia maelekezo kuhusu misingi na mbinu kama zilivyoainishwa

Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathmini umeainisha mfumo wa kupatika/kutoa taarifa za utekelezaji kwa lengo la kuwezesha watunga sera, wafanya maamuzi na wadau muhimu kufahamu mwenendo wa utekelezaji wa mipango, miradi na programu za maendeleo kwa kuzingatia hatua iliyofikia pamoja na mafanikio na changamoto ya utekelezaji wa malengo.

### 4.4.2. Matokeo ya Ufuatiliaji na Tathmini

Matokeo ya ufuatiliaji na tathmini katika utekelezaji wa programu na miradi ya maendeleo yatabainisha kiwango cha mafanikio yaliyopatikana, mafanikio yaliyofikiwa, changamoto zilizojitokeza, na kutoa ushauri wa mbinu bora za utekelezaji zinazopaswa kufuatwa. Hivyo, Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala wa Serikali, Taasisi, Mashirika ya Umma, Sekretarieti za Mikoa, na Mamlaka za Serikali za Mitaa zinazohusika na shughuli za ufuatiliaji na tathmini zinapaswa kutoa mrejesho kwa wadau wote kuhusiana na matokeo yaliyopatikana ili kuhakikisha kuna uelewa mpana wa hali ya utekelezaji wa mpango.

Ili kutathmini ufanisi na thamani ya uwekezaji uliofanywa katika miradi na programu mbalimbali za maendeleo, Serikali na wadau watahakikisha taarifa za ufuatiliaji na tathmini na matokeo ya hatua za utekelezaji zilizofikiwa na viashiria vya uchumi na maendeleo ya jamii vinafungamanishwa. Hii itahakikisha kuwa matokeo ya miradi na programu yanachambuliwa katika mtazamo mpana zaidi unaohusisha athari za kiuchumi na kijamii, hivyo kutoa picha kamili ya namna gani miradi na programu zinaathiri maisha ya wananchi na uchumi wa nchi.

### 4.4.3. Mgawanyo wa Majukumu katika Ufuatiliaji na Tathimini

Ufuatiliaji na Tathmini utazingatia ushirikishwaji mpana wa wadau muhimu katika utekelezaji wa Mpango. Aidha, mgawanyo wa majukumu kama ulivyofafanuliwa katika Mwongozo wa Kitaifa wa Ufuatiliaji na Tathmini ya Miradi ya Maendeleo utakuwa kama ifuatavyo:

i. Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu: Kamati ya Kitaalamu ya Makatibu Wakuu ni chombo cha maamuzi kitakachopokea taarifa za Ufuatiliaji na Tathmini ya miradi ya maendeleo. Kamati hii itapokea taarifa za U&T kwa kipindi cha nusu mwaka na mwaka.

ii. Wizara yenye dhamana na Mipango: Wizara yenye dhamana na Mipango itakuwa na jukumu la kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa mfumo wa ufuatiliaji na tathmini kupitia Tume ya Mipango. Aidha, Wizara itachukua hatua stahiki zinazohusisha upatikanaji wa rasimali fedha kwa ajili ya masuala ya U&T;

iii. Wizara za Kisekta (MDAs): Wizara za kisekta kupitia Kitengo cha U&T zitakuwa na jukumu la kuratibu na kusimamia shughuli zote za ufuatailiaji na tathmini. Hii itajumuisha uainishaji wa gharama na utekelezaji wa bajeti kwa kuzingatia Mipango Mkakati, shabaha na malengo pamoja na jitihada nyingine mbalimbali za utekelezaji wa majukumu ya taasisi husika;

iv. Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa: Taasisi hizi ni muhimu katika utekelezaji hususan katika usimamizi na utoaji wa taarifa za utekelezaji wa siku hadi siku;

v. Kamati za Maendeleo ya Kata: Kamati hizi zinaunda vikundi muhimu vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika ngazi ya chini ambao hutoa taarifa ya utekelezaji moja kwa moja katika Mamlaka za Serikali za Mitaa;

vi. Kamati za Maendeleo ya Kijiji/Mitaa: Kamati hizi zinaunda vikundi muhimu vya utekelezaji wa miradi ya maendeleo ambao hutoa taarifa za utekelezaji katika kamati za maendeleo za Kata; na

vii. Taasisi za Utawala Bora (Role ya Oversight bodies): Mkaguzi wa Ndani Mkuu wa Serikali na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali watakagua uzingatiwaji wa Mwongozo wa Ufuatiliaji na Tathimini wakati wa ukaguzi wa utendaji wa taasisi za umma. Watawajibika kukagua namna Taasisi na Wizara zinavyozingatia Mwongozo huu.

Mgawanyo huu wa majukumu unategemewa kutoa nafasi kwa kila mdau kutoa mchango wake katika ufuatiliaji na tathmini na hivyo kuimarisha uwazi na uwajibikaji.

## 4.5. Vihatarishi na Mikakati ya Kukabiliana Navyo kwa Mwaka 2024/2025

Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2023/24, ulikabiliwa na vihatarishi mbalimbali vilivyohitaji mikakati madhubuti ya kukabiliana navyo. Vihatarishi hivi vilijumuisha changamoto za kiutendaji, mifumo ya kitaasisi, na vihatarishi vilivyotokana na mazingira ya nje yasiyo ya kudhibitiwa na Serikali.

Vihatarishi hivyo ni pamoja na: ufinyu wa rasilimali fedha za utekelezaji wa mpango; ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika utekelezaji; upotevu wa mapato kutokana biashara za kimtandao; mabadiliko ya

viwango vya riba katika masoko ya fedha; masuala ya kimazingira; na vitendo vya rushwa na uadhirifu. Katika kukabiliana na hilo hatua mbalimbali zilichukuliwa ikiwa ni pamoja na: kuendelea na mikakati ya kuongeza wigo wa mapato pamoja na kutumia vyanzo mbadala vya ugharamaiaji wa miradi; kuhamasisha sekta binafsi kushiriki katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa kutumia taratibu mbalimbali ikiwemo utaratibu wa ubia wa sekta ya umma na binafsi; kujumusiha masuala ya mzingira na mabadiliko ya tabia nchi katika miradi inayoibuliwa.

Katika kuhakikisha malengo ya Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2024/25 yanafikiwa kwa ufanisi na kuleta matokeo chanya, Mpango huu umezingatia Mwongozo wa Kuandaa Mfumo wa Usimamizi wa Vihatarishi katika Sekta ya Umma wa Mwaka 2012. Serikali itahakikisha utekelezaji wa Mpango unaenda sambamba na utekelezaji wa mikakati ya kukabiliana na vihatarishi vinavyoweza kujitokeza. Vihatarishi hivi vinaweza kugawanywa katika makundi matatu: vihatarishi vya muda mfupi, muda wa kati, na muda mrefu, ambavyo vinaweza kusababisha mradi kutotekelezwa, kutekelezwa chini ya kiwango, kuongezeka kwa gharama, au kutokamilika kwa wakati. Aidha, vihatarishi hivi vimegawanyika katika makundi mawili: vihatarishi vya ndani vitakavyotokana na utendaji au mifumo ya Serikali na vihatarishi vya nje vitakavyotokana na masuala yaliyoko nje ya udhibiti wa Serikali.

### 4.5.1 Vihatarishi vya Ndani na Mikakati ya Kukabiliana Navyo

Vihatarishi vya ndani ni uwezekano wa matukio yanayoweza kujitokeza ambayo udhibiti wake upo ndani ya Mamlaka ya nchi. Matukio hayo yakiachwa yatokee yanaweza kuathiri utekelezaji wa Mpango. Matukio hayo ni pamoja na:

Upatikanaji mdogo wa rasilimali fedha: kutofikiwa kwa malengo ya makusanyo ya rasilimali fedha za kutosha na kwa wakati ni moja ya kihatarishi kinachoweza kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Katika kukubailiana na hili, Serikali imejipanga kuendelea kubuni vyanzo vipya vya mapato; kuimarisha sera za ukusanyaji na usimamizi wa mapato ikiwemo kuhakikisha kila mfanyabiashara anatoa risiti ya kielektroniki anapouza na mnunuzi anadai risiti anaponunua bidhaa au huduma; Kuongeza wigo wa walipa kodi kwa kuhamasisha sekta isiyo rasmi kujumuishwa katika mfumo rasmi wa ulipaji kodi; Kudhibiti upotevu wa mapato kwa kusimamia ipasavyo mifumo ya ukusanyaji, ikiwemo Mfumo wa Serikali wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato (Government Electronic Payment Gateway - GePG).

Ushiriki mdogo wa sekta binafsi: Mafanikio ya utekelezaji wa mpango unategemea ushiriki chanya wa sekta binafsi katika maeneo ya kipaumbele ya Mpango. Ushiriki mdogo wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ni kihatarishi kinachopelekea kutofikiwa kwa

malengo ya Mpango. Hatua za kukabiliana na kihatarishi hiki ni pamoja na: kuendelea kushirikisha Sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kuendelea kuboresha miundombinu wezeshi katika maeneo mapya ya uwekezaji; na kuvutia ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi kwa utaratibu wa ubia baina ya sekta ya umma na sekta binafsi (PPP).

Upotevu wa mapato ya Serikali yanayotokana na biashara mtandao; Matumizi mabaya ya teknolojia yanaweza kuathiri utekelezaji wa mpango. Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi ya kidigitali katika ukusanyaji wa kodi na kudhibiti upotevu wa mapato kwa kuboresha usimamizi wa mifumo ya kisheria iliyopo.

Mabadiliko ya viwango vya riba katika soko la fedha la ndani: Mabadiliko ya viwango ni moja ya kihatarishi kinachoweza kukwamisha utekelezaji wa Mpango. Katika kukabiliana na kihatarishi hiki, Serikali itaendelea kutekeleza Sera za fedha zitakazowezesha viwango vya riba kuwa himilivu na kuimarisha soko la fedha la ndani.

Uharibifu wa mazingira kutokana na shughuli za binadamu: Shughuli za binadamu huweza kuathiri mazingira na hivyo kusababisha uzalishaji duni katika uchumi. Serikali itaendelea kuhamasisha matumizi sahihi ya teknolojia katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo; kutoa elimu kwa wananchi juu ya umuhimu wa kutunza mazingira; na kudhibiti uharibifu wa uoto wa asili na bioanuai.

Vitendo vya rushwa na ubadhilifu wa rasilimali: Rushwa na ubadhilifu ni adui wa maendeleo na wa haki kama isipowekewa mikakati ya kukabiliana nayo. Rushwa na ubadhilifu wa mali ya umma inaweza kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Hivyo, Serikali itaendelea kuimarisha utekelezaji wa sheria ya mapambano dhidi ya rushwa; kuweka mazingira wezeshi ya biashara yaliyoboreshwa na yenye uwazi ili kuruhusu sekta binafsi kushamiri na kurasimisha sekta isiyo rasmi; kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Udhibiti wa Mifumo ya Kielektroniki ya Usimamizi wa Fedha za Umma; kuimarisha usimamizi na udhibiti wa mifumo ya taarifa ya kielektroniki ya Serikali; na kuimarisha usalama wa maeneo ya kuhifadhia kumbukumbu mbalimbali (Data recovery sites).

### 4.5.2. Vihatarishi vya Nje na Mikakati ya Kukabiliana Navyo

Vihatarishi vya nje ni uwezekano wa matukio yanayoweza kujitokeza ambayo ufumbuzi wake upo nje ya uwezo wa Serikali wa moja kwa moja na hivyo kuathiri utekelezaji wa Mpango. Vihatarishi hivyo ni pamoja na:

Mabadiliko ya tabia ya nchi, majanga ya asili na magonjwa ya mlipuko: matukio haya ni kama matetemeko, ongezeko la joto duniani, mafuriko, ukame na magonjwa ya mlipuko. Matukio haya yasipothibitiwa huathiri uzalishaji na hatimaye utekelezaji wa Mpango wa maendeleo kuathirika. Serikali imejipanga kukabiliana na kihatarishi hiki kwa kuboresha mifumo

ya kuzuia na kukabiliana na majanga; kuimarisha mifuko ya maafa; kutekeleza na kuendelea kuridhia itifaki za kimataifa kuhusu utunzaji wa mazingira na mabadiliko ya Tabianchi; na kuimarisha utekelezaji wa Sera ya Taifa ya Mazingira ya Mwaka 2021.

Mdororo na mitikisiko ya kiuchumi duniani: Mtikisiko wa kiuchumi duniani husababisha kupungua kwa mahitaji ya bidhaa na huduma katika masoko ya nje na hivyo kuchangia kupungua kwa fedha za kigeni zitokanazo na uuzaji wa bidhaa nje na wawekezaji wa mitaji ambao ni muhimu katika kugharamia miradi ya maendeleo. Mikakati ya kukabiliana na kihatarishi hiki ni pamoja na kuimarisha mikakati ya kisera ili kukabiliana na mabadiliko ya kiuchumi duniani; kuendelea kuhamasisha ujenzi wa viwanda vinavyotumia malighafi za ndani na kuzalisha bidhaa zinazotumiwa na watu wengi nchini; kuimarisha ubora wa bidhaa zinazozalishwa nchini ili kuhimili ushindani katika masoko ya kimataifa; na kuweka mazingira wezeshi kwa wawekezaji wa viwanda vinavyozalisha bidhaa kwa kutumia teknolojia na malighafi za ndani ili kupunguza uagizaji wa bidhaa kutoka nje.

Migogoro na hali ya siasa inayojitokeza kwa nchi jirani, kikanda na kimataifa: Migogoro inapojitokeza inaweza kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo kama isipozuiwa mapema. Mikakati ya kukabiliana na kihatarishi hiki ni pamoja na kuendelea kuimarisha ushirikiano na nchi Jirani, kikanda na kimataifa ili kukuza masoko kwa ajili ya bidhaa zinazozalishwa viwandani.

Kuongozeka kwa kasi ya mabadiliko ya teknolojia: Kasi ya mabadiliko ya teknolojia duniani inayojitokeza inaweza kuathiri utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo. Hivyo, ili kukabliana na kasi hiyo, Serikali itaendelea kuboresha mifumo ya kisheria, kisera na kitaasisi ili iendane na mabadiliko ya teknolojia duniani; na kuendelea kuimarisha mikakati ya kuongeza ujuzi, uhawilishaji wa teknolojia na kuhamasisha ubunifu wa teknolojia kwa wataalam wa ndani na kubuni vyanzo vipya vya mapato kwa ajili ya kugharamia shughuli za maendeleo.

**Jedwali Na. 4.1: Miradi Iliyofuatiliwa katika Mwaka 2023/24**

| Mkoa | Sekta | Idadi ya Miradi | Jina la Mradi |
|---|---|---|---|
| Dar es Salaam | Ujenzi | 3 | 1. Ujenzi wa Miundombinu ya Mabasi Yaendayo Haraka Awamu ya II na Awamu ya III |
| | | | 2. Ujenzi wa Barabara za Kupunguza Msongamano Jijini Dar es Salaam (km 138.5) |
| | | | 3. Ujenzi na Ukarabati wa Majengo ya Serikali |
| | Uchukuzi | 3 | 4. 4. Kuboresha Shirika la Ndege Tanzania |
| | | | 5. Ujenzi wa Reli ya Kati kwa Kiwango cha Kimataifa (Standard Gauge Railway - SGR) |
| | | | 6. Uboreshaji wa Bandari ya Dar es Salaam |
| | OR- | 1 | 7. Mradi wa Uendelezaji wa Jiji la Dar es Salaam (DMDP) |
| | Maji | 1 | 8. Uboreshaji wa Huduma ya Maji eneo la DAWASA |
| | Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia | 1 | 9. Upanuzi na Ukarabati wa Chuo Kikuu Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (DUCE) |
| | Nishati | 1 | 10. Usambazaji wa Gesi Asilia Mikoa ya Dar es Salaam, Mtwara, Lindi na Pwani |
| | Mambo ya Ndani | 1 | 11. Vitambulisho vya Taifa |
| | Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki | 1 | 12. Ujenzi wa Majengo ya Ofisi (Upanuzi wa Uboreshaji wa Miundombinu ya Chuo cha Diplomasia) |
| | Afya | 1 | 13. Mradi wa Hospitali ya Rufaa Mkoa Mwananyamala |
| | Viwanda | 1 | 14. Kiwanda cha Europe INC Industries Limited |

| Mkoa | Sekta | Idadi ya Miradi | Jina la Mradi |
|---|---|---|---|
| Pwani | Uchukuzi | 1 | 15. Ujenzi wa Bandari Kavu ya Kwala katika Eneo la Ruvu |
| | OR- | 1 | 16. Ujenzi wa Kongane la Viwanda (Industrial Park) – Kwala |
| | Mipango na Uwekezaji Viwanda | 1 | 17. Kiwanda cha Sukari Bagamoyo (Bagamoyo Sugar LTD) |
| Morogoro | Nishati | 1 | 18. Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere (MW 2,115) |
| | Maji | 1 | 19. Ujenzi wa Bwawa la Kidunda |
| | Ujenzi | 2 | 20. Ujenzi wa barabara ya Rudewa – Kilosa |
| | | | 21. Ujenzi wa barabara ya Kidatu - Ifakara |
| | Kilimo | 1 | 22. Mradi wa Kudhibiti Sumukuvu (Ujenzi wa ghala) |
| | Viwanda | 2 | 23. Ujenzi wa Kiwanda na uendelezaji wa shamba la miwa - Mkulazi |
| | | | 24. Programu ya upanuzi wa kiwanda na mashamba – Mtibwa sugar |
| | Utawala bora | 2 | 25. Ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri – Kilosa |
| | | | 26. Ujenzi wa jengo la Halmashauri ya Morogoro Vijijini |
| | Afya | 1 | 27. Ujenzi wa Hospitali ya Wilaya ya Morogoro |

| Mkoa | Sekta | Idadi ya Miradi | Jina la Mradi |
|---|---|---|---|
| Iringa | Ujenzi | 2 | 28. Ujenzi wa barabara ya barabara ya Iringa – Dodoma |
| | | | 29. Ukarabati na Upanuzi wa Kiwanja cha Ndege Iringa |
| | Afya | 2 | 30. Ujenzi wa miundombinu ya maji, vyoo na ukarabati wa wodi katika Zahanati ya Ikokoto |
| | | | 31. Ujenzi wa Kituo cha Afya Itamba |
| | Elimu | 13 | 32. Ujenzi wa shule mpya ya Msingi Idumulavanu |
| | | | 33. Ujenzi wa shule mpya ya Msingi Mseke |
| | | | 34. Ujenzi wa shule mpya ya sekondari mboliboli |
| | | | 35. Ujenzi wa Mabweni shule ya Sekondari Lukosa |
| | | | 36. Ujenzi wa shule mpya ya Wasichana |
| | | | 37. Ujenzi wa matundu ya vyoo shule ya Msingi Kitumbuka |
| | | | 38. Ujenzi wa shule mpya ya msingi Ikweha |
| | | | 39. Ujenzi wa shule mpya ya msingi Ikweha |
| | | | 40. Ujenzi wa shule mpya ya msingi Tungamalenga |
| | | | 41. Ujenzi wa bweni shule ya Sekondari Mawelewele |
| | | | 42. Ujenzi ya shule Mpya ya msingi Kitwiru |
| | | | 43. Ujenzi wa bweni shule ya sekondari Mgololo |
| | | | 44. Ujenzi wa shule mpya ya msingi Kisalasi. |

| Mkoa | Sekta | Idadi ya Miradi | Jina la Mradi |
|---|---|---|---|
| Dodoma | Kilimo | 2 | 45. Kuongeza Uhifadhi wa Nafaka |
| | | | 46. Kudhibiti Sumukuvu - Dodoma |
| | Maji | 2 | 47. Ujenzi wa Bwawa la Farkwa |
| | | | 48. Ujenzi wa Bwawa la Itaswi |
| | Utawala bora | 2 | 49. Ujenzi wa Makao Makuu ya Mahakama |
| | | | 50. Ujenzi wa majengo ya wizara na taasisi za Serikali katika mji wa Serikali – Mtumba |
| | Elimu | 1 | 51. Programu ya Lipa kulingana na Matokeo katika Sekta ya Elimu – EP4R |
| | Ujenzi | 2 | 52. Kiwanja cha Ndege cha Kimataifa cha Msalato |
| | | | 53. Ujenzi wa Barabara ya mzunguko wa nje ya Jiji la Dodoma (Km 112.3) |
| | Uchukuzi | 1 | 54. Ununuzi wa Rada, Vifaa na Ujenzi wa Miundombinu ya Hali ya Hewa |
| | Viwanda | 1 | 55. Kiwanda cha mvinyo cha ALKO VINTAGES |

| Mkoa | Sekta | Idadi ya Miradi | Jina la Mradi |
|---|---|---|---|
| Manyara | Uchukuzi | 1 | 56. Ujenzi wa Stendi ya Mabasi – Katesh, Hanang |
| | Afya | 1 | 57. Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara |
| | Utawala Bora | | 58. Ujenzi wa Ofisi za Mikoa za Uhamiaji |
| | | | 59. Ujenzi wa jengo la Halmashauri – Mbulu TC |
| | | | 60. Ujenzi wa jengo la Halmashauri – Babati DC |
| | | | 61. Ujenzi wa jengo la Halmashauri – Kiteto DC |
| | | | 62. Ujenzi wa jengo la Halmashauri – Simanjiro DC |
| | | | 63. Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mkuu wa Wilaya – Kiteto |
| | | | 64. Ujenzi wa Ofisi ya RPC |
| | Kilimo | 2 | 65. Kudhibiti Sumukuvu – Babati |
| | | | 66. Kudhibiti Sumukuvu - Kiteto |
| | Maji | 8 | 67. Uchimbaji wa visima 9 katka vijiji vya Endadosh, Mwikantsi, Gijedabung, Riroda, Ayasanda, Endamaghy, Duru, Endagwe na Hewasi. |
| | | | 68. Mradi wa Maji Magara, Boay na Hosahn |
| | | | 69. Mradi wa Maji Mogitu/Gehandu awamu ya I |
| | | | 70. Kuongeza mkondo wa maji kutoka Mayoka – Minjingu Kwenda Kakoi |
| | | | 71. Mradi wa Maji Nadonjukin, Engonongoi na Terrat |
| | | | 72. Mradi wa Maji Langai na Kambi ya Chokaa |
| | | | 73. Mradi wa Maji Ng’orati na Maretadu Juu |
| | | | 74. Mradi wa Endahagiachan |

| Mkoa | Sekta | Idadi ya Miradi | Jina la Mradi |
| --- | --- | --- | --- |
| Simiyu | Ujenzi | 1 | 75. Barabara ya Mwigumbi Maswa – Bariadi Lamadi (km 171.8) na Maswa by pass (km 11.3) |
| | MAJI | 1 | 76. Mradi wa maji wa ziwa Victoria – Busega, Simiyu (kata za Lamadi na Mkula) |
| Mwanza | Ujenzi | 2 | 77. Daraja la J.P. Magufuli (Kigongo – Busisi) km 3.2 na barabara unganishi km 1.66 |
| | | | 78. Mradi wa ujenzi wa vivuko vipya |
| | Uchukuzi | 2 | 79. Mradi wa ujenzi wa jengo la abiria kiwanja cha ndege Mwanza |
| | | | 80. Ujenzi na ukarabati wa Meli |
| | Maji | 1 | 81. Mradi wa kuboresha huduma za maji katika jiji la Mwanza |
| | Viwanda | 3 | 82. Kiwanda cha kuzalisha Dawa za Binadamu cha Prince Pharmaceuticals – Buhongwa |
| | | | 83. Kiwanda cha kuzalisha Mvinyo cha Mwanza Quality Wines LTD |
| | | | 84. Kiwanda cha Kuzalisha nguo cha Mwanza Textile Limited |
| Tanga | Uchukuzi | 1 | 85. Mradi wa uboreshaji wa bandari katika mkoa wa Tanga awamu ya pili |
| | Nishati | 1 | 86. Mradi wa usambazaji wa nishati ya umeme Vijijini Nishati |
| | Viwanda | 2 | 87. Amboni spinning Mill large-Urowa Pongwe |
| | | | 88. Upanuzi wa kiwanda cha cementi – Maweni Tanga |

| Mkoa | Sekta | Idadi ya Miradi | Jina la Mradi |
|---|---|---|---|
| Arusha | Nishati | 1 | 89. Mradi wa uimarishaji wa gridi ya Taifa (National Grid Stabilization) |
| | Maji | 1 | 90. Mradi wa maji na usafi wa mazingira Arusha |
| | Mawasiliano | 1 | 91. Mradi wa kimkakati wa mkongo wa Taifa wa Mawasiliano |
| Kilimanjaro | Maji | 1 | 92. Mradi wa uboreshaji wa maji Same –Mwanga - Korongwe |
| | Viwanda | 2 | 93. Mradi wa kiwanda cha uzalishaji sukari-(TPC)-Moshi- Kilimanjaro |
| | | | 94. Mradi wa Kiwanda cha ngozi Kilimanjaro |
| Mara | Maji | 1 | 95. Ujenzi/ukarabati na upanuzi wa miradi ya maji katika miji mikuu ya Wilaya, miji midogo na miradi ya kitaifa |
| Lindi | Uvuvi | 1 | 96. Ujenzi wa bandari ya uvuvi Kilwa |

**Ofisi ya Rais, Tume ya Mipango**
**Jengo la Kambarage Ghorofa ya 9,**
**1 Mtaa wa Kambarage**
**S. L. P. 1324**
**41104 Tambukareli, Dodoma**

**www.planning.go.tz**

**Tume ya Mipango Tanzania** **@planning_tz** **@planning_tz** **@planningtz**